

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Kumi na Sita - Tarehe 25 Juni, 2010

(Mkutano ulanza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Katiba na Sheria kwa Mwaka 2010/2011.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE - MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:

Taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MHE. SHOKA KHAMIS JUMA (K.n.y. MHE. FATUMA MUSSA MAGHIMBI - MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA KATIBA NA SHERIA):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA, NA WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Randama ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

NAIBU WAZIRI WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Randama ya Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 111

Walimu kuondoka bila ruhusa katika vituo vyta Kazi

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA aliuliza:-

Kwa kuwa kuna baadhi ya walimu ambao huamua kuondoka katika vituo vyao vyta kazi bila sababu maalum na hivyo kuongeza uhaba wa walimu katika shule zetu:-

Je, Serikali inatoa kauli na adhabu gani kwa walimu hawa ili tabia hii isiendelee kujenga mizizi?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchaya, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, walimu kama walivyo watumishi wengine wa umma wanapaswa kuwepo kwenye vituo vyao vyta kazi wakati wote. Endapo kuna haja ya watumishi hao kutokuwepo vituoni kwa sababu yoyote ile kama vile ugonjwa, likizo au masomo, watumishi hao wanapaswa kupata kibali cha mwajiri cha kuondokea katika kituo hicho.

Hata hivyo ni kweli kuwa baadhi ya walimu wamekuwa wakiondoka vituoni bila ruhusa ya mwajiri hususan kwenda masomoni bila kibali cha mwajiri. Mtumishi yeoyote wa umma anayeondoka kituoni bila kibali cha mwajiri wake anakuwa ametenda kosa na anastahili kuchukuliwa hatua za nidhamu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua zinazochukuliwa dhidi ya watumishi wa umma wakiwepo walimu wanaoondoka vituoni bila ruhusa maalum ni kuwa huchukuliwa hatua za kinidhamu kwa kuzingatia, Sheria, Kanuni na taratibu za uendeshaji katika utumishi wa umma.

Kwa walimu Mamlaka yao ya nidhamu ni Tume ya Utumishi wa Umma, Idara ya Utumishi wa Walimu katika eneo husika yaani Ofisi ya Wilaya/Mkoa. Hivyo inapothibitika kuwa mwalimu ametoroka kazini (hayupo katika kituo chake cha kazi bila kibali) kwa zaidi ya siku tano kama inavyobainishwa katika Kanuni ya 42 Jedwali la

kwanza “A” kipengele cha nne atachukuliwa hatua za nidhamu ambazo ni pamoja na kupewa adhabu ya kufukuzwa kazi, kushushwa cheo na kushushwa mshahara.

Mheshimiwa Spika, kabla ya hatua hizo kuchukuliwa utaratibu ufuatao unazingatiwa:-

Kwanza, mtumishi kufunguliwa Hati rasmi ya Mashtaka inayokidhi matakwa ya kisheria kwa mujibu wa Kanuni ya 44(3).

Mtumishi kupewa muda wa kutosha wa kujitetea.

Hatua ya tatu, uchunguzi kufanywa kwenye tuhuma husika kama mtuhumiwa amekana mashtaka kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, walimu wanaondoka kwenye vituo vyao vya kazi bila kibali wamekuwa wakichukuliwa hatua za kinidhamu. Mfano katika Wilaya ya Masasi ambapo lipo Jimbo la Lulindi walimu wanne walichukuliwa hatua za kinidhamu katika mwaka 2009/2010. (*Makofi*)

MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya kuridhisha ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa tatizo hili ni kubwa sana katika Jimbo la Lulindi. Unafika mahali unakuta shule ya Sekondari yenyé Kidato cha Nne kuna mwalimu mmoja ama wawili. Je, Serikali iko tayari sasa kutengeneza utaratibu maalum ambao utasaidia walimu hawa wasiondoke katika maeneo haya ili wanafunzi wale waweze kupata elimu yao iliyokamilika?

Mheshimiwa Waziri yuko tayari kufanya ziara katika Jimbo la Lulindi ili athibitishe haya ambayo ninayasema hapa Bungeni? Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hatua mbali mbali zimechukuliwa na Serikali ili kuhakikisha kwamba walimu au watumishi wa Serikali wanakuwa katika vituo vyao. Hatua ya kwanza ni kuhakikisha kwamba mshahara wa mtumishi ye yote wa mtumishi wa Serikali wakiwemo walimu unatoka tarehe moja tu kuanzia tarehe 25 mshahara unatoka.

Kwa hiyo karibuni nchi nzima utaratibu huu umefanikiwa sana kuanzia tarehe 25 walimu na wafanya wengine wanaenda kuangalia mishahara yao benki na hatua hii mimi nasema kwamba kwa upande wetu tumefanikiwa sana badala ya walimu kwenda kukaa Wilayani kwa muda mrefu kungoja kupata mishahara yao. Hilo la kwanza hatua ambayo tumechukuwa Serikali.

Hatua ya pili, kuwapanga walimu katika shule mbalimbali. Hatua hii tumeichukua kuanzia mwaka uliopita kwamba tunapopanga walimu tunapeleka na mishahara yao moja kwa moja kwenye Halmashauri husika. Kwa hiyo, walimu wengi ambao wamepangiwa vituo vyao kwa mwaka 2009/2010 wamekwenda kwenye vituo

vyao kwa sababu akienda kuripoti kwingine hakuti mshahara wake. Kwa hiyo, hilo limefanikiwa sana kwa upande mmoja au mwingine.

Kuhusu uchache wa walimu mwaka huu tunategemea kupata walimu watano kwa kila shule ya sekondari na tukiwapanga tunapeleka na mshahara wao huko huko. Kwa hiyo, mshahara wao ukisha kwenda huko Lulindi akitaka kubadilisha kuja Dar es Salaam inakuwa ngumu sana kubadilisha kwenda katika kituo kingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la pili kutembelea jimbo la Mheshimiwa Kumchaya, Mheshimiwa Kumchaya anajua kabisa kwamba Bunge linavunjwa tarehe 16 na kipindi hicho kila mmoja anaenda kwenye kampeni, itakuwa siyo rahisi kumdanganya hapa kwamba nitaenda kutembelea kwenye jimbo lake kwa kipindi hiki kifupi. Labda aniombee tu kwamba nirudi tena katika nafasi hii. (*Makof*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika. Nitauliza swali tu la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Swali langu linahusu uhaba wa walimu hasa katika shule zetu za Sekondari ambao unasababishwa na sababu mbalimbali.

Lakini kwa ujumla wake kuna baadhi ya Shule kwa mfano jimboni Kongwa ambapo walimu ni wachache kufikia wawili hadi watatu kwa shule ambayo ina *Form One* mpaka *Form Four*. Ametuahidi kwamba Serikali itajitahidi kupata angalau wastani wa walimu watano kwa kila sekondari ambao bado ni wachache. Sasa swali langu lilikuwa linasema hivi kwamba tumeshaingia katika makubaliano ya soko la pamoja la Afrika Mashariki ikiwa ni pamoja na ajira.

Je, Serikali haiwezi kuangalia na kukubali kuruhusu ajira za walimu wa sekondari kama katika nchi yetu ni chache angalau tukapata walimu kutoka nchi jirani iwe ni Burundi, Rwanda na Kenya?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, suala hili linazungumzika na tuko katika mazungumzo kuangalia uwezekano wa kupata hasa walimu wa Sayansi kutoka katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

MHE. GRACE S. KIWELU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna sababu nyingi zinazosababisha upungufu wa walimu katika mashule yetu na vyuo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikisha vyuo binafsi na shule binafsi katika kusomesha walimu kwa sababu walimu wengi wanatosmeshwa na Serikali na baada ya hapo wanakwenda kwenye shule binafsi na vyuo binafsi. Je, Serikali ina mpango gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI): Mheshimiwa Spika, hicho ndicho kinachofanyika sasa hivi Serikalini kwamba tunatosmeshwa walimu katika vyuo vikuu

binafsi na wengi tunawachukua kwenye ajira moja kwa moja Serikalini. Lakini kuna wachache ambao wanaenda kwenye shule binafsi na kutokana na soko huria siyo rahisi sana kuwabana hao walimu kwamba lazima waende Serikalini. Kwa hiyo, hata tukiwabana ina maana kwamba vyuo binafsi wanasona watoto wa Kitanzania. Sasa ukisema kwamba wasiende kufundisha huko itakuwa tumeingilia sana uhuru wa hizo shule binafsi.

Na. 112

Eneo lililotolewa na Kijiji cha Kihanga

MHE. BENITO W. MALANGALILA alijibu:-

Kwa kuwa kijiji cha Kihanga kilitoa ardhi yake kwa Idara ya Misitu na Nyuki iweke kitalu cha kuoteshea miche ya kupanda Shamba la *Sao Hill*:-

- (a) Je, kwa nini Serikali imeendelea kung'ang'ania eneo hilo la wananchi ikidai kuwa ni la kwake, jambo ambalo sio kweli?
- (b) Kwa kuwa wananchi wa eneo hilo huuliza maswali juu ya hatima ya eneo hilo lakini Mbunge wa eneo hilo anakosa majibu. Je, Serikali itamsaidiaje Mbunge kupata suluhu juu ya tatizo hilo?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, shamba la miti la *Sao Hill* lilianzishwa kwenye hifadhi ya *Sao Hill* (*Sao Hill Forest Reserve*) inayoundwa na hifadhi 13 za misitu ikiwa ni pamoja na *Irunda Forest Reserve*. Hifadhi hizi kwa pamoja zina ukubwa wa hekta 135,903 ambapo kati ya hizo takribani hekta 45,000 kwa sasa zimepandwa miti aina ya misindano na mikaratusi, hekta 48,200 ni maeneo ya misitu ya asili ambayo ni kwa ajili ya vyanzo vya maji, hekta 41,003 ni kwa ajili ya upanuzi wa upandaji wa miti na hekta 1,700 ni maeneo ya makazi na matumizi mengine. Kutokana na ukubwa wake, shamba la miti la *Sao Hill* limezungukwa na takribani vijiji 43 kikiwemo kijiji cha Kihanga kilichopo karibu kabisa na eneo la msttu wa kupanda wa Irunda lenye ukubwa wa hekta 289.94 ndani ya *Irunda Forest Reserve*, ambayo imehifadhiwa kisheria kwa Tangazo la Serikali Namba 224 la tarehe 23 Mei, 1958. Baada ya kutoa maelezo hayo, naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Benito William Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uongozi wa Wizara ulitembelea kijiji cha Kihanga tarehe 26 Januari, 2010 na kufanya mkutano na uongozi wa Kijiji. Lengo lilikuwa ni kutafuta ufumbuzi wa mgogoro baina ya msitu wa *Sao Hill* na Kijiji cha Kihanga kuhusu eneo

linalodaiwa kuwa lilitolewa na kijiji kwa ajili ya bustani ya miti miaka ya nyuma. Pia mkutano huo ulijumuisha Maofisa Ardhi na Misitu wa Wilaya ya Mufindi.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo, uongozi wa Kijiji cha Kihanga ulieleza bayana kuwa eneo la bustani linalodaiwa, lilirudishwa kwa wenyewe waliokuwa wametoa eneo hilo baada ya Miche Iliyokuwa imeoteshwa katika bustani hiyo kupandwa katika mashamba ya kwanza katika maeneo ya Kibao na Kigogo mwaka 1957 na 1958. Pia uongozi wa Kijiji cha Kihanga ulieleza kuwa uongozi wa Wilaya ya Mufindi na Mkoa wa Iringa ulishatoa maelezo ambayo yaliwatosheleza wananchi wa Kijiji cha Kihanga.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kuwa kijiji cha Kihanga kilianzishwa mwaka 1974 wakati wa operesheni ya vijiji. Wakati huo kijiji hicho kilikuwa na Kaya 350 na jumla ya wakazi 1,680, ambapo hivi sasa kijiji kina kaya 610 zenye jumla ya wakazi 2,955. Kutohana na ongezeko hili la watu katika vijiji vilivyoko karibu na misitu, wananchi wengi kwenye maeneo mbalimbali nchini wanakuwa na upungufu wa maeneo hasa ya kilimo na ufugaji. Hali kama hii na hususan pale zinapokuwepo kumbukumbu potofu, inasababisha migogoro ya kugombea maeneo ya hifadhi ya misitu iliyo karibu, kama ilivyojitekeza kwa suala la kijiji cha Kihanga.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Sasa kutokana na majibu yake ni kwamba Viongozi wa Wizara walikwenda kuongea na uongozi wa kijiji cha Kihanga, nadhani ilikuwa ni mwaka huu Januari. Lakini mimi nimefanya mkutano wa hadhara mwaka huu, bado wananchi wanalamikia Wizara ya Maliasili na Utalii kwamba lile eneo walilokuwa wameazimisha Wizara ili iweke kitalu pale, wao wanalihitaji. Pia swal la pili ni kwamba jirani na kijiji cha Kihanga kuna kijiji cha Ikomasa, kijiji kile kina mgogoro kama huu. Kwamba pale Wamasa kuna msitu wa asili, wakati wa ukoloni wakoloni waliweka mawe ya kutenganisha eneo lao la...

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge, lenga swal, sio maelezo.

MHE. BENITO W. MALANGALILA: Mheshimiwa Spika, swal; pale kijiji cha Wamasa, kuna mawe yaliyokuwa yamewekwa kutofautisha msitu wa asili wa *Mufindi Scape* na eneo la wananchi. Lakini Serikali imepanda miti nje kabisa ya yale mawe kuonesha kwamba imechukua ardhi ya wananchi. Sasa ni kwa nini, Serikali inawatendea hivi wananchi?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Benito Malangalila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa kusema kwamba wananchi bado wanalihitaji eneo hilo, mimi naopenda kumfahamisha kwamba nitamtuma tena Mkurugenzi wangu wa Misitu, aweze kuhakiki hali hiyo na kuona kwamba ni nini kitendeke kwa ajili ya hawa wananchi kama bado wanalihitaji eneo hilo. Kuhusu kijiji cha Homasa, ni kwamba napenda kusema kwamba tutakwenda kutazama hiyo sehemu na kuhakiki tena mipaka hiyo ya kuhusu kijiji hicho.

Napenda tu kuongeza kwa kusema kwamba kuna matukio mengi ya kuhusu malalmiko ya mipaka. Kwamba kuna mipaka imeingiliana kati ya mipaka ya hifadhi na mipaka ya baadhi ya vijiji. Jambo hilo sasa hivi ni mojawapo ambalo tunahakiki upya kila mpaka ili kuhakikisha kwamba haki inatendeka na kila mwanakijiji aweze kukaa sehemu ambayo anastahili kuwepo.

Na. 113

Shirikisho la vijiji la utunzaji mazingira ya Kuhifadhi ya Wanyamapor

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA (K.n.y. MHE. VITA R. KAWAWA) aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa vijiji vya Wilaya ya Namtumbo walihamasishwa kutenga eneo la Jumuiya ya Hifadhi la Wanyamapor katika utunzaji mazingira/wanyamapor na njia zao za misimu, ili wale nufaika na maliasili yao kwa njia mbalimbali kama vile uwindaji na kuwa na miradi mikubwa ya ufugaji nyuki na kurina asali na kwa kuwa hadi sasa hawajapatiwa leseni ya "AA" na badala yake ni kwamba ndani ya hifadhi hiyo waliyonza kwa miaka mingi yameibuka machimbo ya madini ya *uranium* kwa waliopata leseni/vibali kutoka Serikalini:-

(a) Wanyamapori na nyuki. Je, wananchi wa vijiji vilivyounda Jumuiya ya Mbarang'andu yenye vijiji vya Kitanda, Nambecha, Likuyuseka, Mchomoro na Kilimasera watafaidikaje kimapato moja kwa moja kutoka mradi wa uchimbaji *uranium*?

(b) Je, Serikali imejiandaaje katika Mkataba wa wachimbaji hao wakati wakiwa kwenye uzalishaji na wananchi/vijiji hivyo na Wilaya ya Namtumbo wenyewe maliasili yao wamewekwa katika kundi gani la mapato yatakayopatikana na mradi huu?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Vita Rashid M. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, naomba kutoa maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor (WMAs) huanzishwa na vijiji katika ardhi ya vijiji husika kwa ridhaa ya wananchi wenyewe, kwa kutenga ardhi kulingana na Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya kijiji. Ardhi iliyotengwa kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapor husimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya Kijiji Namba 5 ya mwaka 1999 pamoja na Kanuni za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor (WMAs).

Mheshimiwa Spika, eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor la Mbarang'andu linalosimamiwa na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor ya Mbarang'andu, lilitengwa mwaka 2003. Vijiji wanachama vinavyounda Jumuiya hiyo ambavyo ni Mchomoro, Kilimasera, Mterawamwahi, Songambele, Kitanda, Nambecha na Likuyuseka katika Wilaya ya Namtumbo vilianzisha eneo hilo kwa lengo la kuhifadhi wanyamapor ili waweze kunufaika moja kwa moja na rasilimali ya wanyamapor katika maeneo yao kwa mujibu wa Sheria na Sera ya Wanyamapor.

Mheshimiwa Spika, kulingana na utaratibu Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor iliyoidhinishwa hupatiwa haki ya matumizi ya Rasilimali ya Wanyamapor na siyo leseni. Aidha, haki ya matumizi hutolewa baada ya Jumuiya husika kutuma maombi kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapor na kukidhi vigezo na matakwa yaliyowekwa katika Kanuni za WMAs. Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor ya Mbarang'andu ilipata Haki ya Matumizi ya Rasilimali ya Wanyamapor kwenye eneo lake tarehe 29 Machi, 2010 baada ya kutekeleza matakwa na vigezo vyote husika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, naomba sasa kujibu swalii la Mheshimiwa Vita Rashid M. Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa madini bado haujaanza katika eneo la Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapor Mbarang'andu Wilayani Namtumbo. Hata hivyo, kulingana na Sheria husika ya Madini, sambamba na Tathmini ya Athari kwa Mazingira, yaani *Environmental Impact Assessment (EIA)* itakayofanyika kwenye eneo la Jumuiya ya Mbarang'andu na uchimbaji kamili kuanza, mgawanyo wa faida utakuwa umebanishwa ipasavyo.

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linaulizia juu ya uchimbaji wa madini ya *Uranium*, nilikuwa napenda kujua Serikali inaweza ikawaeleza wananchi wa mkoa wa Ruvuma uchimbaji huu utaanza lini? Swali la pili ni kwa kuwa, katika maeneo mengi sana ya uchimbaji wa madini kunakuwa na migogoro mingi sana. Je, Waziri atakuwa tayari kuwaeleza wananchi wa Wilaya ya Namtumbo na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla wajiandae kivipi ili kuepuka migogoro ambayo inaweza kujitekeza katika uchimbaji wa madini?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Devota Likokola, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la uchimbaji utaanza lini. Swali hilo mimi siwezi kuwa na jibu kwa sababu, uchimbaji huu utakuwa tayari kuanzwa baada ya ile tathmini ya mazingira itakapomalizika. Na tathmini ya mazingira haisimamiwi na Wizara yangu, inasimamiwa na Ofisi ya Mheshimiwa Makamu Wa Rais ambayo inahusika na mazingira.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu migogoro ya uchimbaji. Migogoro ya uchimbaji pia ni migogoro ya ardhi. Kwa sababu ni migogoro ya ardhi, sasa hivi tunazo Kamati ambazo tumeziunda tukishirikiana na Wizara zote zinazohusika kwa ajili ya kutatua migogoro ya namna hiyo pindi inapotokea. Wizara zinazohusika ambazo tunashirikiana katika kutatua migogoro mbalimbali ni Wizara yangu ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Mazingira, Wizara ya Mifugo, Wizara ya Kilimo pamoa na mikoa husika ambayo kwa wakati huo inakuwa katika migogoro.

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Wananchi wa vijiji vitano katika tarafa ya Makami, wameandaa jumuiya ya *WMA* iitwayo Endema, yenye jumla ya hekta 167,000. Wamejibidiisha wamesajili Jumuiya yao, wameandaa ofisi, wameandaa na watumishi na mipango ya matumizi bora ya ardhi pia wameandaa. Lakini kwa muda mrefu wamekuwa wakihangaika kupata *user rights* ili waweze kuanza hifadhi hiyo ya wanyamapori, lakini Wizara imekuwa na uzito wa kuwapa *user rights*.

Mheshimiwa Spika, swali kwa Mheshimiwa Waziri ni. Je, ni lini Serikali itawapa wananchi wa Makami, *user rights* kwa ajili ya *WMA* yao ya Endema?

WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kijiji cha Endema, wameanzisha *WMA* yao na imefikia hatua ya kupewa *user rights*, lakini kuna mgogoro uliojitekeza ambao umetufanya kwamba tusitishe kwanza kwa muda, kwa sababu, kawaida *WMAs* kila vijiji vinavyohusika vinachangia kutoa sehemu ya ardhi.

Sasa kwa upande wao katika kijiji hiki, ardhi ambayo ingeweza kutolewa, ina mgogoro kwa sababu ni ardhi ambayo ikpo katikati ya mikoa miwili ambayo ni katikati ya mkoa wa Manyara na mkoa wa Dodoma, ambapo sehemu ya Kondoa inahusika katika mbuga ya wanyama ya Mkungunero.

Mheshimiwa Spika, kijiji hicho kwa upande wa Kondoa wanasema sehemu ni ya kwao na pia kijiji hicho upande wa Manyara ambapo ndio Kiteto, na wenyewe wanasema sehemu ni yakwao. Sasa bado tuko katika kushughulikia utatuzi huo, na leo hii mkuu wa mkoa wa Manyara ameitisha kikao maalum, atakutana na pande zote hizi mbili kuweza kuweka bayana ili tuweze kuweka mpaka utakaoweza kuainisha kwamba ni nani wana haki au ni nani wanaweza wakawa upande upi katika mgogoro huo ili tuweze kutoa *user right* kwa hii WMA ya Endema.

Na. 114

Wilaya ya Singida Kutokuwa na Kambi ya Jeshi la Taifa

MHE. MOHAMED H. MISANGA aliuliza:-

Kambi ya Jeshi la Wananchi (*JWZ*) pamoja na Jeshi la Kujenga Taifa (*JKT*) ni muhimu sana kwa ulinzi na usalama na pia yanatoa mchango mkubwa sana nchini kiuchumi na kijamii kwa kushirikiana vizuri na wananchi katika kujiletea maendeleo na ustawi wa Jamii mahali ambapo kambi hizo zipo:-

- (a) Je, kuna Kambi ngapi za Jeshi la Kujenga Taifa hapa nchini na yako wapi?
- (b) Je, ni sababu zipi zilizosababisha wilaya ya Singida kutokuwa na kambi hata moja ya Jeshi la Kujenga Taifa?

NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako kabla sijajibu swal, naomba kwanza nitumie nafasi hii kutuma salamu za pole kwa ndugu jamaa na marafiki wa ndugu Bajoji Zakaria, aliyekuwa Katibu wa *CCM* Wilaya ya Mbarali, kutowana na kifo chake kilichotokea juzi. Tutamkumbuka kama mtu mwewenyi, mchapakazi na mtu mwewenyi msimamo kwenye mambo ya msingi, Mungu aiweke roho yake mahala pema Peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Mohamed Hamis Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Jeshi la Kujenga Taifa linazo kambi zaidi ya 15 ambazo zipo katika mikoa na wilaya mbalimbali Tanzania kama ifuatavyo:- Dar-es-Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Arusha, Dodoma, Tabora, Mara, Kigoma, Mbeya, Ruvuma, Lindi na Iringa.

(b) Mheshimiwa Spika, kati ya wilaya 127 ni wilaya 16 tu ndizo zenye makambi ya *JKT*, hii inatokana na ufinyu wa Bajeti. Hali itakaporuhusu, wilaya ya Singida itapewa kipaumbele.

MHE. MOHAMED H. MISANGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza ni kwa kuwa, makambi ya *JKT* pamoja na jukumu la msingi la ulinzi na usalama, yanajihusiaha pia na masuala ya kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kilimo na ufugaji. Na kwa kuwa, Wilaya ya Singida ina maeneo makubwa na mazuri sana yanayofaa kwa kilimo pamoja na ufugaji.

Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba Singida inastahili kupata fursa ya kuwa na kambi za *JKT* haraka iwezekanavyo?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili. Kwa kuwa, nafasi za kujiunga na jeshi la kujenga taifa hutolewa kwa kila mkoa, lakini baadhi ya watendaji wanaofanya usaili wa nafasi hizi hufanya hila ya kuwaita jamaa zao na ndugu zao kutoka mikoa mingine kuja kufanya usaili na kwa sababu hiyo kuwanyima haki au kuwanyima stahili yao wananchi na vijana wa mkoa unaohusika.

Je, Serikali haioni kwamba huo ni utaratibu mbaya ama unawanyima haki wananchi au vijana wanaohusika wakati wao katika mkoa wao tayari wameshapelekewa nafasi zao?

NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Misanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza naomba nimhakikishie Mohamed Misanga, kwamba hoja zake mpya za uwepo wa maeneo mazuri ambayo yanafaa kiuchumi, zitazingatiwa wakati tutakapokuwa tunachambua mpango wa kupanua/kuongeza makambi zaidi.

Mheshimiwa Spika, pili niseme kwamba ni nia ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kuona kwamba haki inatendeka wakati wote wa usaili wa vijana wa kuingia *JKT*. Tunaomba wale wenye dhamana, na hasa viongozi wa Serikali za Vijiji na Mitaa katika ngazi zinazohusika, pamoja na viongozi wa Wilaya kutimiza wajibu wao ipasavyo. Kila mtu akiwa mzalendo akapenda uwkweli, haki inawezekana na haki haiwezi kuanzia Wizarani, ni lazima ianzie huko chini. Kwa hiyo, tushirikiane wote kuhakikisha kwamba haki inatendeka kila mtu katika ngazi yake.

MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ili niweze kuuliza swalii dogo la nyongeza. Kwa sababu, hali ya mkoa wa Singida inahusu kabisa na inafanana kabisa na mkoa wa Rukwa amba tulikuwa na Kambi ya *JKT* inayoitwa Lula, ambayo ilikuwa inahusika na kilimo cha mahindi, maharage pamoja na ngano.

Lakini Kambi ile ilifungwa na mpaka leo Serikali wala haifikirii kwa sababu, wangeweza kuuona umuhimu huo kwa sababu tuko katika mpaka wan chi ya Zambia na *DRC* katika Ziwa Tanganyika. Je, si vizuri kuanzisha kambi ambayo itafanya kazi zote za ulinzi na kilimo?

NAIBU WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:
Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kufufua au kuanzisha Kambi mpya katika eneo la Rukwa ni suala muhimu na lenyewe totalitafakari. Lakini tunaomba na ndugu zetu wa Rukwa, nao watupe ushirikiano, maana tukianza kufungua kambi halafu wakianza tena kulia mmechukua eneo la wananchi! Tutapata tabu kidogo.

Na. 115

Upungufu wa Wataalam Kwenye Hospitali ya Tumbi Kibaha

MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR aliuliza:-

Hospitali ya Tumbi iliyoko Kibaha, inahudumia wagonjwa wanaopata ajali wanapokuwa safarini kutoka mikoa mbalimbali kwa kuwapatia matibabu, lakini hospitali hiyo ina upungufu mkubwa wa wataalam kwa baadhi ya fani za udaktari kama vile *Orthopaedic Surgeon, General Surgeon, Physician, Neurologist, n.k.*:-

- (a) Je, Serikali inalitambua suala hilo?
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha hospitali hiyo inakuwa na wataalam, dawa na vifaa vya kutosha ili kuokoa maisha ya watu wanaopata ajali katika maeneo hayo?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Al-Shymaa John Kwegyir, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwa kuna upungufu wa watalaam wa afya katika fani mbalimbali katika Hospitali ya tumbi. Hali hii ya upungufu wa watumishi inapatikana katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya hapa nchini. Na kwa kweli, upungufu huu unaathiri utoaji wa huduma bora za afya. Mikakati ya nchi nzima imeandaliwa kwa kuitia mpango wa *MAM* na imeanza kutekelezwa ili kukabiliana na changamoto hii na tayari tumeanza kuona matunda.

(b) Mheshimiwa Spika, hospitali ya Tumbi ni ya rufaa ngazi ya Mkoa wa Pwani. Na kwa sababu hiyo, imepewa dawa na vifaa pamoja na wataalamu kama inavyotoa kwa hospitali nyingine za Rufaa za Mikoa.

Kwa sasa, Hospitali hiyo ina Madaktari Bingwa wawili wa magonjwa ya wanawake na afya ya uzazi, mmoja wa tiba (*Physician*), wawili wa magonjwa ya watoto, mmoja wa upasuaji na mmoja wa huduma za mionzi. Daktari Bingwa mwengine wa upasuaji yuko masomoni akimalizia kozi ya “*Hospital Management*”, jumla ya Madaktari Bingwa ni saba. Idadi hii ya madaktari bingwa ni kubwa kuliko hospitali nyingi za mkoa hapa nchini.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa Hospitali ya Tumbi, hasa ikizingatiwa kwamba Hospitali hiyo ipo karibu na barabara kuu ya kwenda na kutoka mikoani.

Serikali itaendelea na imeendelea kuimarisha huduma ili iweze kutoa huduma kwa wananchi kwa viwango vya ubora unaotakiwa. Serikali imekuwa ikiongeza Bajeti kwa ajili ya dawa na vifaa mwaka hadi mwaka.

Aidha Halmashauri zina vyanzo vingine vya mapato kama vile Mfuko wa Afya ya Jamii, Bima ya Afya ya Taifa na Mfuko wa pamoja na Wahisani yaani, “*Basket Fund*.” Pesa hizi zikitumiwa kwa uangalifu zinaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa upungufu wa dawa na vifaa tiba. Rai yangu ni kuziomba Halmashauri ikiwa ni pamoja na utawala unaoongoza hospitali ya Tumbi, kusimamia kwa karibu mifuko hii ili iwe na tija.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa kuzingatia dhana nzima kwamba kinga ni bora kuliko tiba, na kinga ni gharama nafuu kuliko tiba, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, nawaomba watumiaji wote wa barabara, wenye vyombo vya usafiri na watembea kwa miguu, kuwa waangalifu wanapotumia barabara ili kuepusha ajali ambazo matibabu yake ni ya gharama kubwa lakini vile vile husababisha vifo au ulemavu wa kudumu.

MHE. AL-SHYMAA J. KWEGYIR: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana pia namshukuru Waziri wa kwa majibu yake mazuri lakini hapo hapo nina maswali ya nyongeza. Kwa kuwa hospitali ya Tumbi ina matatizo pia la maji hili nimelishuhudia mimi mwenyewe tarehe 7 Mei, 2010 kulikuwa pale hospitalini nilikuwa na mgonjwa nimeenda kumwona nimekuta tatizo hilo lina siku tatizo ambalo limeathiri sana limeleta imekuwa hali ngumu pale hospitalini wodini na *labour ward*. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba hospitali ya tumbi inapata maji wakati wote angalau kwa kuweka matenki au kuchimba kisima pale kwenye ile hospitali ya Tumbi au kuhakikisha kwamba kunapatikana maji pale kuliko kutegemea maji kutoke Ruvu mto pekee?

Wataalam na watumishi wa afya wamekuwa ni wachache sana hapa nchi ambayo inaathiri huduma ya afya. Je, tatizo ni nini hasa?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo, nimelichukua swalii la maji hapa inabidi tuangalie kama ni matatizo ya wingi wa maji unaofika pale kituoni au ni matatizo ya plumbing katika hospitali yenye na tutashirikiana na wenzangu wanaohusika ili tuwapatie ufumbuzi.

Suala la uhaba wa watumishi ni suala ambalo tumelitoa maelezo hapa mara kwa mara ni kwamba hawapo, hatuna watumishi wa kutosha yaani changamoto ambayo imepewa kipaumbele sana katika mpango mzima wa maendeleo ya afya ya msingi. Kama nilivyojibu katika swalii lake la msingi ni kwamba mikakati imeendelea tumeipa kipaumbele kwa mfano mpango ulipoanza usahili ulikuwa wanachuo kama 1,113 nia yetu ni kufikisha elfu sita na nusu kwa mwaka sasa hivi tuko 4,100 na suala la kuzalisha lakini pia kwamba hawa watu wetu tunaowazalisha wawezesha kufanya kazi hapa nchini lakini zaidi waende kufanya kazi vijijini. (*Makofsi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuwa hospitali ya mkoa wa Singida ina upungufu mkubwa wa madaktari hasa madaktari bingwa kama ilivyo hospitali ya Tumbi na kwa kuwa Serikali ilishatupatia madaktari wanne bingwa toka Januari na taarifa akapelekewa Mkuu wa Mkoa. Je, hao madaktari wamepotelea wapi?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyokiri kuna upungufu mkubwa wa watumishi wote na hasa madaktari bingwa, miaka mitatu iliyopita Waheshimiwa Wabunge kutoka mkoa wa Singida walikuja wakachangia hela nyingi tukawapa mganga mmoja na sasa Mheshimiwa Mkumbo Chilolo anasema kwamba tumewapatia madaktari nilidhani ataanza kwa kutushukuru kwa kufanya hivyo lakini tungenesema kwamba nitakwenda nifuatilie wamekwenda wapi. (Makofi)

MHE. RAMADHAN A. MANENO: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza kwenye la msingi la Mheshimiwa amezungumzia sana hasa wasafiri wanaopata ajali za barabarni ambao wagonjwa hao hupelekwa kwenye hospitali ya Tumbi.

Lakini hao wagonjwa ambao wanaopata ajali wengi ni kati ya Chalinze mpaka Tumbi, na majeruhi wengi ni wale ambao wanaanza kupata tiba kwenye kituo cha afya cha Chalinze, lakini tatizo linajitokeza wakishapata tiba hiyo awali kabla hawajapelekwa Tumbi ni jinsi gani wanavyosafirishwa kupelekwa tumbi wakitokea pale Chalinze.

Je, Wizara au Serikali sasa iko tayari kukipatia kituo cha Afya cha Chalinze usafiri wa uhakika ili wagonjwa wanaopata ajali pale wapelekwe haraka sana Tumbi?

WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII: Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu Mheshimiwa Maneno kama ifuatavyo. Kwa kweli hili suala amewahi kuuliza hata kwenye maswali ya kawaida nakubaliana naye kwamba mtu akipata ajali kule kumfikisha mapema ili apate huduma zinazostahili ndiyo inaweza ikamweka katika hatari ama ya kufa au ya kupona.

Kwa hiyo, upo umuhimu wa kuwa na usafiri. Niahidi tu kwamba nitawasiliana na mwenzangu Mheshimiwa Celina Kombani tuone jinsi tutakavyoliangalia hili suala. (Makofi)

Na. 116

Kutumia Mto Kagera kwa Usafiri wa Majini

MHE. JANETH B. KAHAMA aliuliza:-

Katika miaka ya 1950, Mto Kagera ulikuwa ukitumiwa kwa usafirishaji rasmi wa bidhaa za biashara (*Commercial Navigation*) kama vile Madini ya Bati (*Tin-Ore*) Kampuni ya Kyera Syndicate huko Karagwe kutoka Bandari ndogo ya Nyakanyasi - Kagera hadi Bandari ndogo ya Bukakata - Uganda.

(a) Je, Serikali kwa kushirikiana na Serikali za Afrika Mashariki ina mpango gani wa kufufua usafirishaji huo muhimu kutoka Kagera kwenda mikoa ya magharibi mwa nchi ya Uganda na *Congo DRC?* (*Makofi*)

(b) Je, Serikali haioni kuwa, kufuta usafirishaji katika njia hiyo itasaidia pia kuokoa Mto Kagera usimezwe na Magugu - Maji na kukauka kabisa?

NAIBU WAZIRI WIZARA YA MIUNDOMBINU alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Bina Kahama, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa usafirishaji rasmi wa biashara yaani *Commercial Navigation* katika mkoa wa Kagera unaweza kuwa muhimu kulingana na mahitaji kama ilivyokuwa katika hiyo miaka ya 1950. Kwa vile mahitaji ya usafiri kuitia mto huu unahusisha nchi nyingine jirani kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge.

Serikali inaupokea ushauri wa ufufuaji wa usafiri huo ambao unaweza kufanya chini ya mpango wa Jumuia ya Afrika Mashariki ili kuhusisha nchi nyingine zinazohusika katika kuisaidia utekelezaji wake kwa manufaa ya nchi zetu.

Mheshimiwa Spika, hata bila kufufua usafiri kuitia mto huu bado uko umuhimu wa kutunza mazingira katika mto huu ili usimezwe na magugumaji.

Kwa hiyo, Serikali itafuutilia jambo hili katika mikutano husika ya Jumuia ya Afrika Mashariki ili lifanyiwe kazi kwa lengo la kutunza mazingira na kulinda mto huu muhimu si kwa usafiri tu bali pia kwa shughuli za kiuchumi na kijamii katika eneo la maziwa makuu.

MHE. JANETH B. KAHAMA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa nashukuru kuwa ushauri wangu ameuchukua tunangoja utekelezaji. Nina maswali mawili ya nyongeza. Miaka michache iliyopita wananchi wa Kanda ya Ziwa Victoria kuitia Bunge hili walikuwa wameahidiwa kuwa watapatikawa dawa ya kuua magugumaji ambayo itateketeza kabisa kwa muda mfupi. Je, Serikali imechukua hatua gani mpaka sasa katika kufanikisha hilo?

Je, upungufu wa kina cha maji katika ziwa Victoria utakuwa umeathiri kiasi gani usafiri wa meli hata bodi na stima ili watu wetu waweze kusafiri bila kupata matatizo? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WIZARA YA MIUNDOMBINU: Mheshimiwa Spika, swali la kwanza juu ya ahadi ya dawa ya kuua magugu maji ambayo Serikali ilitoa nataka nimhakikishie tu kwamba ahadi hiyo iliyotolewa bado inafanyiwa kazi na kama nilivyosema katika jibu la msingi hapa kwamba suala hili kwa sababu linahusisha na nchi zingine za jumuiya ya Afrika Mashariki, linaendelea kufanyiwa kazi katika vikao hivyo ambavyo vinatuhusisha sote. Hivi karibuni kulikuwa na mukutano kule Kisumu ambao ulikuwa unahusika na masuala haya ya kuondoa magugu maji katika maeneo yetu ya Maziwa Makuu. Suala hili lilijitokeza na lilizungumziwa sana.

Kwa hiyo, nataka niseme kwamba Serikali bado linaendelea kulizingatia.

Hili suala la pili juu ya upungufu wa kina cha maji unaathiri kiasi gani usafiri wa maji, napenda nikiri tu kwamba nilichukue kwa sababu ningependa nimpe jibu la uhakika niweze kushirikiana wenzangu wa sekta zingine zinazohusika na suala hili tuweze tukampa jibu la uhakika kwamba ni kiasi gani kinathiri cha usafirishaji katika upunguaji wa maji katika ziwa Victoria. (*Makofi*)

Na. 117

Mashamba ya Kiwanda cha Nyama Mbeya

MHE. BENISON M. MPESYA (K.n.y MHE. MCH. LUCKSON MWANJALE) aliuliza:-

Kutokana na kwamba kiwanda cha Nyama Mbeya hakijaanza kazi bado vilevile mashamba yanayohusika na kiwanda hicho nayo hayatumiki kwa sasa:-

Je, kwa nini Serikali isiruhusu wananchi kuyalima mashamba hayo hadi hapo kiwanda kitapoanza kufanya kazi?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, Mbunge wa Mbeya Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwanda cha nyama cha Mbeya ulianza mwaka 1975 na ulitegemea kukamilika mnamo mwaka 1978. Hata hivyo kutokana na matatizo ya fedha, ujenzi ulisimama mwaka 1978. Kwanda hiki kina uwezo wa kuchinja ng'ombe wapatao 250 kwa shifti ya masaa manane kwa siku ama ng'ombe wapatao 15,000 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, kiwanda kina eneo la ukubwa la hekta 102 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji ikiwa ni pamoja na kutunza ng'ombe kwa masaa 48 wanasosubiriwa kuchinjwa. Aidha, kiwanda kina eneo la malisho lenye ukubwa wa hekta 4,912 lililopo Nsalala karibu na kiwanja cha Ndege cha Songwe.

Eneo hili litatumika kunenepesha ng'ombe wapatao 180,000 kwa mwaka. Maeneo yote mawili yana hati miliki na. LO/188772/3 na LO/18771/3 zilizotolewa tarehe 1 Septemba, 1999 za umiliki wa kipindi cha miaka 33.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu za nyuma zinaonyesha kwamba baada ya kuanzishwa kwa sera ya kilimo cha kufa na kupona mwaka 1974 wananchi waliruhusiwa kulima kwa muda katika mashamba haya. Lakini walipotakiwa kuacha kulima ulizuka mgogoro mkubwa hadi Serikali ilipowafidia mwaka 1998.

Hivyo isingekuwa busara kwa Serikali kuyagawa maeneo haya kwa wananchi kwa muda na kurudia matatizo yaliyojitekeza huko nyuma, wakati shirika la *Consolidated Holding Corporation (CHC)* liko katika mchakato wa kufanya tathmini ya shamba ili kutangaza upya kwa ajili ya kumpata mwekezaji.

MHE. BENISON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza, kwa sababu mgogoro uliozuka pale mwanzo mwaka 1998 kulikuwa hakuna makubaliano rasmi kati ya wananchi na Serikali. Lakini sasa kukiwa na utaratibu rasmi wananchi wakaweka mkataba na Serikali nafikiri jambo hili linawezekana kabisa kwa wananchi kupewa eneo na kulima kukiwa na mkataba maalum wa kisheria.

Je, Serikali haiwezi kulizingatia hilo?

Mheshimiwa Spika, nilifikiri jana nilipojieleza vizuri juu ya kiwanda hiki kwa kutegemea mahusiano mazuri niliyonayo na mawaziri hawa wawili nilifikiri walinisikiliza vizuri sana lile ombi langu ninaomba kwa sababu tunatimiza nguzo ya tano ya kilimo kwanza ya kutoa ardhi kwa wananchi ili wazalishe, ninaomba Serikali iliridhie kuwapa wananchi hawa eneo.

Je, Serikali imekubaliana na mimi katika hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mheshimiwa Mpesa tumekuwa kwenye Kamati moja kabla sijawa Naibu Waziri na tulifuatilia sana kiwanda hiki. Ukweli Serikali ingelipenda kuwapatia wananchi hao hilo eneo, lakini tatizo ni kwamba walipewa wananchi hawa eneo hilo, lakini wakati ulipofika sasa kuwaambia jamani wapishe kulizuka matatizo makubwa mpaka wengine ikabidi wafidiwe.

Halafu kwa sasa tuko katika harakati za kutamfuta mwekezaji ili akifufue kile kiwanda ambacho kiligharimu mamilioni ya hela. Sasa kama tutakuwa na watu wanalima pale na mwekezaji akaja pale atashindwa kukichukua kiwanda mimi nafikiri jambo zuri hapa tuhakikishe kwamba kiwanda kinachukuliwa wananchi watapata kazi na tutauza pale mifugo yetu na hili nalo itakuwa wananchi wamenufaika badala tena kurudisha mgogoro ule ule kwa sababu tulishawapa wananchi kutoka pale ilibidi mambo yaende mpaka mahakamani na wengine ikabidi wafidiwe.

Malimbikizo ya Madai ya Askari Polisi

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA (K.n.y MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA) aliuliza:-

Kwa kuwa, kuna madai mengi ya malimbikizo ya madai mbalimbali ya Askari Polisi:-

- (a) Je, ni fedha kiasi gani ambazo Serikali inadaiwa?
- (b) Kwa kuwa, malimbikizo ya madai ya posho yanawakera zaidi askari. Je, Serikali itawalipa lini posho zao ili kupunguza malalamiko?
- (c) Je, ni kwanini baadhi ya askari huchelewa sana kupata nyongeza ya mishahara yao?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, swali hili linafanana na swali Na. 23 lililoulizwa na Mheshimiwa Ibrahim Muhammad Sanya, Mbunge wa Mji Mkongwe na kujibiwa tarehe 14 Aprili, 2010. Wakati nikijibu swali hilo nilieleza kwamba madeni ya askari polisi yanatokana na posho za safari za kikazi, uhamisho na likizo kutoka mwaka 2001 hadi Juni, 2009 ni Tshs. 9,227,707,000.00. (*Makofi*)
- (b) Mheshimiwa Spika, Mkaguzi Mkuu amemaliza zoezi la uhakiki wa madai ya askari yaliyowasilishwa kwake. Baada ya uhakiki huu Hazina italipa madeni hayo kama tulivyokuwa tumesema awali.
- (c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa siku ya nyuma baadhi ya askari walikuwa wakichelewa kupata nyongeza za mishahara yao.

Hata hivyo tatizo hilo kwa sasa limepungua sana baada ya mtandao wa mishahara (*Payroll Point*) kufungwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi ambapo urasimu katika kufanya marekebisho ya mishahara umepungua kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, iwapo Mheshimiwa Mbunge ana majina ya askari ambao bado hawajarekebishiwa mishahara yao anipatie majina yao ili niweze kuyafanya kazi. (*Makofi*)

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa deni la bilioni 9.2 la kuanzia mwaka 2001 hadi 2009 na labda hadi leo hii. Na kwa kuwa hili deni la askari wakiwemo askari wadogo wenye yleo vya chini.

Je, Serikali haioni kwamba kutokuwalipa hawa watu ambao wanafamilia wanasomesha watoto na wana wagonjwa ni kuwanyima haki hazi zao za msingi na kwa kuwa Waziri amekiri kwamba uhakiki umeisha watalipwa lini sasa hizi haki zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa safari za kikazi uhamisho na likizo ni mambo au matukio ya kisheria ya kiutaratibu na yanajulikana, ni kwanini kunatokea uzembe kwa miaka zaidi ya kumi kwa mtu kutokulipwa na kiasi tunafikia madeni makubwa kiasi hiki.

Je, Serikali inawachukulia hawa viongozi ambao wanachelewesha haki za watu labda kwa makusudi wanachuliwa hatua gani? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dr. Willibrod P. Slaa, kama ifuatavyo:-

Anaposema kwamba, deni ni kubwa, kweli hilo tunakubali lakini ninamwomba Mheshimiwa Dr. Slaa akumbuke kwamba, deni lilikuwa kubwa kuliko lilipokuwa na jitihada zimekuwa zikifanyika kulipunguza mpaka tukafikia hapo tulipofikia. Tatizo lililokuja kujitokeza na alilileta yeye mwenyewe Dr. Slaa, lakini katika maeneo mengine siyo ya Polisi ya kusema kwamba, baadhi ya malipo yamekuwa yanalipwa kinyume na taratibu na Sheria bila kuhakiki madeni hayo.

Sasa tulichofanya ni kuhakikisha kwamba, tunahakiki ili tuwe na uhakika kwamba kweli yale madeni yapo au ni madeni hewa na baada ya kujua kama kweli madeni yapo, ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema kwamba, tayari Mkaguzi Mkuu ameshafanya uhakiki na ninamhakikishia kwamba, hizi pesa zitalipwa na amri ya kulipa hizi pesa ninataka nimwambie kwamba Waziri Mkuu ambaye yuko hapa amekwishaagiza hivyo na hizi pesa zitalipwa.

La pili, hii anayoisema kwamba, umekuwepo uzembe na kutaka kuonesha kwamba Wizara na Serikali haiko makini katika kutazama hawa maana yake imekuwa ni miaka mingi wakati wanahamishwa na kadhalika. Mimi naomba nimhakikishie Mheshimiwa Dr. Slaa uchungu aliokuwanao yeye ni huo huo tulionao sisi Viongozi katika Serikali; hawa ni watu ambao wanatazama amani ya taifa letu, hawa ni watu ambao wanalinda usalama wa taifa letu.

Kwa hiyo, sisi tuna wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba, haki zao zinatendeka na ndiyo maana tumefanya uhakiki wa uhakika na sasa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu Wizara yetu ametamka rasmi kwamba, pasiwepo na uhamisho wa

watu mpaka fedha za kuwahamisha ama likizo na kadhalika zimekuwepo ndiyo haya yafanyike. (*Makofi*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na mtazingatia ukweli kwamba, ingawa muda wa maswali sasa umefika mwisho, lakini tulikuwa na dakika kumi zilizotumika katika kuwasilisha hati mbalimbali mezani ili kuzifidia hizo dakika kumi; basi tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo na swali linaulizwa na Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mbunge wa Muhamwe.

Na. 119

Kuboresha Kituo cha Redio Mahembe Kigoma

MHE. FELIX N. KIJIKO aliuliza:-

Kwa kuwa Mkao wa Kigoma uko mpakani na pia uko mbali ya Makao Makuu ya Nchi; na kwa kuwa Mkao huo hauna mawasiliano ya redio ya kuaminika kwa maana Redio ya Taifa; na kwa kuwa redio hiyo ni muhimu sana kwa wananchi hasa wakulima ili kuwapasha habari za mambo mbalimbali yanayojiri kila siku ndani na nje ya nchi:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuboresha Kituo cha Redio Tanzania kilichopo Mahembe - Kigoma ili mitambo yake iwe na nguvu ya kupokea na kusambaza masafa ya redio hiyo kwa Wilaya zote za Mkao huo?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhamwe, kama ifuatavyo:-

Nia ya Serikali wakati wote ni kuhakikisha kuwa, vyombo vyake vya habari kama TBC Taifa vinaboreshwa na kuwa na uwezo wa kutoa matangazo yake ili yamfikie kila mwananchi mahali popote pale alipo. Mkao wa Kigoma una kituo cha kurushia matangazo kilichoko Mahembe, nje kidogo ya Mji wa Kigoma. Mtambo uliofungwa hapo ni wa KW 100. Mtambo huu ni mkubwa na ungeweza kufikisha matangazo yake katika Wilaya zote za Mkao huo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tatizo kubwa la Mkao huo ni upatikanaji wa umeme wa uhakika kuweza kuendeshwa mtambo huo wa KW 100. Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa Mkao wa Kigoma hutumia majenereta kuzalisha umeme. Hivyo, kutokana na matumizi makubwa ya umeme unaozalishwa, hauna nguvu ya kuendesha mtambo wa redio wenye KW 100 uliopo Mahembe. TBC Taifa imelazimika kutumia mtambo mdogo wa KW 10 ambaa uwezo wake hauwezi kufika eneo kubwa la Mkao wa Kigoma. Hivyo basi, pindi tatizo la umeme katika Mkao wa Kigoma litakapopatiwa ufumbuzi, Mkao huo utaweza kupokea matangazo ya uhakika ya TBC Taifa kupitia mtambo huo wa KW 100.

Mheshimiwa Spika, kwa habari ambazo nimepata hivi karibuni, baada ya kuwasiliana na Waziri wa Nishati na Madini, ameniambia kwamba ifikapo mwezi Juni tatizo hilo sasa litaondoka. Kwa hiyo, matangazo Kigoma yatapatikana kama kawaida.

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mkoa wa Rukwa uko katikati ya Mbeya na Kigoma ambako kote kuna mitambo ya kurushia matangazo ya TBC lakini usikivu hasa katika Wilaya ya Mpanda ni duni kabisa. Je, Serikali inasema nini juu ya kuboresha usikivu wa Redio Tanzania katika Wilaya ya Mpanda?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda, kama ifuatavyo:-

Wiki iliyopita, nilijibu swali linalohusiana na usikivu wa Mkoa wa Rukwa, ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila na nilimhakikishia kwamba, Mikoa ambayo imebaki iko tisa na niliitaja mmojawapo ni Mkoa wa Rukwa, itakapofika mwezi Septemba tayari tutakuwa tumeshaweka mitambo mipya na kufanikisha Mikoa tisa yote ikiwemo Shinyanga, Manyara, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa na Rukwa na hasa Mpanda watakuwa wanapata matangazo ya TBC Taifa na TBC FM. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, asiwe na wasiwasi.

Na. 120

Utamaduni wa Taifa Letu

MHE. MARTHA M. MLATA aliuliza:-

Kwa kuwa utamaduni ni kielelezo kikubwa cha utaifa; na kwa kuwa katika mazingira ya utandawazi utamaduni wa nchi nyingi za Kiafrika umeathirika kwa kiwango kikubwa na hivyo kutishia baadhi ya tamaduni zetu kupotea:-

(a) Je, Serikali imefanya utafiti wowote (*Field Research*) ili kutathmini athari za utandawazi kwa utamaduni wetu?

(b) Kwa kuwa vijana wengi walioko mashulenii na vyuoni ndiyo wanaoonekana kuiga sana tamaduni za kigeni ambazo zinatofautiana sana na tamaduni zetu. Je, Serikali ina mpango gani wa kukabiliana na tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Martha Mlata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, utamaduni ni kielelezo kikubwa cha utaifa na vilevile katika mazingira ya utandawazi, utamaduni wa nchi nyingi za Kiafrika umeathirika kwa kiwango fulani.

Kwa kutambua hilo, Serikali imekuwa ikifanya tafiti mbalimbali za kiutamaduni ili kuweka misingi imara ya kupambana na utandawazi; kwa mfano, kuna Mradi wa JIPEMOYO, Mradi wa pamoja kati ya Serikali ya Tanzania na Finland, uliofanyika Magharibi mwa Bagamoyo. Nia ni kuboresha Mila na Desturi za watu wetu katika nyanja za ufugaji, muziki, vyakula vya asili na viwanda vidogovidogo. Mradi mwingine ni wa Utafiti wa Jando na Unyango, Mkoa wa Mtwara. Lengo ni kuchunguza mafunzo, maadili (*values*), imani (*beliefs*) na aina mbalimbali za elimu ya jadi.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ya kutathmini athari za utandawazi kwa utamaduni ni kutoa msimamo mpya wa ukuzaji wa utamaduni wetu. Tathmini ya Serikali inaonesha kuwa, Mila na Desturi zetu nyingi zina vipengele vya kimaendeleo ila vinapuuza au havijulikani ipasavyo. Kinachotakiwa ni kuufanya utamaduni wetu uzidi kuwa wa kimaendelezo zaidi.

Wizara yangu imeona kuna haja ya kuongeza kasi ya utafiti wa Mila na Desturi ili kuzitambua zile ambazo ni kikwazo cha maendeleo au kinyume na utashi wetu ili zitokomezwe. Nia ni kufahamu kwa undani utamaduni wetu na kuuendeleza badala ya kuubeza. Tunataka kujenga tabia ya kutambua, kuenzi na kuheshimu vitambulisho vya Taifa.

(b) Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, kuendelea kupambana na utandawazi kwa kuyaona mambo yake yote kama hayana manufaa kwetu, ni sawa na kupambana na wakati. Hata hivyo, ni wajibu wetu kama Taifa Huru, kutohoa yaliyo mema na kuendelea kutetea na kulinda misingi ya maadili na tamaduni zetu ili kuwanusuru vijana kuiga kila kitu ambacho pengine kinatofautiana sana na tamaduni zetu.

Sera ya Elimu na Mafunzo (1995) na Sera ya Utamaduni (1997), zinatambua mchango wa elimu ya jadi katika kuboresha mfumo wa elimu nchini. Kwa upande wake, Sera ya Utamdauni imejiekea lengo la kuzitambua, kuzithamini na kuzitumia amali nzuri za utamaduni wa jamii katika Ujenzi wa Taifa. Amali hizo ni pamoja na maadili mema, utu bora, ari ya kazi, usawa, mshikamano, ukarimu, upendo, uzalendo, amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, katika mikutano mikuu ya elimu, Idara yetu ya Maendeleo ya Utamaduni imekuwa ikihimiza kwamba, Mitaala ya Elimu ya Msingi, Sekondari na Vyuo vya Elimu, ijulimushe mafunzo kuhusu fani za sanaa, maarifa, ujuzi wa stadi za kazi, uraia na historia ya nchi yetu na kuwa masomo husika yatahiniwe katika mitihani ya

mwisho ya ngazi mbalimbali za elimu. Huu ni mpango wa kuaminika katika kukabiliana na tatizo la vijana walioko mashulenii kuiga tamaduni za kigeni.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, ahsante na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Naibu Waziri na ninashukuru sana kwa sababu amesema kunahitajika kasi ya kuweza kudumisha utamaduni wetu. Sasa kwa kuwa njia mojawapo inayosambaza utandawazi ni pamoja na vyombo nya habari.

Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba ni vyombo hivyo ambavyo pia vinaweza vikasambaza na kuweza kudumisha tamaduni zetu hasa utamaduni wa Mtanzania kwa upande wa mavazi pamoja lugha?

Swali la pili; kwa kuwa kuna Siku ya Utamaduni wa Mtanzania ambayo huadhimishwa pale Makumbusho Dar es Salaam lakini kwa kabile moja tu.

Je, Waziri atakubaliana nami kwamba sasa Serikali ipange Siku Maalum kabisa ambayo itakuwa ni Siku ya Utamaduni wa Mtanzania lakini zifanyike kwenye Mikoa husika?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Martha Mlata, maswali yake ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Hili la vyombo nya habari ni kweli kwamba, moja ya tamaduni zetu kupotoka ama kupata maadili mabovu mojawapo ni vyombo nya habari vinahusika. Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tuko waangalifu sana, tuna Kamati Maalum ya Maudhui, ambayo moja ya kazi yake kubwa ni kutazama vyombo vyote nya habari kuona kwamba, vinafuata maadili ya nchi yetu na vinakutana na kumshauri Waziri mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba, hatupotiki na hatuendi kinyume na maadili ya nchi yetu.

Hili la pili nakubaliana naye lakini ninataka nimkumbushe tu kwamba, sisi katika Wizara yetu tuna Siku ya Utamaduni. Mwaka huu ninafurahi kusema, Mheshimiwa atakumbuka kwamba, yamefanyika katika Mkoa wake. Kila mwaka tunafanya, hapo awali tulikuwa tunafanya Dar es Salaam mara kwa mara lakini baada ya kupata ushauri imeonekana tuwe tunafanya katika Mikoa mbalimbali. Mwaka huu tumefanya Siku ya Utamaduni katika Mkoa wa Singida na tulifanikiwa sana na tunafanya kwa Mikoa yote; tulikuwa tunazunguka kwa Mikoa yote hii ili angalau kila Mkoa uweze kuona na kuweza kutambua utamaduni.

MHE. MHONGA S. RUHWANYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Moja ya Utambulisho wa Utaifa ni Vazi la Taifa; je, kwa nini Tanzania mpaka sasa hatuna Vazi la Taifa?

NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba, mchakato wa Vazi la Taifa umeshafanyika na kwa bahati nzuri ulifanyika hapahapa Dodoma katika miaka ya 1995. Suala lile bado lina utata wa kitaalamu, tunaendelea kulifanyia utafiti ili tuweze kupata vazi ambalo halitaleta mgogoro wa aina yoyote. Kumekuwa na matatizo mbalimbali kwa Wataalamu mbalimbali kwamba, vazi lifanane vipi, lakini mpaka sasa hivi mchakato unaendelea, tunazidi kupata ushauri kutoka kwa Wataalamu mbalimbali ili tutakapopata vazi hili kusiwe na utata wa kuonekana kwamba, labda tumependelea Mkoa fulani ama kabilia fulani.

Ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mhonga kwamba, mchakato huo utakapokwisha, vazi hilo totalitamka humu Bungeni na Wananchi wote wataambiwa.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wa maswali umepita. Kama ilivyo ada ...

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mwongozo wa Spika!

SPIKA: Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Kanuni ipi?

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa mujibu wa Kanuni Namba 68, kwa sababu suala hili ni nyeti na kama ambavyo alizungumza Mheshimiwa Marehemu Amina Chifupa, linahusu viwanda vyta kuagulia binadamu.

Leo asubuhi nimesikia taarifa kwamba, kuna madawa yanavushwa mpakani ambayo yana sumu. Kwa hali hiyo, naomba nitoe rai kwa Serikali kwamba, watusaidie kufuatilia jambo hili kwa karibu ili kuepusha madhara ambayo yanaweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana kwa tahadhari hiyo, kwa sababu inahusu maisha ya watu ni hakika ni jambo la dharura. Serikali imesikia, nina hakika Mheshimiwa Waziri wa Afya na Wizara mbalimbali kwa kweli hatujui yanatengenezwa humuhumu yanaingizwa nchini na kadhalika, wafuatilie ili tuweze kupata tamko lenye kutupa faraja.

Natumaini itawezekana ndani ya wiki moja tukapata kauli ya Waziri ili kina Mama na Wananchi wote wawewe kutulia. Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya. (*Makofit*)

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo; kwanza ni wageni waliopo Bunge asubuhi hii. Wageni wa Mheshimiwa Waziri wetu wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias M. Chikawe ni kama ifuatavyo:-

Kwanza ni Mheshimiwa Agustino Ramadhani, ambaye ni Jaji Mkuu wa Tanzania, karibu sana Mheshimiwa Jaji Mkuu. Mara kwa mara tunafarijika sana unapopata wasaa kuja hapa Bungeni, inaonesha jinsi unavyojali shughuli zinazoendelea hizi za kutunga Sheria. Ahsante sana. (*Makofi*)

Yupo pia Katibu Mkuu, Ndugu Oliver Mhaiki, naona Naibu Waziri wa Ulinzi ametoka sasa sijui ni ishara ya nini, lakini Ndugu Mhaiki karibu sana. (*Kicheko/Makofi*)

Wapo Majaji kama ifuatavyo; Mheshimiwa Jaji Regina Rweyemamu, naomba asimame tafadhalii; Mheshimiwa Jaji Mary Shangali; Mheshimiwa Jaji Robert Makaramba; Mheshimiwa Jaji Emilian Mushi ambaye ni Jaji lakini pia ndiye Mkuu wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto; yupo Ndugu Japhet Sagasii, Katibu wa Tume ya Kurekebisha Sheria, karibu sana Japhet hii ni ishara ya jinsi ambavyo utumishi wako hapa Bungeni kwa miaka minge tunavyouenzi. (*Makofi*)

Yupo pia Jaji Francis Mutungi ni Msajili wa Mahakama ya Rufani; Mheshimiwa Elieza Feleshi, Mkurugenzi wa Mashtaka kwa maana nyingine ni *DPP*; yupo Mheshimiwa Jaji Mstaafu Amir Manento, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, amefuatana na Mheshimiwa Mahfoudha Alley, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Ahsanteni sana na karibuni sana. (*Makofi*)

Yupo pia Mheshimiwa George Mlawa, Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu; bado tunaendelea kuenzi utumishi wako hapa katika Bunge lakini pia na kipindi ulichokuwa Mbunge.

Yupo pia Ndugu Bernadetha Gambishi, ambaye ni Naibu Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu; pia yupo Mheshimiwa Joachim Dimello, naye ni Kamishna wa Tume hiyo ya Haki za Binadamu. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia kwenye *Gallery* ndugu. Mary Masai, Kaimu Katibu Mtendaji, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Tunatoa wito kwa wahusika, huyu mama amekaimu muda mrefu sana, sijui maana yake nini, hii ni mara nyingine ninamsoma, kaimu, kaimu, sijui kama sheria za kazi zinaruhusu mambo ya namna hii, mtu anakaimu zaidi ya mwaka, *any way!* Mgeni mwininge ni ndugu Celina Wambura, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, yule pale. (*Makofi*)

Huyu sasa ni mgeni wa kisiasa, ndugu Ally Kanga, ni Mwenyekiti Mstaafu wa CCM wa Wilaya ya Nachingwea na kwa maneno ya Waziri siyo yangu, ni kada motomoto wa CCM na ni mmoja wa wapiga debe mashuhuri wa Mbunge wa Nachingwea, duh, yuko wapi huyu bwana? Aah, ndiye yule pale, ahsante sana, basi uendelee kumlea Mheshimiwa Waziri, anafanya kazi nzuri sana, kwa hiyo, kazi yako unayoifanya hiyo basi uendelee nayo vizuri tu kwa sababu tunamhitaji. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mbunge wa Dodoma Mjini, ambao ni viongozi wa Chama cha Wachimbaji wadogo wadogo wa Madini Tanzania, wakiongozwa na Jeremia Msabi, Mwenyekiti. Wale wachimbaji wa madini, naona hawapo, basi pengine hawakupata nafasi.

Tunao wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe, ambao ni ndugu Mariana Simbachawene, mkewe Mbunge sijui yuko wapi na watoto Caritas na Wilfred Simbachawene, karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo wageni wa Mheshimiwa Alhaji Athuman Janguo, ambao ni Nadhifa Janguo, mkewe Mbunge, aah yule pale karibu sana, na ndugu Said Janguo ambaye ni mwanawe.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Naam, taarifa.

MBUNGE FULANI: Nadhifa Janguo ni Mkwe wa Mbunge, siyo mke wa Mbunge na amekuja na mumewe. (*Kicheko*)

SPIKA: Loh, ahsante. Hili ni sahihisho la maana sana, lakini anachosoma Spika ni kile kilichoandikwa, hawezi kubuni mengine, lakini tunabadilisha ni mkwewe, siyo mkewe, loh, hatari sana hii. (*Kicheko*)

Wapo wageni 27 wa Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o ambao ni washiriki wa Warsha kuhusu mafunzo ya uhamasishaji dhidi ya UKIMWI, wakiongozwa na ndugu Peter Munene, Mkurugenzi Mkazi wa Asasi inaitwa *Help Action*. Ndg. Peter Munene, aah, basi labda bahati mbaya hakuweza kupatikana.

Tunao wageni kutoka Ethiopia, hawa ni viongozi wa Tume ya Maadili na Kuzuia Rushwa ya Nchi ya Ethiopia, ambao ni ndugu Girma Worku, karibu sana, karibu sana, Afisa wa Tume ya Maadili na ndugu Farnose Hassan.

We are very happy to welcome you brothers from Ethiopia; it is a pleasure to receive you here. We have been learning from you and you also have been learning from us and this is all in the spirit of African Unity. Thanks and have a pleasant stay in our country.

Maafisa kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Tanzania, ni ndugu Getrude Ishengoma, Mwanasheria Mwandamizi wa Serikali, mwenyeji wao huyu, ahsante sana. Ndugu Salvatory Kilasara, Afisa Uchunguzi labda anaendelea huko nje kuchunguza, ndugu Waziri Kipacha, Afisa Mfawidhi hapa Dodoma, ahsante sana na karibuni.

Pia tuna Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, ndugu James Kazoba, Mjasiriamali lakini pia Kada wa CCM kutoka Ukerewe, yule pale mkono wa kushoto, karibu sana.

Kuna wageni wa Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi ambaao ni Lilian Lwanji, sasa hapa inasema mke wake isije ikawa tena Mkwe, ni Mke sawasawa na mwingine ni ndugu Mallale Diallo, Mwenyekiti wa Serikali katika Kijiji cha Mkajenga.

Wapo wageni wa Mheshimiwa Benson Mpesa, Mbunge wa Mbeya Mjini, ambaao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kama ifuatavyo: ndugu Simon Baisi ambaye ni Mwenyekiti wa Serikali ya Wanachuo Dodoma, aah, ahsante sana, karibu sana Mwenyekiti wa Serikali ya Wanachuo. Yupo ndugu Joseph Marwa, Katibu Mkuu Serikali ya Wanachuo, yule pale karibu sana viongozi na ndugu Verian Bildad, Katibu wa Fedha wa Serikali hiyo hiyo ya Wanafunzi. Ahsante sana, karibuni sana na tunawatachia mema na mafanikio katika uongozi wenu na zaidi katika masomo ili mjiunge na jamii na kuweza kuendeleza maendeleo ya nchi.

Wapo wanafunzi 55 na walimu watatu kutoka shule ya Sekondari ya Tubuyu Morogoro, sijui ni jina sahihi hili Tubuyu! Aah, ndiyo, karibuni sana, nadhifu kabisa, ahsante tunawaombeeni vema katika masomo na pia mjifunze maadili, ili tuendelee kupata kizazi chenye maadili mema, karibuni sana.

Wapo Wanafunzi kutoka shule ya Chekechea ya Azania *Front Dar es Salaam*, na Walimu wao, aah, ndiyo wale pale, ahsante sana, ahsante sana, basi wajukuu zangu mnaanza vizuri. Ni vizuri kuanza kwenye shule ya Chekechea halafu unakwenda shule ya Msingi, Sekondari na baadaye unakwenda elimu ya juu. Tunawaombea mema, muwasikilize Walimu wenu, muwe na nidhamu na mtafanikiwa.

Huo ndiyo mwisho wa matangazo ya wageni, matangazo mengine; leo kutakuwa na kikao cha Kamati ya Uongozi, hapana siyo leo, kesho saa saba, samahani. Kamati ya Uongozi *Steering Committee* ya Bunge, itakuwa na Mkutano kwenye Ukumbi wa Spika, kesho saa saba, *Steering Committee*, Kamati ya Uongozi kesho saa saba mchana.

Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Katibu Msaidizi wa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi, ameomba nitangaze kwamba Kamati ya Uongozi wa Wabunge wa CCM, itakuwa na kikao leo mchana Saa saba katika Ukumbi wa Spika. Saa saba Mchana Kamati ya Uongozi ya *Caucus* ya CCM. Huo ndiyo mwisho wa matangazo na sasa nitamuita Katibu atuongoze kwa shughuli inayofuata.

MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.3) ya Mwaka 2010. [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No.3) Bill, 2010*]

SPIKA: Ahsante, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba, katika *briefing* tuliwaeleza juu ya Miswada ambayo itakuja hapo baadaye katika Mkutano huu. Kwa hiyo, wa kwanza ambao unasomwa mara ya kwanza ni Muswada huo na nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, ama Mwanasheria Mkuu, aah basi unasomwa mara ya kwanza, hivyo huna haja ya kuja Mheshimiwa, nimeghafilika. Kwa hiyo, endelea na Muswada wa pili.

Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma wa mwaka 2010 [*The Public Procurement Bill, 2010*]

SPIKA: Kwa hiyo, Muswada huo wa Sheria ya Manunuzi sasa umesomwa mara ya kwanza, endelea Katibu.

Muswada wa Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Kampuni Binafsi wa Mwaka 2010. [*The Public Private Partnership Bill, 2010*]

(*Miswada mitatu iliyotajwa hapo juu ilisomwa
kwa Mara ya Kwanza*)

SPIKA: Kwa hiyo, Muswada huo wa Sheria ya Ubia kati ya Serikali na Kampuni Binafsi wa Mwaka 2010 nao umesomwa kwa mara ya kwanza. Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2010/2011- Wizara ya Katiba na Sheria

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kuitisha Mpango na makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2010/11.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuishukuru kwa dhati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, ni matumaini yangu kuwa wananchi wa Mpwapwa wataona busara na muhimu ambao mimi na wenzangu tunauona kwa Mheshimiwa Lubeleje na kumchagua tena ili arudi Bungeni na kuiongoza Kamati hii kwa mara nyingine. Kama hii imefanya kazi kubwa ya kuichambua bajeti ya Wizara yangu kwa kina na kuafiki kuipitisha Bajeti hiyo ya makadirio ya mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2010/11. Wizara yangu kama ambavyo ilivyokuwa inafanya kila siku itazingatia na kutekeleza ushauri na maoni yaliyotolewa na Kamati kwa lengo la kuongeza ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiki ni kikao cha mwisho cha Bunge hili la tisa kabla halijavunjwa, niruhusu nichukue nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwanza kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kunitfea mara mbili kuwa mmoja wa Washauri wake Wakuu katika sekta ya Katiba na Sheria. Katika kipindi hiki cha miaka mitano nimejifunza mengi sana kutoka kwake na mimi nategemea kuwa nimetoa mchango uliotegemewa katika kumsaidia yeye kutimiza majukumu yake kama kiongozi mkuu wa nchi yetu na pia kutimiza malengo tuliojiwekea katika Ilani yetu ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005. Pili napenda nimshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Ali Mohamed Shein ambaye katika kipindi hiki cha miaka mitano, amekuwa mfano mkubwa kwangu wa uelewa, umahiri na uvumilivu katika uongozi.

Aidha, nachukua nafasi hii kumshukuru Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda kwa uongozi wake na maelekezo yake mahiri katika utendaji wangu wa kazi wa siku hadi siku. Katika safu hii pia sina budi kumshukuru sana kaka yangu Jaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania Mheshimiwa Jaji Augustino Ramadhani kwa ushirikiano wa karibu sana alionipa na kunirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu kama Waziri wa Sekta hii katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, vile vile nawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote pamoja Majaji na Mahakimu na Maafisa wa Serikali wote ambao katika kipindi hiki wamenipa ushauri na ushirikiano mkubwa ulioniwezesha nitekeleze majukumu yangu kwa umakini kama Waziri wa Katiba na Sheria. Wote nawashukuru sana na nawaombea Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya pekee kabisa napenda niwashukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema, Katibu Mkuu wangu ndugu Oliver P.J. Mhaiki, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndugu George Masaju na Mkurugenzi wa Mashtaka ndugu Eliezer M. Feleshi ambao nimefanya nao kazi kwa karibu sana na leo hii tumeifikisha sekta ya sheria hapa tulipofika. Mwisho kabisa napenda nimshukuru msaidizi wangu Kamana Stanley Kamana kwa umakini na uvumilivu wake mkubwa. Wote hawa nawaombea baraka za baba Mungu wetu, Amina.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuungana na Wabunge wenzangu kuwapongeza viongozi wetu wa Chama na Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya tangu wateuliwe kushika nyadhifa mbalimbali. Ni matumaini yangu kwamba bado wananchi wana imani na Chama chetu cha Mapinduzi, pamoja na Wabunge wake, hivyo ni matarajio yangu kuwa watatupigia kura tena kuendelea kuwawakilisha katika kipindi kijacho cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri walionitangulia kuwasilisha hoja zao, hususan Waziri wa Fedha na Uchumi Mheshimiwa Mustafa Mkulo, Mbunge wa Jimbo la Kilosa, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo

Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa hotuba zao ambazo zimeweka bayana sera, malengo na mwelekeo wa ujumla na mikakati ya Serikali katika kukuza uchumi na kuinua maisha ya wananchi. Pia napenda nichukue fursa hii kuwashukuru Mawaziri wote walioeleza mikakati ya Wizara zao katika kuleta maendeleo ya wananchi, mikakati hiyo ni mojawapo ya sehemu muhimu katika kufanikisha mipango na shughuli za maboresho ya sekta ya sheria hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii ni bajeti ya kwanza tangu Taifa letu kuondokewa na aliyekuwa Makamu wa Rais na Waziri Mkuu na aliyekuwa Mbunge wa kwanza wa Jimbo langu la Nachingwea, Simba wa Vita hayati Rashid Mfaume Kawawa, nachukua fursa hii kuungana na wenzangu waliotangulia kutoa rambirambi kwa ndugu, jamaa, marafiki na Watanzania wote kwa kumpoteza Mzee huyo. Aidha nachukua nafasi hii kutoa salamu za pole kwa ndugu, jamaa na wapiga kura Jimbo jirani la Ruangwa kwa kumpoteza Mbunge wao na rafiki yangu Sigfrid Selemani Ng'itu aliyetangulia mbele za haki mwishoni mwa mwaka jana, Mungu azilaze roho za marehemu hawa mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Wizara yangu imeendelea kuwa mhimili mkuu wa kuhakikisha kuwa usalama, utulivu na uzingatiaji wa utawala wa sheria hapa nchini unaendelea kuwapo. Pamoja na nchi yetu kushuhudia kuwepo kwa mtikisiko wa uchumi ulioikumba dunia nzima nchi yetu iliendelea kuwa tulivu na kuendeshwa kwa kuzingatia utawala wa sheria. Napenda niwashukuru sana viongozi wetu wakuu kwa jitihada zao kubwa walizozifanya kuwezesha nchi yetu kutoteteraka katika kipindi kile kigumu kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutekeleza ahadi za Chama Tawala zilizomo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2005, inayoelekeza Wizara kutekeleza maeneo manane muhimu katika kuiboresha Sekta ya Sheria katika utoaji wa huduma bora zaidi kwa jamii. Katika kutekeleza malengo hayo, Wizara kwa mwaka 2009/2010 imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za Kisekta zinaimarishwa na kuendelezwa. Maeneo yenye maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ni pamoja na marekebisho ya Sheria ya Mirathi na Sheria zote zinazoonekana kuwakandamiza wanawake; kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara; kuanzisha Mahakama Kuu katika kila Mkoa; kutenganisha shughuli za Upelelezi na uendeshaji Mashtaka; kutekeleza Programu ya Uboreshaji wa Mfumo wa Sheria; kuziimarisha na kuzioanisha sheria zinazohusiana na mapambano dhidi ya rushwa; kuweka mfumo wa kuwasaidia wananchi wasiojiweza kupata msaada wa Kisheria; kutumia Wanasheria wenyе Shahada ya Kwanza ya Sheria katika Mahakama za Mwanzo na kukuza, kulinda na kuhifadhi Haki za Binadamu na Utawala Bora katika jamii.

Mheshimiwa Spika, kuzifanyia marekebisho Sheria za Mirathi na sheria zote zinazoonekana kuwakandamiza wanawake. Napenda nilitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ya Chama Tawala cha CCM katika kutimiza ahadi zake kwa wananchi imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za utekelezaji wa kazi ya kutazama upya Sheria

za Mirathi na ndoa. Mchakato wa kukusanya maoni ya wananchi kuhusu sheria hizo unaendelea na unatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha wa 2010/11.

Mheshimiwa Spika, kulipatia Ufumbuzi Suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara. Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka jana, Serikali haina kipingamizi kwa uongozi wa dini ya kiislamu kuanzisha mahakama au Ofisi ya kadhi Tanzania Bara. Mara baada ya hotuba yangu ile ya mwaka jana Mheshimiwa Waziri Mkuu alikutana na Viongozi Wakuu wa Dini ya Kiislamu walioongozwa na Sheikh Mkuu, na ilikubaliwa kuwa viongozi hao wangeanzisha mchakato wa kuanzisha Mahakama ya Kadhi. Kwa taarifa tulizonazo ni kuwa jopo la wanazuoni wa kiislamu wanaziangalia na kuzihuisha sheria za kiislamu zinazohusiana na ndoa, mirathi na urithi kwa madhumuni ya kuziorodhesha ili zitambuliwe chini ya sheria ya *Islamic Laws Restatement Act*. Ni matarajio yangu kuwa kazi hii itakamilika katika mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, kutekeleza Mpango Maalumu wa kuanzisha Mahakama Kuu katika kila Mkoa. Mpango maalum wa Serikali wa kuanzisha Mahakama Kuu katika kila mkoa kwa lengo la kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi umekuwa na mafanikio ya kuridhisha. Mwaka jana niliahidi katika Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa Mahakama Kuu katika Mikoa ya Mara, Singida na Mtwara kupitia Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria na mradi endelevu wa kuboresha Mahakama ungeanza. Napenda kutoa taarifa kuwa hadi sasa hatua ya kwanza ya mchakato wa kumpata mshauri mwelekezi zimekamilika na ripoti imepelekwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali cha kuendelea na hatua ya mwisho ya kumpata Mshauri mwelekezi atakayefanya marejeo ya michoro. Ni matarajio yangu kuwa kazi ya ujenzi itaanza katika mwaka wa fedha 2010/2011.

Aidha, pamoja na utekelezaji wa Mpango wa kuanzisha Kanda za Mahakama Kuu kwa kila mkoa, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mahakama za mwanzo mbili za Lugoba-Bagamoyo na Karabagaine-Bukoba, ambazo zimefikia hatua za mwisho za ukamilishaji. Ujenzi wa nyumba ya Hakimu katika Mahakama ya Lugoba, Bagamoyo umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara yangu kupitia Mahakama imeamua kuendelea kukamilisha majengo ya Mahakama za Mwanzo zilizojengwa na wananchi huko Tingi - Mbinga, Mbondo-Nachingwea, Kirando-Nkasi, Sopa, Laela na Msanzi - Sumbawanga, Robanda Wilayani Serengeti na Itaka-Mbozi badala ya kuanza ujenzi mpya katika Mahakama za Mwanzo Machame na Katesh.

Mheshimiwa Spika, chini ya mradi endelevu wa kuboresha Mahakama zetu upanuzi wa jengo la Mahakama ya Rufani Dar-es salaam umekamilika na samani za ofisi zimewekwa na jengo kukabidhiwa rasmi tarehe 17 Machi, 2010. Aidha, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mafia na Mahakama ya Hakimu Mkazi Manyara upo katika hatua za ukamilishaji. Kazi ya ukarabati wa Mahakama za Mwanzo sita za Tanga Mjini, Ikugi-Singida, Lisekese-Masasi, Lembeni-Mwanga na Mabamba-Kibondo umekwisha kukamilika na tayari majengo haya yameshaanza kutumika.

Aidha, Mahakama ya Mwanzo ya Kyela iliyochomwa moto na wananchi imeshakarabatiwa na inatumika. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 kazi zifuatazo zitafanyika: kuendelea na ujenzi wa Mahakama Kuu Shinyanga ambapo tumetenga shilingi bilioni 1.3 pamoja na ukamilishaji wa ujenzi wa Mahakama Kuu Bukoba shilingi milioni 500, kufanya marejeo ya michoro kwa ajili ya Mahakama Kuu na ujenzi wa Mahakama ya Rufani chini ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria na kuanza ujenzi wa Masijala ya Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara, Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo ishirini zilizotarajiwa kujengwa mwaka jana 2009/10 chini ya Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria za Kawe-Kinondoni, Kigamboni-Temeke, Maili Moja-Kibaha, Kisarawe, Gairo-Morogoro, Mwanga-Mwanga, Usevya-Mpanda, Mkomazi-Korogwe, Lukuledi-Masasi, Terrati-Simanjiro, Makuyuni-Arusha, Mafinga-Mufindi, Makongorosi-Chunya, Bunda Mjini, Sangabuye-Ilemela, Ulyankulu-Urambo, Songea Mjini, Buguruni-Ilala, Bariadi mjini, Mtowisa-Sumbawanga na Namanyere-Nkasi hazikujengwa kutoptaka na kuchelewa kupata kibali toka Benki ya Dunia kwa ajili ya kumpata mshauri na Mkandarasi wa Ujenzi.

Aidha, Serikali inatarajia kuanza ujenzi wa Mahakama hizi baada ya kupata kibali kutoka Benki ya Dunia kwa mwaka wa fedha 2010/11. Hata hivyo kazi hii tunategemea itafanyika chini ya mpango wa sasa ambapo kila Mahakama ya mwanzo itakayojengwa itaambatana na ujenzi wa nyumba ya Hakimu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya mwaka jana nililieza Bunge lako Tukufu kuhusu mchakato wa kutenganisha jukumu la upelelezi na mashtaka ambao utasaidia kuondoa tatizo la upelelezi kuchukua muda mrefu na kusababisha mashauri kuchukua muda mrefu mahakamani na kufanya haki isipatikane kwa wakati. Chini ya mpango huu, Mawakili wa Serikali watahusika na uendeshaji wa mashauri ya makosa ya Jinai katika ngazi za Mahakama za Wilaya na Mahakama za Mahakimu Wakazi na Polisi pamoja na vyombo vingine vinavyohusika na upelelezi wa makosa ya jinai watabaki na jukumu la kazi ya upelelezi.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Mpango huu na kuufanya kuwa endelevu na wenyewe mafanikio, jitihada za kutafuta majengo ya Ofisi katika mamlaka za miji na wadau mbalimbali katika Mikoa ya Pwani, Morogoro, Manyara, Kigoma na kwenye wilaya za Korogwe, Nzega, Mbinga, Njombe, Tunduru, Kahama, Bariadi, Geita, Magu, Rombo, Same, Monduli, Ilala Kinondoni, Temeke, Kibondo, Igunga, Misungwi, Handeni, Lushoto na Arumeru (Arusha) zilifanyika. Aidha, hatua za kuyaandaa majengo hayo kuwa tayari kwa ajili ya kutumika kama Ofisi zinaendelea. Hadi sasa zoezi hili limepata mafanikio kutoptaka na msaada mkubwa uliotolewa na Serikali Kuu, Mamlaka ya Miji na Wilaya pamoja na Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria nchini (*Legal Sector Reform Programme*).

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika kutekeleza jukumu la mapitio ya sheria mbalimbali na kuandaa Miswaada ya Sheria imefanikiwa kufanya mapitio ya kuzainisha, kuziimarisha na kuzioanisha sheria mbalimbali zinazohusu mapambano dhidi ya rushwa kama vile Sheria dhidi ya Usafirishaji wa Fedha Haramu (*Cap.432*) Na.12 ya mwaka 2006, Sheria ya Uchaguzi (*Cap.343*) Na.1 ya mwaka 1985, Sheria ya Vyama vya Siasa (*Cap. 258*) Na.5 ya mwaka 1992, Sheria ya Mawakili (*Cap.341*) Na.25 ya mwaka 1954, na Sheria ya Mashirika na Taasisi zinazotoa Msaada wa Kisheria kwa Umma (*Cap.21*) Na.21 ya mwaka 1969. Aidha, Wizara yangu imekuwa ikifanya kazi ya kuzitafsiri baadhi ya Sheria zilizopo na zinazopitishwa na Bunge kwa kuwezesha urahisi wa watumiaji mbalimbali. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa agizo la Bunge lenye lengo la kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, ni vema ikaeleweka kuwa Sheria nyingi zilizopo, isipokuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na marekebisho yake zipo katika lugha ya Kiingereza ambayo hajulikani kwa wananchi wengi. Kazi ya kutafsiri Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 kutoka lugha ya Kiswahili kwenda lugha ya Kiingereza ilikamilishwa. Jumla ya sheria kumi na nne (14) zilitafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili. Sheria hizo ni Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343 pamoja na Kanuni zake mbili; Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Sura ya 292 pamoja na Kanuni zake mbili; Sheria ya Gharama za Uchaguzi ya mwaka 2010 pamoja na Kanuni zake mbili; Kanuni za Baraza la Ardhi na Nyumba; Kanuni za Taasisi ya Mifupa Muhimbili (Usimamizi, Udhibiti na Utawala).

Mheshimiwa Spika, Sheria nyingine ni Sheria ya Tafsiri ya Sheria, sura ya 1; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, sura ya 20; Sheria ya Upangaji wa Matumizi ya Ardhi, Sura ya 116 na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Sura ya 2. Sheria za Uchaguzi na Kanuni zake zimewasilishwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi kwa ajili ya kuzipitia na kujiridhisha kabla ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali. Iteleweke kuwa Sheria hizi zilikuwa katika mchakato wa kufanyiwa marekebisho, hivyo tulilazimika kutozitangaza katika Gazeti la Serikali mpaka marekebisho hayo yakamlike. Kwa upande wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi na Kanuni zake ninayo furaha kubwa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa tupo katika hatua za mwisho za matayarisho kabla ya kupelekwa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Kadhalika, Sheria ya Tafsiri ya Sheria na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai nazo zipo katika hatua za mwisho za uhakiki kabla ya kupelekwa kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Aidha, katika mwaka wa fedha ujao 2010/11, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007 inayohusu mapambano dhidi ya rushwa itafanyiwa tafsiri katika lugha ya Kiswahili ili wananchi wengi waweze kuielewa. Hatua hiyo itaimarisha jitihada za Serikali katika kuzuia na kupambana na rushwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10 utekelezaji wa Programu ya Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Sheria hapa nchini umekuwa ukisaidia kuimarisha mchakato wa utenganishaji wa Uendeshaji wa Mashtaka na Upelelezi kwa kuwezesha uanzishaji wa ofisi katika wilaya na mikoa kama ilivyoainishwa kwenye ibara ya 14 ya

maelezo ya mpango wa utenganishaji wa shughuli za uendeshaji wa Mashtaka na upelelezi. Aidha mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria umesaidia mchakato wa kumpata Mshauri Mwelekezi aliyetathimini mpango wa ukarabati wa majengo ya Ofisi tatu za Mikoa na ofisi 10 za Wilaya. Kazi hii imehusisha Mikoa ya Pwani, Iringa na Manyara na Wilaya za Monduli, Korogwe, Handeni, Temeke, Misungwi, Geita, Bariadi, Mbanga na Lushoto.

Hali kadhalika, programu hii imeliwezesha Jeshi la Polisi kutoa mafunzo maalum ya mbinu za kisasa za upelelezi kwa kuzingatia haki za binadamu ambapo jumla ya Maafisa Waandamizi 40 walipatiwa mafunzo ya ukufunzi (*Training of Trainers Course*) ili kuwezesha jeshi kuwa na mpango endelevu wa kuwapatia mafunzo maafisa wake kila mwaka. Pia katika kipindi hicho, Wizara kupitia programu hii, imeliwezesha Jeshi la Polisi kujenga kituo kimoja cha Polisi cha wilaya ya Bahi na kujenga vyumba maalum vya kuhifadhia watoto wanaojikuta katika migogoro na Sheria za nchi (*Juvenile Offenders*) katika vituo vitatu vya Polisi katika mkoa wa Dar-es salaam. Mchakato wa ujenzi wa Chuo cha Mafunzo ya Upelelezi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Kituo cha Mafunzo cha Polisi (*Police Model Station*) katika chuo hicho uko katika hatua ya kumpata mshauri mwelekezaji atakayesimamia ujenzi huo.

Aidha, Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria umeendelea kuboresha mfumo wa usafirishaji na usindikizaji wa Mahabusu na Wafungwa kwenda kusikiliza mashauri yao kwa kulipatia Jeshi la Magereza mabasi makubwa mawili (2) ya kisasa. Pia mchakato wa ununuzi wa magari mengine kumi na mawili (12) yatakayohusisha mabasi makubwa matano (5), madogo matano na magari madogo mawili (*Pick up*) ya usindikizaji uko katika hatua za mwisho kukamilika ambapo tathimini ya kumpata Mkandarasi wa Ununuzi wa magari hayo imeishafanywa na hatua iliyobaki ni kuingia mkataba na Mkandarasi atakayepitishwa na Bodi ya Ununuzi.

Mchakato huu utakamilika mwaka wa fedha 2009/10. Moja ya malengo ya Programu hii kwa mwaka huu wa fedha 2010/11 ni kuboresha usimamizi wa programu katika maeneo ya Sheria, Ununuzi, Fedha na Jinsia, ili kuhakikisha kwamba inatekeleza mipango yake ipasavyo. Wataalam washauri katika maeneo husika wameajiriwa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa maeneo hayo yanafanyiwa kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10 Wizara kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iliendelea na juhudhi za kukuza, kulinda na kuhifadhi Haki za Binadamu na Utawala Bora katika jamii. Tume iliendelea kushughulikia malalamiko ya wananchi ambapo jumla ya malalamiko mapya na ya zamani 7,858 yалишхуліківа. Kati ya hayo 1,003 yалихитишва na malalamiko 6,855 yалиобаки yanaendelea kushughulikwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Tume ilianzisha utaratibu wa kusajili malalamiko kwa kutumia kompyuta na kutumia maafisa uchunguzi katika kufuatilia malalamiko. Aidha, Tume ilifanya tafiti zinazolenga kulinda na kuendeleza haki za binadamu na utawala bora sanjari na kutoa ushauri wa kisheria kwa wanaohitaji ikiwa ni pamoja na kuelimisha wananchi juu ya masuala yanayohusu Haki za Binadamu na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010 Wizara yangu ilitekeleza majukumu yanayohusu uzingatiaji wa haki za binadamu na za kiraia. Aidha, Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitoa utetezi mbele ya Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu huko Banjul, Gambia kuhusiana na mashauri mawili yaliyofunguliwa katika Tume hiyo dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Shauri la kwanza lilifunguliwa na Mtanzania aitwaye Sophia Moto akishirikiana na Mtandao wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali ya Kusini mwa Afrika (*SANGONET*) akitaka mwanaume asiye raia wa Tanzania kupewa haki ya uraia wa Tanzania kama ilivyo kwa mwanamke wa kigeni anapooana na Mtanzania. Tume imekubaliana na utetezi wetu na ikalitupilia mbali shauri hilo.

Mheshimiwa Spika, shauri la pili lilifunguliwa na Mtandao mwingine wa Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ya kutetea Haki za Binadamu Kusini mwa Afrika (*SAHRINGON*) ambapo Mtandao huo ulikuwa ukipinga Hukumu iliyotolewa na Mahakama ya Rufaa ya Tanzania katika Shauri la Dominic Mbushuu na Mwenzake ambayo inahalalisha adhabu ya kifo dhidi ya washitakiwa wanaopatikana na hatia ambazo adhabu yake ni kifo. Baada ya kuwasilisha utetezi wetu sasa tunasubiri uamuvi wa Tume hiyo.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilianda taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Mikataba/Maazimio mbalimbali ya Kimataifa ya Haki za Binadamu na za Kiraia yaliyordhiwa na nchi yetu. Taarifa hizo ziliwasilishwa katika Sekretarieti ya Umoja wa Mataifa ya Haki za Binadamu na Tume ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu. Maazimio yanayohusika na taarifa hizo ni “*International Convention on Elimination of all forms of Racial Discrimination*” (CERD), “*International Covenant on Civil and Political Rights*” (ICCPR), na *International Convention on Economic, Social and Cultural Rights*” (ICESCR).

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi hutumika kuzitolea maeleo tuhuma mbalimbali dhidi ya Serikali zinazowasilishwa kwa taasisi za kimataifa na watu au taasisi mbalimbali kuhusiana na matukio yanayotokea katika jamii yetu. Lengo la kuhudhuria vikao hivi na kutoa taarifa ni kueleza namna ambavyo Serikali yetu inatekeleza mikakati mbalimbali ya kimataifa inayohusu Haki za Binadamu katika kukuza na kulinda haki hizo, kutetea nchi yetu pale tuhuma za ukiukwaji wa haki za binadamu zinapotolewa dhidi yake ili kuiweka nchi yetu katika sifa nzuri, na kuendeleza ushirikiano wa Kimataifa ikiwa ni pamoa na kujifunza uzoefu wa nchi nyingine duniani zinavyotekeliza matakwa ya Mikataba au Maazimio haya. Hali kadhalika jukumu hili litaendelezwa katika mwaka wa fedha ujao 2010/11.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10 Wizara ilikamilisha uanzishaji wa Divisheni ya Huduma za Kisheria kwa Umma (*Public Legal Service Division*) kwa ajili ya kuratibu utoaji huduma za ushauri wa kisheria kwa jamii ya watu wasio na uwezo wa kulpia huduma hizo ili kufanikisha azma ya Wizara ya haki sawa kwa wote. Divisheni hii imekua kiungo muhimu kinachowezesha taasisi mbalimbali za

watu binafsi na vikundi vinginevyo nchini vinavyotoa msaada wa kisheria kutekeleza majukumu yao vyema. Aidha, Wizara imeendelea na mchakato wa kutayarisha utaratibu maalum chini ya sheria ili kuanzisha kada ya Mawakili Jamii (*Paralegals*) ili waweze kutoa huduma na elimu ya sheria kwenye maeneo mbalimbali nchini hususan maeneo ya vijiji ambako kwa kawaida hakuna huduma za Mawakili wa Kujitegemea (*Advocates*).

Mheshimiwa Spika, kama nilivylitaarifu Bunge lako Tukufu mwaka jana kuhusu kukabili ana upungufu wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na pia kuimarisha dhana nzima ya uwakilishi Mahakamani, Wizara yangu inakusudia kuajiri wahitimu wa Shahada ya Kwanza ya Sheria kuwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Mchakato wa kutimiza azma hii unaendelea na sasa Wizara kwa kushirikiana na Mahakama inasubiri kuidhinishwa kwa mapendekezo ya Muundo wa Utumishi mpya wa kutekeleza mkakati huo uliowasilishwa Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Ikiwa Muundo huo utaidhinishwa utachangia kupunguza tatizo la uhaba wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na kuwezesha wahitimu wa Shahada ya Kwanza ya Sheria kupata ajira. Aidha, itabidi Sheria mbalimbali husika zifanyiwe marekebisho kabla ya wanasheria hao kuajiriwa kuwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza dira na majukumu yetu, Wizara yangu bado inakabili na changamoto nyingi katika vyombo vyake vya utoaji haki nchini. Aidha, changamoto nyingi zinazoikabili Wizara ni pamoja na uwezo mdogo wa Serikali kifedha na rasilimali watu katika vyombo vyake vya utoaji haki kwa wananchi wake na kusababisha kuendelea kuwepo kwa mlundikano wa mashauri ya jinai na madai kwa kiwango kikubwa, kunakotokana na ucheleweshaji wa kusikiliza mashauri, kutatua migogoro ya ardhi na mashauri ya kazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na ongezeko la idadi ya Majaji, Mahakimu, Mawakili wa Serikali na watumishi wengine bado uwezo wa Serikali kifedha ni mdogo kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi katika utoaji wa haki hapa nchini. Pia Wizara yangu ina upungufu wa nyenzo za kufanya kazi kama magari, ofisi, samani na nyumba za watumishi. Changamoto hizi zinaathiri utekelezaji wa azma ya Serikali ya upatikanaji wa haki kwa wote mapema na kupunguza tija ya Taasisi mbali mbali zilizoko chini ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2009/10 ilikuwa na malengo ya kuongeza ufanisi katika uanzishaji wa utoaji wa ushauri wa kisheria nchini, utayarishaji wa miswada ya sheria na Hati mbalimbali za Serikali, uendeshaji wa mashauri nchini, utafiti na mapitio ya sheria mbalimbali, uboreshaji wa shughuli za Usajili, Ufilisi na Udhamini ushauri wa Mikataba mbalimbali nchini. Pia Wizara ilikuwa na malengo ya kuboresha mfumo wa Habari, Elimu na Mawasiliano kwa jamii, utekelezaji wa miradi ya maendeleo, usimamizi wa vyuo vya mafunzo na ufuatiliaji wa masuala mtambuka na maendeleo ya watumishi. Wizara yangu kwa mwaka 2010/2011

itaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuboresha mfumo wa Sheria kwa lengo la kusimamia utoaji wa haki na kuimarisha utawala bora nchini kwa kutekeleza majukumu yaliyoainishwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, katika uimarishwaji wa utoaji wa ushauri wa kisheria kwa Serikali na Taasisi zake, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali iliendelea kutoa ushauri wa mambo ya kisheria yanayohusu masuala ya Katiba na Haki za Binadamu, uendeshaji wa mashauri ya madai na jinai, uandishi wa sheria, uhuishaji na tafsiri ya sheria, uandaaji na uchambuzi wa mikataba mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Maombi 511 ya ushauri wa mambo mbalimbali ya kisheria yalipokelewa, kati ya hayo 468 yalifanyiwa kazi na maombi 43 yaliyobaki yanaendelea kushughulikiwa.

Aidha, ushauri wa kisheria ultolewa katika timu za wataalam zenyenkuhusisha sekta mbalimbali ambazo zinahusika katika majadiliano ya mikataba. Pia katika mwaka wa fedha 2009/2010, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali ilishiriki katika uendeshaji wa mashauri ya madai katika Mabaraza na Taasisi za kikanda na katika Mahakama za Kimataifa za Usuluhishi. Vile vile, katika kuhakikisha kwamba nchi inatoa huduma bora ya kisheria kwa wananchi wake mapema, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali iliendelea kujengewa uwezo wa kuajiri watumishi wenye sifa na taaluma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali itaendelea kuimarisha eneo la utoaji wa ushauri wa kisheria kuhusu masuala ya mikataba, Katiba na Haki za Binadamu, uandishi na uhuishaji wa sheria na kuiwikilisha Serikali katika mashauri mbalimbali ya jinai na madai ndani na nje ya nchi kwa kuwajengea uwezo wa kitaaluma Mawakili wa Serikali na Waendesa Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, utayarishaji wa Miswada ya Sheria na Hati mbalimbali za Serikali. Katika mwaka 2009/10, Miswada 37 iliandaliwa na Miswada 18 ilipitishwa na Bunge lako Tukufu na kuwekwa saini na Mheshimiwa Rais kuwa sheria. Miswada mingine 19 iliandaliwa na kupitia hatua mbalimbali katika mchakato wa kuiwezesha kujadiliwa Bungeni. Aidha, Sheria 50 zilifanyiwa marekebisho na Sheria Ndogo 500 ikiwa ni pamoja na Hati mbalimbali za Serikali zilihakikiwa na baadaye kuchapishwa katika Gazeti la Serikali. Zoezi la urekebu wa Sheria linaendelea na juzu za Sheria za mwaka 2009 ziko mbioni kutolewa. Maandalizi ya sheria mbalimbali ikiwa ni pamoja na Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 yalifanywa. Sheria hii ni matokeo ya kazi kubwa ya kuzioanisha Sheria mbalimbali za watoto zilizokuwepo awali kwa lengo la kuondokana na tatizo la kukinzana kwa baadhi ya vifungu vya Sheria hizo ilhali zikimlenga mtoto.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11, Wizara itaendelea na majukumu ya uandishi wa Miswada ya Sheria, uandaaji Hati mbalimbali za Serikali, uandaaji wa Sheria Ndogo zinazotungwa na mamlaka nyingine pamoja na kutafsiri baadhi ya Sheria katika lugha ya Kiswahili. Jumla ya Miswada ya Sheria 30 na Sheria Ndogo 520 zitaandaliwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Ofisi hii pia itatafsiri Sheria 20 katika lugha ya Kiswahili ili wananchi wengi waweze kuzisoma na

kuzielewa. Aidha, maazimio ya Bunge kuridhia Mikataba ya Kimataifa yataandaliwa na kuwasilishwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Serikali imeiwezesha Mahakama ya Rufani kutekeleza jukumu lake la utoaji haki na utawala wa sheria. Katika kipindi hicho, jumla ya mashauri 2,624 yalipokelewa kati ya hayo, mashauri 627 yalihitimishwa na mashauri 1,997 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa katika vikao 13 kati ya vikao 16 vilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mahakama Kuu kulikuwa na jumla ya mashauri 18,502. Kati ya hayo, mashauri 8,754 yalisikilizwa na mashauri 9,748 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Utekelezaji huo ni matokeo ya vikao 76 kati ya vikao 136 vilivyopangwa. Aidha, kwa upande wa Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya kwa mwaka 2009/10 kulikuwa na jumla ya mashauri 62,154. Kati ya hayo, mashauri 46,977 yalisikilizwa na mashauri 15,177 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo zilikuwa na jumla ya mashauri 218,767 katika mwaka 2009/10. Kati ya hayo, mashauri 167,228 yalisikilizwa na mashauri 51,939 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Kutokana na umuhimu na ugumu wa kazi zinazofanywa na wazee wa baraza, Serikali imeamua kupandisha viwango vya posho vya Wazee wa Baraza kutoka shilingi 1,500 kwa kesi inayokamilika hadi shilingi 5,000 kuanzia mwaka ujao wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara kwa mwaka 2009/2010 ilikuwa na jumla ya mashauri 318. Kati ya haya mashauri 144 yametolewa uamuzi na mashauri 174 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara itaendelea kusikiliza mashauri na kutoa uamuzi wa haki kwa kutumia vyombo vya teknolojia ya kisasa; itaendelea kuziendesha masjala za Dar es Salaam, Arusha na Mwanza; kuendeleza na kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) na mtandao katika kuchukua na kutunza kumbukumbu mbalimbali. Aidha, Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara itaendelea na shughuli ya kukarabati jengo ambalo litatumika kuanzisha masjala ndogo Mbeya na itaanza ujenzi wa jengo la masjala ndogo Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi katika mwaka 2009/10 ilikuwa na jumla ya mashauri 5,250. Kati ya hayo, mashauri 1,109 yalihitimishwa na mashauri 4,141 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Vile vile, Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi ilifanya ukaguzi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba katika mikoa minane ya Rukwa, Mbeya, Iringa, Morogoro, Dodoma, Tabora, Shinyanga na Mwanza.

Aidha, Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi katika mwaka wa fedha 2010/2011 itaendelea kushughulikia migogoro ya Ardhi kwa kuhakikisha kuwa asilimia themanini (80%) ya mashauri yaliyosajiliwa yanahitimishwa pamoja na kutembelea Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Pia Mahakama ya Ardhi itawezesha Majaji na Wasajili

kuhudhuria kongamano la Kimataifa litakalofanyika Boston, Marekani mwezi Septemba,2010 na Zambia mwezi Mei 11,2011.

Mheshimiwa Spika, Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi chini ya utaratibu wa sheria za zamani za kazi kwa mwaka wa fedha 2009/2010, ilikuwa na jumla ya mashauri 280, kati ya hayo mashauri 169 yalihitimishwa na mashauri 111 yaliyobaki yataendelea kusikilizwa na Mahakama hiyo. Aidha, katika utaratatibu wa sheria mpya za kazi, Divisheni ya Mahakama ya Kazi ilikuwa na jumla ya mashauri 2,002, kati ya hayo mashauri 585 yalihitimishwa na mashauri 1,417 yaliyobaki yanaendelea kusikilizwa. Katika mwaka wa fedha 2010/2011 itaendelea kushughulikia majukumu yake ya utoaji haki. Kazi zifuatazo zitatekelezwa: kukarabati jengo lake lilopo Kinondoni na kupokea mashauri 800 ya kikazi ambapo asilimia sitini (60%) ya mashauri hayo yatasikilizwa na kuhitimishwa.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba ili kuongeza ufanisi katika kusikiliza mashauri mahakamani, mfumo wa kurekodi mwenendo wa mashauri umekwishaanza kutumika katika Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu Kanda ya Dar es salaam na Divisheni za Mahakama Kuu za Ardhi, Biashara na Kazi. Mfumo huu utaendelea kuimarishwa katika mwaka wa fedha 2010/2011 ili uendelee kutumika hadi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Mheshimiwa Spika, ili kupunguza mlundikano wa mashauri ya ardhi katika Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi, Mheshimiwa Jaji Mkuu ametoa mamlaka kwa Waheshimiwa Majaji wote wa Mahakama Kuu nchini kusikiliza mashauri ya ardhi. Ni matumaini ya Serikali kuwa hatua hii ya Mheshimiwa Jaji Mkuu itapunguza kama sio kumaliza mlundikano wa mashauri ya ardhi Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Wizara yangu kuitia Mahakama ya Tanzania itaendelea na jukumu lake la utoaji haki ambapo jumla ya vikao 18 vya Mahakama ya Rufani, vikao 214 vya Mahakama Kuu vitafanyika. Aidha, mashauri 27,000 katika Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya, mashauri 42,000 katika Mahakama za Mwanzo yatasikilizwa na kuhitimishwa. Pia vikao vya Kamati za kusukuma mashauri vitafanyika katika ngazi ya Kitifa, Kanda, Mkoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010, Tume ya Utumishi wa Mahakama imefanya vikao vitatu vya kawaida na kimoja cha dharura.Tume imeshughulikia mapendelekezo ya uteuzi wa Majaji 10 pamoja na Wasajili saba, Naibu Wasajili Mahakama ya Rufani sita, na Naibu Wasajili watatu wa Mahakama Kuu, Wakurugenzi wawili wa Mahakama za Wilaya na Mwanzo. Pia Tume imeajiri katika masharti ya kudumu na malipo ya pensheni na kuwabadilisha vyeo Mahakimu wa kada na ngazi mbalimbali 135, kati yao watumishi walioajiriwa walikuwa 59 na Mahakimu waliopandishwa vyeo walikuwa 76.

Pia iliwathibitisha kazini na katika cheo Mahakimu wa kada na ngazi mbalimbali 154 na kuwapandisha vyeo Mahakimu 119. Aidha, mashtaka ya nidhamu 12 yameshughulikiwa ambapo, Mahakimu wanane wamerejeshwa kazini kwa kufutiwa

tuhuma, Mahakimu watati wamefukuzwa au kuachishwa kazi na shauri moja (1) halijakamilika.

Mheshimiwa Spika, Tume imeshughulikia malalamiko nane kati ya malalamiko 11 yaliyopokelewa na imeratibu safari ya Makamishna nchi za Malaysia, Singapore na Philippines kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo. Tume inaandaa kituo cha Takwimu na mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano. Aidha, Tume imeratibu mafunzo ya kuwajengea uwezo Makatibu wa Kamati za Mahakama 22 katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa pamoja na Wilaya zake kuhusu namna ya kushughulikia malalamiko dhidi ya Mahakimu. Ziara ya kujitangaza katika Mikoa Miwili (2) ya Mtwara na Lindi imefanyika.

Mheshimiwa Spika, Tume imeratibu mafunzo na kazi ya kamati inayoshughulikia kutafuta mfumo mbadala wa upimaji utendaji kazi kwa Majaji na Mahakimu. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Tume itaendelea kushughulikia masuala ya uteuzi, kupandisha cheo, ajira, kuthibitisha kazini na nidhamu kwa Majaji, Maafisa wa Mahakama na Mahakimu pamoja na kujitangaza ili kutoa elimu kwa umma kuhusu kazi zake.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuiwakilisha Serikali katika mashauri ya madai. Kwa mfanu, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2009 hadi Mei 2010, jumla ya mashauri ya madai 293 yalipokelewa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali Makao Makuu pekee, kati ya hayo, mashauri 45 yalihitimishwa. Pia katika kipindi hicho jumla ya mashauri ya Katiba 33 yalifunguliwa Mahakamani. Kati ya hayo 28 yanaendelea kusikilizwa na Mashauri matano yanashubiri kutolewa uamuzi na Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, mashauri mengine mengi ya madai na Katiba yalipokelewa katika Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkoo wa Serikali baada ya kufunguliwa Mahakamani. Kadhalika vikao vya kuendesha mashauri ya jinai katika Kanda zote 14 vilifanyika ikiwa ni pamoja na kushughulikia matatizo ya msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani. Hadi kufikia mwezi Mei, 2010 jumla ya mashauri 12,172 yalikuwa yanaendeshwa na Mawakili wa Serikali katika Mahakama ishirini na mbili (22) za Wilaya na Hakimu Mkazi. Kati ya mashauri hayo 5,776 yamekwishaamuliwa na mashauri 6,356 yanaendelea kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali kuitia Divisheni ya Mashtaka iliendesha mashauri mbalimbali yakiwemo yale yanayohusisha madawa ya kulevyo, unyang'anyi wa kutumia silaha, uvuvi haramu, mauaji ya vikongwe na watu wenye ulemavu wa ngozi na aina nyinginezo nyingi za makosa ya jinai, Mashauri haya yaliendeshwa katika Mahakama mbalimbali hapa nchini. Aidha, mashauri ya jinai 1,605 yaliendeshwa na kusikilizwa katika vikao 65 vya Mahakama Kuu ambapo mashauri 606

yalitolewa uamuzi. Mashauri ya rufaa za jinai 3,525 yaliendeshwa katika ngazi ya Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu ambapo rufaa 1,239 ziliamuliwa.

Jumla ya matukio 43 yanayohusisha watu wenye ulemavu wa ngozi yameripotiwa nchini na Kati ya hayo moja linahusiana na mauaji ya mlemauvu wa ngozi limekwishasikilizwa na kutolewa hukumu na Mahakama ya Rufani na wahusika kupewa adhabu ya Kunyongwa. Shauri moja lilisikilizwa na Mahakama Kuu na wahusika kupewa adhabu ya kunyongwa. Mashauri tisa yanashubiri kupangwa kusikilizwa na Mahakama Kuu na mashauri 32 upelelezi wake bado haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, azma ya Serikali ya kuongeza nguvu ya uendeshaji wa mashauri ya rushwa na udanganyifu imetekelawa kwa kushirikiana na wadau wengine. Hadi kufikia mwezi Mei, 2010 jumla ya majalada 160 yanayohusisha makosa ya rushwa yaliwasilishwa kwenye Divisheni ya Mashtaka kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Kati ya hayo, majalada 45 yaliandaliwa hati za mashtaka, majalada 66 yalirudishwa kwa upelelezi zaidi, majalada matatu yalifungwa baada ya kuridhika kuwa ushahidi usingetosheleza kuthibitisha mashtaka. Majalada 46 yaliyowasilishwa Divisheni ya Mashtaka mwezi Aprili na Mei bado yanafanyiwa kazi.

Aidha, Divisheni ya Mashtaka iliendelea na mashauri 16 yanayohusisha rushwa kubwa na udanganyifu ikiwemo mashauri ya *EPA* na matumizi mabaya ya madaraka yaliyofunguliwa mahakamani mwaka 2008 na 2009. Miongoni mwa mashauri hayo, shauri moja limesikilizwa na kutolewa hukumu ambapo mtuhumiwa alipatikana na hatia na yaliyosalia yako katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Kwa mwaka wa fedha 2010/11 Divisheni ya Mashtaka itaendelea na uendeshaji utakaojumuisha mashauri ambayo hayajahitimishwa na mashauri mapya. Katika eneo la utekelezaji wa shughuli za kutoa ushauri kwenye uingiaji wa Mikataba ya Kitaifa na Kimataifa na uendeshaji wa mashauri nchini na nje ya nchi, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali imekuwa ikiokoa fedha nyangi za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mathalani, katika mwaka wa fedha 2009/2010 Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali katika Shauri la Madai Na. 1 la mwaka 2009 katika Mahakama ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC Tribunal*) huko Windhoek, Namibia. Serikali ilishinda shauri hilo lililokuwa limefunguliwa na Kampuni ya Mauritius iitwayo *CIMEXPAN* kwa kushirikiana na wadai wengine wawili amba ni *CIMEXPAN* (*ZANZIBAR*) *Limited* na AJAYE JOGOO dhidi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wadai hao walikuwa wakidai Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania jumla ya dola za Kimarekani milioni 936 ambazo ni sawa na fedha za kitanzania (trilioni moja, bilioni mia nne na nne) kama fidia ya kuvunjwa kwa mkataba wa uwekezaji, kuteswa na kufukuzwa nchini kwa aliyekuwa Mkurugenzi wa Kampuni hiyo ya Mauritius, Bwana AJAYE JOGOO, raia wa Mauritius, hukumu hiyo ilitolewa tarehe 11 Juni, 2010. Kwa kushinda shauri hilo la madai, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali imeokoa kiasi hicho kikubwa cha fedha za Umma. Yapo mashauri mengi ya madai na ya Kikatiba ambayo Serikali imekuwa ikipata ushindi Mahakamani na

hivyo kuokoa fedha nyingi za Umma. Ofisi hii inaimarisha kitengo chake cha takwimu ili siku za usoni tuweze kuonyesha kwa takwimu shughuli tunazozifanya na kiasi cha fedha tunazoziokoa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepanga kuboresha huduma za kisheria na kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa mashauri yote nchini yanayohusu Madai, Jinai, Katiba na Haki za Binadamu kwa lengo la kupunguza kero ya mlundikano wa mashauri mahakamani. Hatua zifuatazo zitatekelezwa:- kuweka mfumo endelevu wa kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zinazohusu makosa ya jinai, madai, Katiba na Haki za Binadamu; kutayarisha kanuni na miongozo kwa ajili ya Mawakili wa Serikali na waendesha mashtaka; kuimarisha utekelezaji wa mpango wa kutenganisha shughuli za uendeshaji wa mashtaka na upelelezi kwa mikoa ya Arusha, Shinyanga, Mwanza, Dar es salaam, Tanga, Tabora, Mbeya, Moshi, Ruvuma, Dodoma na Kagera na kuimarisha utekelezaji wa mashauri yanayohusu madai, Katiba na Haki za Binadamu katika Mikoa na Wilaya. Tayari utekelezaji umeanza.

Pia, kufungua ofisi mpya kwa mikoa ya Morogoro, Pwani, Manyara na Kigoma, pamoja na uimarishaji ofisi mpya za Kanda ya Musoma, Lindi na Singida, kuunda timu zitakazoendesha na kusimamia mashauri ya uchaguzi kwa wale watakaopinga matokeo ya zoezi la uchaguzi. Vilevile, Ofisi itaboresha mfumo wa ukusanyaji wa takwimu mbalimbali hususan takwimu zinazohusu fedha zinazookolewa kutokana na mashauri ya madai na majadiliano ya mikataba.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/10, shughuli za utafiti na mapitio ya sheria mbalimbali zilifanyika kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria. Mfumo wa huduma ya sheria uliboreshwala kwa kufanya tafiti na mapitio ya sheria na kutoa mapendekezo ya kuhuisha sheria husika. Utafiti wa awali wa mapitio ya sheria zinazosimamia Sekta ya Kilimo umefanyika kwa lengo la kuboresha sheria hizo ili kutekeleza kauli mbiu ya Kilimo Kwanza pamoja na malengo ya MKUKUTA II. Tume inaendelea kuzifanyia mapitio sheria zinazosimamia Sekta ya Mifugo ili kupata ufumbuzi wa kutatua matatizo yaliyopo baina ya wafugaji na wakulima.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria imekamilisha mapitio ya Kanuni za Mahakama ya Rufani za mwaka 1979, hatua iliyowezesha kutungwa kwa Kanuni za Mahakama ya Rufani za mwaka 2009 ambazo zimeanza kutumika rasmi mwezi Februari, 2010. Pia kupitia Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria, Tume inakamilisha Mapitio na Utafiti wa Sheria na Kanuni za Mila na Desturi za upande wa Mama.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea na kutafsiri sheria kutoka lugha ya Kiingereza kuwa katika lugha ya Kiswahili. Jumla ya sheria tano (5) zimetafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kuwa katika lugha ya Kiswahili kwa lengo la kuwarahisishia na kuwapa uelewa watumiaji. Aidha, Tume imekwishesha kwa lugha ya Kiswahili sheria mbalimbali ambazo ziko kwenye hatua ya kuhakikiwa. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16, Toleo la 2002; Sheria ya Taasisi ya Kazi, Sura ya 300; Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Sura ya 366; Sheria ya Magazeti sura ya 229 toleo la 2002; Sheria ya Mikataba sura ya 345 Toleo la 2002; Sheria ya Mapato

yatokanayo na Uhalifu Sura ya 256 Toleo la 2002 na Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi Sura ya 322 Toleo la 2002. Katika mwaka wa fedha 2010/11, Tume imepanga kukamilisha taarifa za miradi mitano kati ya sheria zifuatazo: Sheria za Mila na Desturi Upande wa Mama, Sheria za Kilimo, Sheria za Mifugo, Mfumo wa haki za madai na Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10 Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini umeendelea na mpango wake wa uimarishaji wa utawala bora kwa kuboresha huduma za Usajili, Ufilisi na Udhamini ambapo umeweza kuhakikisha kuwa huduma zinasogezwa kwa wananchi hususani walioko vijijini. Wakala umefanya kampeni za uandikishaji wa vizazi na vifo kwa wananchi katika Wilaya 10 ambazo ni Shinyanga, Kisarawe, Songea, Bukoba, Mbeya, Moshi, Singida, Ilemela, Nyamagana na Morogoro. Aidha, mafunzo ya usajili wa vizazi na vifo katika ngazi ya Wilaya, Tarafa, Kata na Mitaa au Vijiji yalitolewa kwa watumishi 7,911 wa kada mbalimbali. Mafunzo haya yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuongeza ufanisi wa usajili wa vizazi na vifo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Wakala imesogeza huduma ya kutoa shahada za ndoa na leseni kwa viongozi wa dini wanaofungisha ndoa hadi ngazi ya Wilaya badala ya Makao Makuu. Aidha, Wakala umeendelea kuboresha mfumo wa utunzaji wa kumbukumbu kwa kutumia mfumo wa kompyuta katika kutoa vyeti vya kuzaliwa na vifo. Vile vile, katika mwaka wa fedha 2009/10 Wakala imefanikiwa kusajili vizazi 469,274; vifo 47,118, ndoa 17,106, Talaka 85, miunganisho ya wadhamini 277, mirathi 13, watoto wa kuasili 46, vifo 47,118, na wosia 83, pia, Wakala inaendesha shauri la *IPTL* mahakamani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11, Wakala utaendelea kufanya shughuli za usajili wa vizazi na vifo, ndoa na talaka, watoto wa kuasili kwa mtindo wa kampeni katika Wilaya 15 ambazo ni Mbeya vijijini, Kiteto, Ngorongoro, Kinondoni, Temeke, Bunda, Moshi Vijijini, Kilosa, Iringa mjini, Tabora Mjini, Musoma, Dodoma Mjini, Bagamoyo, Masasi na Igunga, ili kuwasogezea huduma wananchi na kuongeza kiwango cha usajili kwa vizazi na kutoa vyeti vyenye alama za usalama ili kudhibiti matukio ya kughushi nyaraka za Serikali. Aidha, wakala itazipitia sheria na taratibu mbalimbali zinazoongoza shughuli zake katika kuboresha huduma kwa wananchi pamoja na kutoa elimu kwa njia mbalimbali katika masuala ya usajili, mirathi, wosia na udhamini.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ina jukumu la kutoa ushauri wa kisheria katika mchakato wa majadiliano na mapitio ya mikataba mbalimbali inayosainiwa na Serikali. Ili kuongeza ufanisi katika mchakato wa kupata mikataba yenye maslahi kwa Taifa letu, Serikali kwa uhisani wa Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) inatekeleza mradi wa kuwajengea uwezo wataalam katika nyanja za kujadili, kuandika na kuhakiki Mikataba.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2009/2010, kazi zilizofanyika kupitia mradi huu ziliwu ni kutoa mafunzo kwa wataalam kuhusu mbinu na vigezo vya Kimataifa, mafunzo ya mbinu na stadi zenyi viwango vya Kimataifa katika kujadili viwango vya kodi katika mikataba ya uwekezaji inayohusisha maliasili za nchi, kama vile, madini, mafuta na gesi asilia. Wataalam walioshiriki mafunzo haya ya awamu ya nne ni Mawakili kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Wanasheria na Wajiolojia kutoka Wizara ya Nishati na Madini, Wachumi na Wanasheria kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Wizara ya Fedha na Uchumi na Ofisi ya Waziri Mkoo. Kwa kipindi cha miezi saba tu, Warsha nne (4) zimeshafanyika chini ya mradi huo ambapo watumishi husika 85 wa taaluma mbalimbali wamenufaika na mafunzo hayo. Mradi huu wa mafunzo utaendelea katika mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali itaendelea kuungana na timu mbalimbali za Serikali za majadiliano katika kujadili mikataba mbalimbali itakayoihusisha Serikali. Lengo litakuwa ni kuhakikisha kuwa maslahi ya nchi yanalindwa kisheria katika mikataba hiyo. Ni matumaini yangu kwamba utaalam wa kisheria wa Mawakili wa Serikali watakaohusika, utaungana na ule wa Wataalam wengine katika fani zinazohusika na maeneo yatakayojadiliwa. Aidha, Ofisi itahakikisha kwamba Mawakili wa Serikali katika Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali na Mawakili wa Serikali walio katika Wizara na Idara za Serikali wanaendelea kupewa mafunzo ya aina mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kujadili, kuandika na kuhakiki mikataba katika maeneo mbalimbali yakiwemo yale ya madini, gesi asilia, mafuta, kodi, mambo ya fedha na miradi mikubwa ya uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, Wizara imeendelea kuboresha vitengo vya Habari, Elimu na Mawasiliano kwa kuajiri Maafisa Habari ili kuwezesha jukumu la utoaji Habari za Wizara kwa jamii. Aidha, kupitia Programu ya Maboresho ya Sekta ya sheria, Wizara imeanzisha tovuti inayojulikana kwa jina la www.sheria.go.tz kwa lengo la kuboresha utoaji wa taarifa na elimu kwa wananchi. Kwa kuanzia tovuti hii ina taarifa kuhusu Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Hadi mwisho wa mwaka huu wa fedha wa 2009/2010, Wizara itakuwa imerusha vipindi vitano vya luninga na viwili vya redio vitakavyorushwa moja kwa moja kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu masuala ya utoaji wa haki na maboresho yanayoendelea katika sekta ya sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa utoaji wa elimu ya sheria kwa jamii, Tume ya Kurekebisha Sheria ilifanya ziara katika Wilaya ya Mbanga mkoa wa Ruvuma kwa lengo la kuwaelimisha wananchi juu ya sheria mpya ya vinasaba na sheria ya mirathi. Aidha, Tume ilitoa nakala na vipeperushi 15,000 vinavyohusu taarifa mbalimbali za Tume ya Kurekebisha Sheria, pamoja na kuonesha vipindi 60 kwa njia ya radio kwa lengo la kuwaelimisha wananchi.

Mheshimiwa Spika, elimu kuhusu haki za binadamu na utawala bora iliendelea kutolewa kwa kuendesha mafunzo ya utawala bora kwa wenyeviti na makatibu wa Vijiji na Kata katika Wilaya kumi (10) za Tanzania Bara. Njia zilizotumika ni kusambaza fulana, vijitabu vya Tambua Haki na Wajibu Wako na vipeperushi. Aidha, Tume ya Utumishi wa Mahakama katika kuhakikisha inatoa habari pamoja na kupata maoni mbalimbali kutoka kwa wananchi na wadau wengine muhimu, imeandaa mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano. Pia Tume ilishiriki kwenye maonesho ya Nanenane pamoja na kuchapisha na kugawa kwa wananchi vipeperushi elfu nne (4,000) vinavyoceleza mamlaka, majukumu na kazi za Tume.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara yangu inatarajia kuendelea kuboresha utoaji elimu kwa jamii kwa kuanzisha na kuimarisha vitengo vya Habari, Elimu na Mawasiliano katika Taasisi zote za Wizara kwa kuajiri Maafisa Habari zaidi na kukamilisha mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano kwa Taasisi zote za Wizara. Aidha, vipindi 18 vya luninga na vipindi 18 vya redio vitatayarishwa na kurushwa hewani kwa ajili ya kuelimisha jamii juu ya sekta ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Uingereza (*DFID*) iliendelea kutekeleza mradi wa kuijengea uwezo wa kupambana na rushwa kubwa, kwa kuzijengea uwezo wa kitaaluma na vifaa vya taasisi tano za Kitaifa zinazohusika na mapambano dhidi ya rushwa (*Tackling Corruption Project – TCP*). Taasisi hizo ni Divisheni ya Mashtaka, TAKUKURU, Sekretariati ya Maadili ya Viongozi, Mamlaka ya kudhibiti Manunuvi katika Sekta ya Umma (*PPRA*) na Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (*FIU*). Chini ya mradi huu, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepatiwa vitendea kazi mbalimbali kama vile magari manane (8), Kompyuta (44), Kompyuta mpakato (*Laptop*) nane, vitabu na sheria mbalimbali pamoja na kufanya mafunzo ya namna ya kuendesha mashauri ya rushwa.

Katika mwaka wa fedha 2010/2011, mradi huu utaendesha mafunzo ya utambuzi wa mianya ya rushwa nchini kwa Mawakili mia moja, kuitisha mikutano ya ushauri wa vyombo vinavyohusiana na upeletezi wa mashauri ya rushwa, kutoa ushauri wa kisheria kuhusu mwenendo wa mashauri ya rushwa pamoja na kununua vitendea kazi kwa ajili ya matumizi ya ofisi.

Mheshimiwa Spika, sambamba na utekelezaji wa mpango wa kutenganisha shughuli za mashtaka na upeletezi kwa mara ya kwanza, Divisheni ya Mashtaka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliwezesha uanzishwaji wa Jukwaa la Taifa la Haki Jinai nchini (*The National Criminal Justice Forum–NCJF*) ambalo uzinduzi wake ulifanyika mwezi Desemba, 2009. Lengo la kuwa na jukwaa hili ni kuwa na mfumo madhubuti wa utendaji kwa vyombo vyote vinavyoshirikiana katika usimamizi wa utoaji haki jinai. Mwaka 2009/2010, Kikao kimoja cha kujadili changamoto zilizopo katika utoaji wa haki kimefanyika. Aidha, baada ya kuzinduliwa kwa jukwaa hili, kamati maalum zinazojumuisha baadhi ya wajumbe wa Jukwaa zimefanya vikao vitatu kujadili na kutafuta ufumbuzi wa changamoto kadhaa zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inasimamia Vyuo viwili vya Mafunzo vinavyohusika na Sekta ya Sheria. Vyuo hivyo ni Chuo cha Uongozi wa

Mahakama-Lushoto (*Institute of Judicial Administration*) na Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania (*The Law School of Tanzania*). Katika mwaka wa fedha 2009/10, Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Lushoto kimeendelea na jukumu lake la kutoa Mafunzo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Makarani wa Mahakama.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2009/10 Chuo kimefanikiwa kupanua jengo la maktaba ya muda pamoja na kukarabati nyumba mbili za kukaa wahadhiri. Ujenzi wa jengo la hosteli ya wanachuo wa kike lenye ghorofa tatu unaendelea. Jengo hili likikamilika litaongeza uwezo wa kuingiza wanachuo wasiopungua 278 na hivyo kuongeza idadi ya wanachuo. Katika mwaka wa fedha 2010/11, Chuo kimepanga kuanza ujenzi wa hosteli nyingine kwa ajili ya wanachuo wanaume, kukarabati nyumba ya Mkuu wa Chuo na kukarabati nyumba mbili za wahadhiri.

Pia Chuo kitadahili wanachuo wapya 450 na hivyo kuongeza idadi ya wanachuo kutoka 628 waliopo na kufikia wanachuo 650. Matarajio ya muda mrefu ni kukitumia Chuo hiki kuwapatia watumishi wa Mahakama, hususan Majaji, Mahakimu na Watumishi wengine wa Mahakama mafunzo ya muda mfupi ya mambo mapya katika masuala ya Sekta ya sheria ili waende sambamba na mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2009/10, Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania ilidahili wanafunzi 346 na hivyo kufikisha idadi ya wanafunzi 1,446 ambao wamepata udahili katika Taasisi hiyo tangu mafunzo hayo yalipoanza rasmi Machi 2008. Taasisi ilihuisha na kuboresha mtaala wake wa mafunzo kwa vitendo na kuzifanyia marekebisho mbalimbali Kanuni na Taratibu za Kuendesha Mafunzo na Mitihani ili ziweze kukidhi mahitaji mbalimbali ya wanafunzi na Sekta ya Sheria kwa ujumla. Ili kujenga uwezo wa Taasisi katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi imeajiri watumishi wapya kumi na moja (11) na kununua samani na vitendea kazi vingine.

Pia, Taasisi imenunua vitabu mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi na wahadhiri. Kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Msaada (*International Lawyers Project*) ya London, Uingereza, Taasisi imeanzisha programu maalum ya kuboresha utoaji na undeshaji wa mafunzo yake.

Chini ya programu hiyo, Mawakili na wataalam wengine thelathini na watano (35) kutoka Uingereza walishirikiana na wahadhiri wa Taasisi hiyo kutoa mafunzo mahsus i kwa wanafunzi 190 wa Taasisi hiyo kwa kiwango kikubwa cha mafanikio. Mafunzo hayo yalihusu Mbinu za Uwakili, Uendeshaji wa Mashauri ya Madai, Maadili na Taratibu za Uwakili na Uandishi wa Mikataba ya Kimataifa. Sambamba na mafunzo hayo, vitini (*training manuals*) vitano kwa ajili ya mafunzo viliandaliwa na kutolewa kwa wanafunzi.

Taasisi ilipata Mshauri Mwelekezi ambaye amekwishatayarisha michoro ya majengo yake ili kuwezesha kuanza ujenzi katika kiwanja cha Taasisi cha ekari 23

kilichoko eneo la Barabara ya Sam Nujoma, jijini Dar es Salaam. Tayari idhini ya Benki ya Dunia imekwishapatikana na Zabuni ya Ukandarasi wa Ujenzi imekwishatangazwa.

Katika mwaka wa fedha 2010/11, Taasisi inatarajia kudahili wanafunzi 850, kununuu juzuu mbalimbali za vitabu vya sheria, kutayarisha vitini vipyta sita, kuajiri watumishi wengine na kusimamia ujenzi wa majengo yake. Ni matumaini ya Wizara yangu kuwa ujenzi utaanza Robo ya Pili ya mwaka ujao wa fedha (baada ya taratibu za zabuni kumalizika) na kukamilika ndani ya miezi kumi na tano (15).

Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya Watumishi. Katika mwaka 2009/10, Wizara yangu iliendelea na jukumu lake la kuendeleza na kuwahudumia watumishi wake kijamii na kitaaluma. Aidha, jumla ya watumishi 543 walajiriwa katika nafasi za Mahakimu, Mawakili, Wachunguzi na Kada, nyingine. Aidha, masuala ya kuthibitishwa kazini na kupandishwa cheo kwa ngazi mbalimbali za watumishi yalishughulikiwa. Jumla ya Watumishi 237 walipandishwa vyeo na watumishi 191 walithibitishwa kazini na katika vyeo vyao. Mafunzo ya muda mrefu na mfupi yalitolewa kwa watumishi 595 yalisaidia kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara katika utoaji huduma kwa ufanisi na tija.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2009/10, Tume ya Utumishi wa Mahakama, ilishughulikia malalamiko manane (8) yaliyowasilishwa na wananchi dhidi ya Mahakama na Majaji kati ya malalamiko 11 yaliyopokelewa. Aidha, Tume iliratibu Mafunzo ya kuwajengea uwezo Makatibu wa Kamati za Maadili za Mahakama 22 kutoka katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Ruvuma na Rukwa pamoja na Wilaya zake kuhusu namna ya kushughulikia malalamiko yanayowasilishwa kwenye Kamati ya nidhamu dhidi ya Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2010/11 Wizara inakusudia kuajiri watumishi 565 wa kada ya Uwakili, Uhakimu na kada nyingine. Aidha, jumla ya watumishi 754 watapandishwa cheo, na 219 kuthibitishwa kazini.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na masuala mtambuka kama vile Rushwa, Jinsia na UKIMWI. Wizara yangu iliendelea kuchukua hatua katika kuboresha huduma zitolewazo kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI, Wizara imerejea mpango Mkakati wake na kuingiza majukumu hayo katika mahitaji ya fedha zinazohitajika ambazo tayari zimezingatiwa katika mpango na bajeti ya 2010/11. Fedha hizi zitatumika katika kununulia virutubisho. Aidha, juhudi za kuwaelimisha watumishi juu ya madhara ya rushwa na maadili zinaendelea. Kamati za Uadilifu zimeanzishwa na kuendelea na juhudi za kufanya uchunguzi na ufuutiliaji pamoja na kuchukuliwa hatua zinazostahili kwa watumishi dhidi ya tuhuma za rushwa.

Mheshimiwa Spika, uzingatiaji wa masuala ya jinsia ni suala linalopewa kipaumbele katika maboresho ya sekta ya sheria. Katika mwaka wa fedha 2010/2011, Wizara yangu kupitia Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria imelenga kufanya tathimini ya hali halisi ya masuala ya jinsia katika taasisi zilizo chini ya Sekta ya Sheria ili kuwa na mkakati wa utekelezaji wa shughuli za jinsia; kutoa mafunzo kwa viongozi waandamizi wa taasisi zinazotekeleza programu ili kuwawezesha kufanya maamuzi yanayozingatia takwimu sahihi za kijinsia katika maeneo yao; kuhakikisha kuwa taasisi zilizo katika Programu ya Maboresho ya Sekta ya Sheria zinazingatia upatikanaji na utumiaji wa takwimu zilizoainishwa katika mtazamo wa kijinsia kwenye utekelezaji wa majukumu ya Taasisi; kuwawezesha dawati la Jinsia katika Vituo vya Polisi litakalojihusisha na kusikiliza na kushughulikia malalamiko yanayotoka katika kundi la wanawake na watoto na hasa kuhusu unyanyasaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

(Hapa Kengele Ililia)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, shukrani. Kwa niaba ya Wizara yangu, nawashukuru kwa dhati wale wote walioshirikiana nasi katika kipindi cha 2009/10 katika kutimiza malengo yetu. Shukrani zetu pia ziwaendee wabia wa maendeleo wanaoshirikiana nasi katika kuiendeleza Sekta ya Sheria nchini. Wahisani hao wanajumuisha mashirika na taasisi za kimataifa zinazochangia katika kuboresha utoaji wa haki sawa kwa wote na kwa wakati. Nchi na mashirika hayo ni pamoja na Denmark (*DANIDA*), Canada (*CIDA*), Uingereza (*DFID*), Benki ya Dunia (*WB*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Watoto (*UNICEF*) na Shirika na Umoja wa Mataifa la Maendeleo (*UNDP*).

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru wananchi na wadau mbalimbali hasa sekta binafsi, wanahabari, Vyuo vya Elimu vinavyohusika na mambo ya Sheria kwa ushirikiano wao katika kutekeleza malengo ya Sekta ya Sheria. Shukrani za pekee ziwaendee Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa michango yao ambayo imechangia katika kuboresha huduma zitolewazo na Wizara. Naomba waendelee na ushirikiano huo ili tuweze kuendeleza Sekta hii muhimu katika utoaji haki kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru wafanyakazi wenzangu wa Wizara ya Katiba na Sheria, nikianza na Mheshimiwa Jaji Mkuu, Augustino Ramadhan; Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema; Mheshimiwa Fakihi A.R. Jundu, Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu; Bwana Oliver P.J.Mhaiki, Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria; Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Bwana George Masaju; Msajili wa Mahakama ya Rufaa, Bwana Francis Mutungi; Mkurugenzi wa Mashtaka, Bwana Eliezer M. Feleshi; aliyekuwa Msajili wa Mahakama Kuu, Mheshimiwa Jaji John Utamwa na aliyekuwa Msajili wa Mahakama Kuu Divisheni ya Kazi, Mhe. Jaji Samuel G. Karua.

Mheshimiwa Spika, wengine ni aliyekuwa Msajili wa Mahakama Kuu Divisheni ya Ardhi; Mheshimiwa Jaji Grace Mwakipesile; Msajili wa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara, Bwana John Kahyoza; Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Bibi Celina Wambura; Katibu Mtendaji wa Tume ya kurekebisha Sheria Bwana Japhet Sagasii; Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Bibi Mary Massay; Kaimu Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Usajili na Ufilisi na Udhaminii, Bwana Philipo Saliboko na Kaimu Mkuu wa Taasisi ya Uanasheria kwa Vitendo Tanzania Dr. Gerald Ndika.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru kipekee wataalam na watumishi wa Wizara yangu kwa mchango wao katika kukamilisha Hotuba yangu pamoja na ushirikiano mzuri wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba niwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Nachingwea kwa ushirikia mkubwa walionionesha kipindi chote ambacho nimekuwa nao katika shughuli zote za maendeleo katika Jimbo letu. Pamoja tumefanya mengi sana na wanaotubeza ni wale wenye wivu tu na Mwenyezi Mungu ametupa vipaji vingi na wapo wale amba wana macho lakini hawataki kuona. Aidha, niishukuru sana familia yangu, mke wangu Amandina na watoto kwa kunitia moyo kwa kunipa ushauri mzuri katika kutekeleza majukumu yangu na hasa kwa uvumilivu wao hasa nyakati ambazo sikuweza kuwa nao nyumbani kutokana na majukumu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha, kwa mwaka 2010/2011. Ili Wizara iweze kutekeleza malengo yake yaliyoainishwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2010/11, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi bilioni mia moja kumi na sita, milioni mia nane sabini na moja, sita elfu, (116,871,006,000) kwa ajili ya matumizi ya Wizara kwa mwaka 2010/2011. Kati ya fedha hizi, matumizi ya kawaida ni Shilingi bilioni sabini na sita, milioni mia nane hamsini na tatu mia mbili sabini na moja elfu, (76,853,271,000).

Fedha za miradi ya Maendeleo ni Shilingi bilioni arobaini, milioni sabini na moja, mia saba, thelathini na tano elfu (40,071,735,000). Kati ya hizi, Shilingi bilioni saba, milioni mia mbili na mbili, mia mbili tisini na moja elfu (7,202,291,000) ni fedha za ndani na Shilingi bilioni thelathini na mbili, milioni mia nane kumi na tano, mia nne arobaini na nne elfu (32,815,444,000) ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio hayo ya Fedha za Maendeleo na Matumizi ya kawaida kwa mafungu kumi na mbili kama ifuatavyo:-

Fungu 12: Tume ya Utumishi wa Mahakama

| | |
|-------------------------------|-------------|
| Matumizi ya Kawaida | 977,101,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | - |

| | |
|-----------------------------|--------------------|
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | - |
| JUMLA | 977,101,000 |

Fungu 16: Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

| | |
|-------------------------------|----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | 9,478,842,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | - |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | 420,000,000 |
| JUMLA | 9,898,842,000 |

Fungu 18: Mahakama Kuu

| | |
|-------------------------------|-----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | 17,244,324,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | - |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | - |
| JUMLA | 17,244,324,000 |

Fungu 19: Mahakama za Wilaya

| | |
|-------------------------------|-----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | 18,320,185,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | - |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | - |
| JUMLA | 18,320,185,000 |

Fungu 35: Divisheni ya Mashtaka

| | |
|-------------------------------|----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | 6,688,958,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | - |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | 1,500,000,000 |
| JUMLA | 8,188,958,000 |

Fungu 40: Mahakama

| | |
|-------------------------------|-----------------------|
| Matumizi ya kawaida | 9,937,579,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | 6,113,584,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | 22,061,970,000 |
| JUMLA | 38,113,133,000 |

Fungu 41: Wizara ya Katiba na Sheria

| | |
|-------------------------------|-----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | 5,732,058,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | 996,435,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | 4,000,000,000 |
| JUMLA | 10,728,493,000 |

Fungu 55: Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora

| | |
|-------------------------------|----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | 3,660,452,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | - |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | 1,126,215,000 |
| JUMLA | 4,786,667,000 |

Fungu 59: Tume ya Kurekebisha Sheria

| | |
|-------------------------------|----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | 1,335,218,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | - |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | 877,500,000 |
| JUMLA | 2,212,718,000 |

Fungu 60: Mahakama ya Kazi

| | |
|-------------------------------|----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | 1,277,601,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | - |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | 1,824,356,000 |
| JUMLA | 3,101,957,000 |

Fungu 64: Mahakama ya Biashara

| | |
|-------------------------------|----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | 1,117,468,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | 92,272,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | 470,187,000 |
| JUMLA | 1,679,927,000 |

Fungu 90: Mahakama ya Ardhi

| | |
|-------------------------------|----------------------|
| Matumizi ya Kawaida | 1,083,485,000 |
| Matumizi ya Maendeleo (ndani) | - |
| Matumizi ya Maendeleo (nje) | 535,216,000 |
| JUMLA | 1,618,701,000 |

Mheshimwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2010/11, Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni mbili, milioni mia moja thelathini na tisa, (2,139,000,000) kama Maduhuli ya Serikali. Mchanganuo wa Makusanyo kwa kila fungu husika ni kama ifuatavyo:-

| | |
|--------------|-----------------|
| Fungu 16 ... | Sh. 31,400,000 |
| Fungu 18 ... | Sh. 277,100,000 |
| Fungu 19 ... | Sh. 801,800,000 |

| | |
|--------------|--------------------------|
| Fungu 40 | Sh. 129,600,000 |
| Fungu 41 | Sh. 2,900,000 |
| Fungu 55 | Sh. 4,600,000 |
| Fungu 59 | Sh. - |
| Fungu 64 | Sh. 824,900,000 |
| Fungu 90 | Sh. 66,700,000 |
| JUMLA | Sh. 2,139,000,000 |

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja Ilitolewa iamuliwe*)

MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, Kanuni ya 99(7) na Kanuni ya 114(11), naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya katiba, Sheria na Utawala ilikutana tarehe 01/06/2010, kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Kuchambua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2010/2011. Katika Taarifa hiyo Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Waziri wa Katiba na Sheria alieleza Kamati kuhusu Muundo wa Wizara hii ili kubainisha upekee uliopo Kimuundo pamoja na kuonyesha Taasisi zenyenye Mafungu 12 ya Bajeti. Taasisi hizo na Mafungu yake ni kama ifuatavyo:-

- (i) Tume ya Utumishi wa Mahakama, Fungu 12
- (ii) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,Fungu 16
- (iii) Mahakama Kuu, Fungu 18
- (iv) Mahakama za Wilaya,Fungu 19
- (v) Mkurugenzi wa Mashitaka, Fungu 35
- (vi) Mahakama, Fungu 40
- (vii) Wizara ya Katiba na Sheria, Fungu 31

- (viii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Fungu 55
- (ix) Tume ya Kurekebisha Sheria, Fungu 59
- (x) Mahakama ya Kazi, Fungu 60
- (xi) Mahakama ya Biashara, Fungu 64
- (xii) Mahakama ya Ardhi, Fungu 90

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingine zilizotajwa kuwa chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ni pamoa na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*), Taasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo (*Law School of Tanzania*) na Chuo cha Uongozi wa Mahakama (*Institute of Judicial Administration*). Pamoja na maelezo hayo Kamati pia ilielezwa kuhusu majukumu, Dira na Dhima ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2009/2010. Kamati ilielezwa kuwa Wizara ilitekeleza Muundo mpya ili kuongeza ufanisi. Katika Taarifa ya Mheshimiwa Waziri tulielezwa jinsi Wizara na Taasisi zake zilivyotekeliza majukumu na malengo yaliyowekwa kwa Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo ya kina na ufanuzi wa hoja mbalimbali zilizojitokeza, Kamati iliridhika na Utendaji wa Wizara ikilinganishwa na malengo yaliyokuwa yamewekwa kwa Mwaka wa Fedha 2009/2010, kwa Taasisi zote na Mafungu husika. Pamoja na hivyo, Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria alibainisha changamoto mbalimbali zilizopatikana wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, napenda kueleza kuwa changamoto hizo zilibainika wakati Kamati ilipofanya ziara ya kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Maeneo tuliyotembelea ni:-

- (i) Mahakama za Wilaya tano Mkao wa Pwani.
- (ii) Kurugenzi ya Uendeshaji Mashitaka.
- (iii) Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkao wa Morogoro.
- (iv) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora.
- (v) Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Spika, katika ziara hizo Kamati ilibaini kuwepo kwa changamoto mbalimbali zinazoweza kuathiri utekelezaji wa azma ya Serikali ya kujenga mazingira ya utoaji haki sawa kwa wote na kwa wakati pamoja na kujenga, kukuza dhana ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2009/2010, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa kuzingatia mipango iliyokuwepo, hali ilivyo na fedha zilizoombwu kuidhinishwa. Maeneo yaliyotolewa ushauri ni pamoja na yafuatayo:-

- (i) Mbinu ya kuiongezea fedha Mahakama.
- (ii) Uanzishwaji Mfuko Mahakama (*Judiciary Fund*).
- (iii) Kuongeza wigo wa ajira na kuajiri Mahakimu zaidi na kuteua Majaji.
- (iv) Kuongeza bajeti kwa ajili ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.
- (v) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kutafsiri Sheria na Kutoa machapisho zaidi.

Mheshimiwa Spika, mpango malengo na makadirio ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011. Kkabla ya Mheshimiwa Waziri kueleza Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2010/2011, alieleza Kamati kuhusu malengo na majumu yanayopangwa kutekelezwa kwa Mwaka 2010/2011. Maelezo hayo yalihusu Mipango ya Taasisi na Idara zote chini ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa ujumla Kamati iliafiki malengo, mipango na majukumu ya Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi, kama ambavyo wengi tunafahamu baada ya uchambuzi wa kina yapo masuala yaliyojitekeza katika kikao cha Kamati cha tarehe 5 Juni, 2010. Kutokana na hivyo, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala ilikutana tena tarehe 15 Juni, 2010 ili kuendelea kushughulikia Bajeti hii. Tunaishukuru na kuipongeza Serikali kwa usikivu na umakini mkubwa katika kushughulikia masuala yaliyoibuliwa na Kamati na kuyatolea maelezo yanayoonyesha kuwa masuala yaliyoibuliwa na wajumbe yatazingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia Taarifa ya Utekelezaji wa majukumu ya Wizara na kupitia kifungu kwa kifungu, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu

yote chini ya Wizara hii na kuyapitisha ili yawasilishwe Bungeni kwa hatua zinazofuata pamoja na kuzingatia ushauri wa Kamati hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maoni na ushauri. Ili kusimamia vyema utoaji haki nchini na kuhakikisha kuwa Sheria na taratibu za nchi zinafuatwa, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iandae mkakati maalum wa ukarabati wa majengo chakavu ya Mahakama za Wilaya na Mwanzo nchini;

(ii) Mpango maalum wa ujenzi wa nyumba za watumishi wa Mahakama nchini uandaliwe sanjari na ujenzi wa Mahakama katika maeneo ambayo hakuna majengo ya Mahakama;

(iii) Serikali ianzishe Mahakama maalumu kwa ajili ya mashauri yanayohusu rushwa ili kuboresha utoaji haki kwa wakati katika masuala yanayohusu Rushwa;

(iv) Chuo cha Uongozi wa Mahakama Lushoto (*Institute of Judicial Administration*) kiongeze idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa ili pamoja na kutoa wanasheria, Serikali iweze kuongeza idadi ya Mahakimu hususan katika Mahakama za Mwanzo;

(v) Kuhusu usawa wa maslahi baina ya Wanasheria wa Serikali na wale waliopo Tume ya kurekebisha Sheria na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ni vyema tofauti iliyopo ifanyiwe kazi kwa kuzingatia sifa walizonazo wataalam hao;

(vi) Kama ilivyo kwa Mfuko wa Bunge na ule wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu Hesabu (CAG), Serikali iamue kuanzisha Mfuko wa Mahakama;

(vii) Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iwezeshwe zaidi Kibajeti ili iweze kuendelea na ufanisi katika Utekelezaji wa majukumu yake;

(viii) Kasi ya kushughulikia malalamiko kuhusu uvunjaji wa Haki za Binadamu na misingi ya Utawala Bora iongezwe;

(ix) Ili kuiwezesha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kuwa na watumishi wenyewe uzoefu, utaratibu unaotumika kuwahamisha watumishi kutoka Tume hii uangaliwe vizuri; na

(x) Sheria iliyoanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iangaliwe upya na kuitaka Tume hii kuwajibika kuwasilisha mezani taarifa zake na kujadiliwa. Mabadiliko haya yatasaidia kuongeza tija katika juhudzi za kusimamia misingi ya Utawala Bora na udhibiti wa ukiukwaji wa Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Pia, nawashukuru Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, Mb, Waziri wa Katiba na Sheria na Mhehimiwa Jaji Frederick Werema, Mb, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushirikiano mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Vile vile, nawashukuru Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya Kujadili na Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka 2010/2011. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu Sekta za Utawala, Uendeshaji, Haki za Binadamu na Utawala Bora, umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti na Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, Makamu Mwenyekiti. (Makofi)

Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Salim Yussuf Mohamed, Mheshimiwa Kingunge Ngombale-Mwiru, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Stephen J. Galinoma, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Nimrod E. Mkono, Mheshimiwa Rajab Hamad Juma, Mheshimiwa John Paulo Lwanji, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbiri, Mheshimiwa Yusuf Rajabu Makamba na Mheshimiwa Abbas Zuberi Mtemvu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa shukrani za dhati kwa Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashilillah, kwa kuratibu vyema shughuli za Vikao vya Kamati. Kipekee nawashukuru Makatibu wa Kamati hii Ndugu Athuman Hussein na Elihaika Mtui, chini ya Uongozi wa Ndugu Charles Mloka, Mkurugenzi wa Kamati za Bunge kwa juhudzi zao katika kuratibu masuala ya Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na

Taasisi zake, Jumla ya Shilingi 116,871,006,000/=. Kati ya hizo Shilingi 76,853,271,000/= zinaombwa kwa ajili ya matumizi ya Kawaida kwa Mafungu yote na Shilingi 40,071,735,000/= ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo kama alivyowasilisha Mto hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofî*)

SPIKA: Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuwasilisha kwa ufanisi kabisa taarifa ya Kamati yako. Kama ilivyo kawaida ya Kanuni, sasa ni zamu ya Msemaji Mkuu wa Upinzani kuhusu masuala ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Fatma Maghimbî.

MHE. FATUMA M. MAGHIMBI MSEMAMI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingu wa rehema, kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kufika katika kikao hiki cha mwisho cha Bunge la Tisa tokea nchi yetu ilipopata Uhuru mwaka 1961.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, napenda kutoa maoni kuhusu bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 99 (7), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kukushukuru wewe binafsi pamoa na Naibu Spika, kwa kazi nzuri mliyoifanya katika uhai wa Bunge hili. Kwa umuhimu mkubwa sana, napenda kumshukuru mume wangu, Bwana Mussa Maghimbî, kwa upendo na uvumilivu mkubwa alionao wakati ninapokuwa katika shughuli za siasa.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wenzangu wa Kambi ya Upinzani, wakiongozwa na Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed (Mb) na Naibu Kiongozi Mheshimiwa Dkt. Slaa (Mb), kwa msaada mkubwa walionipa katika kipindi chote cha miaka mitano tunayoelekewa kumaliza sasa kama Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpe pongezi zangu Mwenyekiti wangu wa Kamati ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa George Malima Lubeleje, kwa jinsi anavyoendesha Kamati yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu wa kipekee, ni kwa Mheshimiwa Mathias Chikawe (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria na Mheshimiwa Frederick Werema (Mb), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kwa ushirikiano wao ambao wamekuwa wakinipatia nikiwa Waziri Kivuli wa Sheria na Katiba katika kipindi chote walichokuwa katika ofisi zao.

Mheshimiwa Spika, katika matayarisho ya hotuba hii, tafiti zimefanyika sehemu mbalimbali zilizoko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria. Pia nimeangalia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ili kuona Ilani hiyo imetekelezwa kiasi gani kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita kwa Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza uchambuzi wetu, naomba nitoe lalamiko langu kuhusu mpangilio wa vifungu katika Katiba yetu ya *version* ya Kiingereza. Mpigachapa amechanganya mno kurasa na hivyo kumfanya msomaji kushindwa kufuatalia. Tukumbuke kuwa wageni wanasoma *version* hii ya Katiba. Ninaomba kuwepo umakini wa kukagua kifungu kwa kifungu kabla ya kusambazwa. Hili limenikera sana na linatuaibisha sana kama nchi machoni pa wageni.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Lengo la kuanzisha Tume hii, ni kuona haki za wananchi zinalindwa na pia kuhakikisha hazivunjwi ili kila mwananchi aone kuwa haki hizo ziko ndani ya mikono safi. Japokuwa Tume hii imeundwa kisheria na inafanya kazi zake ili kuisaidia Serikali kutimiza wajibu wake kwa wananchi, cha ajabu Tume hii badala ya kupewa ushirikiano na viongozi wa Serikali, Tume inaonekana ni adui hasa na Wizara ya Katiba na Sheria. Hii ni kwa sababu uamuzi na mapendekezo ya Tume hii hayatiliwi maanani na hudharauliwa. Kwa mfano, kesi ya Nyamuma na ile ya Loliondo na vile vile mapendekezo mengi yanayotolewa na taarifa zake za kila mwaka kuhusu Serikali kutokuheshimu haki za raia.

Mheshimiwa Spika, Tume hii imetumia fedha nyangi pamoja na nguvu nyangi za wafanyakazi wa Tume. Mategemeo ni kuwa Serikali kwa kuititia Wizara ya Katiba na Sheria ithamini kazi yao. Lakini Serikali inaonyesha wazi kudharau juhudhi za wachapa kazi hao. Imekuwa ni kama vile Serikali ya CCM iliunda Tume hii kuwahadaa Watanzania na Jumuiya ya Kimataifa tu kwamba Tanzania inachukua hatua muhimu ya kuunda taasisi za kulinda na kutetea haki za binadamu na utawala ilhali ikiwa haina nia wala dhamira ya dhati ya kufanyia kazi mapendekezo yake au hukumu zake. Kambi ya Upinzani inasema hii ni kasoro kubwa kwa nchi inayotangaza kuwa inafuata na kuongozwa na misingi ya utawala bora na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uundwaji wa Tume ilifanyiwa marekebisho kuititia *Miscellaneous Amendments* (No. 19) iliyosema, na naomba kunukuu:

“The Act is amended in Sec. 33 by deleting the closing words of sub-section (1) and substituting for them the phrase “and the Minister shall cause the report to be laid before the National Assembly”.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kuona maneno hayo yalitolewa ili Ripoti za Tume zisiletwe na kujadiliwa Bungeni. Haileleweki ni kwa nini AG aliagiza maamuzi ya Tume yasitekelezwe. Ikumbukwe wana-Tume ni Wanasheria hivyo basi hawawezi kutoa maamuzi yasiyozingatia misingi ya haki na sheria. Kwa maneno mengine hawawezi kutoa maamuzi ya *ki-layman*.

Mheshimiwa Spika, Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali huwa inaletwa na kuwasilishwa Mezani kwa Spika na baada ya hapo utaratibu wa kikanuni unaendelea. Je, Wizara ya Katiba na Sheria kwa nini haileti Ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ndani ya Bunge?

Mheshimiwa Spika, inaonyesha kama vile Serikali haioni umuhimu wa haki za binadamu. *Draft Bill of Rights for the East African Community*, ukurasa wa 2, unasema hivi nanukuu:-

“States cannot arbitrarily ignore them [the rights] or purport to take them away. If they do so, the act constitutes a violation of Rights and Fundamental Freedom.”

Mheshimiwa Spika, sisi ni wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki ambayo baadaye itakuwa Shirikisho. Hivyo ndivyo inavyosema *draft* hiyo. Je, ikipita hatuoni kuwa sisi tutakuwa hatutekelezi ipasavyo matakwa ya sheria hiyo? Tume inafanya kazi lakini Serikali haitaki kutekeleza maamuzi ya Tume, kama yale ya Loliondo na Nyamuma, itakuwaje iwapo Tume itachukua hatua inayotajwa kwenye Katiba ya nchi, Ibara ya 130 (1) (e), inaongelea juu ya uwezo wa Tume wa kufungua kesi Mahakamani?

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria. Tume hii ilianza kwa nia ya kuangalia Sheria zisizofaa au Sheria kandamizi na pia kupendekeza sheria zinazofaa.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya Ripoti za Tume hazifanyiwi kazi kama Tume yenyewe inavyofanya kazi. Ziko ripoti za miaka mingi, kwa mfano Sheria ya Mwaka 1986 iitwayo *“Delay of Disposal of Civil Suit”*. Kesi hizi zinachelewa sana na hata zile zilizomalizika basi kukaza hukumu inachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, Tume ilipendekeza pia kuanzishwa kwa Mahakama Maalum (*Specialized Courts*) mfano Mahakama za Biashara, Ardhi na Kazi. Serikali inaelewa umuhimu wa Mahakama hizi lakini hadi leo hii ziko katika Mikoa mitatu (3) tu. Pamoja na kuwa wafadhili wanasaidia sana, Serikali haioni umuhimu wa mapendekezo ya Tume hii ya Kurekebisha Sheria. Hii ni kuwakatisha tamaa Watendaji wa Tume.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine muhimu ni kuwa Tume ilipendekeza kuanzishwa kwa Mahakama ya Kesi za Familia. Kambi ya Upinzani inasema laiti kama kungekuwa na Mahakama za Familia basi msongamano wa kesi katika Mahakama za Wilaya na Mikoa ungepungua ama kumalizika kabisa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *BEST (Business Environment Strengthening For Tanzania)*. Katika shughuli za Mradi huu, kuna kipengele cha kuufanya maboresho Mfumo wa Kesi za Madai (*Civil Justice System*). Lengo ni kuwa kesi za madai ziende haraka na hukumu kutolewa badala ya usumbufu uliopo sasa kwani kesi zinachukua hadi miaka kumi (10) na wengine wanakata tamaa na kesi hizo. Laiti Ripoti ya Tume ya 1986 ingefanyiwa kazi basi sasa hivi kusingekuwa na haja ya kufanya Mapitio katika Mradi huu wa *BEST*.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani imetoa angalizo hili kuonyesha ukweli uliopo kuwa Serikali inashindwa kufanya kazi mapendekezo ya Taasisi zake yenyewe na hivyo kusababisha Taifa kuingia gharama kubwa (rasilimali watu na fedha), kwani mapendekezo ya taasisi zake yanatumia muda, fedha na nguvu kazi ambayo baadaye

haifanyiwi kazi. Mwisho wa siku, kazi yote inawekwa kwenye makabati bila kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kwa vigezo hivyo peke yake, watendaji makini katika Serikali makini walitakiwa wajiuzulu au wasiombe tena ridhaa ya wananchi ili kuwatumikia kwani wameshindwa kazi tayari.

Mheshimiwa Spika, *Report on Succession And Inheritance*. Moja katika sheria nzito ni hii ya “*Succession and Inheritance*” kwa sababu inagusa mambo nyeti sana. Lakini Serikali haijaitilia maanani Ripoti hiyo. Tume inapata changamoto nyingi na kupoteza pesa nyingi katika ufanisi wake wa kazi. Pia Tume imeandaa Ripoti takribani 20 lakini mchakato wa kutekeleza mapendekezo ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nyingi na nzito zinazoikabili Tume hii, bado maslani ya wataalamu wa Tume hii ni madogo sana. Bajeti yao ni ndogo ukilinganisha na kazi wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, Wanasheria wengi walioko chini ya Wizara ya Katiba na Sheria, wameboreshewa maslahi yao kama vile Mahakimu na Mawakili wa Serikali (*State Attorneys*), lakini Wanasheria walioko chini ya Tume na vitengo vingine vilivyo chini ya Wizara wamesahauliwa.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaikumbusha Serikali kuwa Wanasheria wengi walioko kwenye Tume na wakala zilizo chini ya Wizara hii wana uzoefu sana na kuwapoteza itakuwa ni hasara kubwa kwa Taifa. Wanaweza pia wakafika mahali wakakata tamaa na hivyo kukosa ari ya kuwajibika kama wanavyofanya sasa. Tukumbuke ule usemi wa Kiingereza kuwa “*You pretend to pay me, I pretend to work.*”

Mheshimiwa Spika, kuna haja pia ya kutambua kazi inayofanywa na Tume hii, hasa pale Sheria inapokuja hapa Bungeni basi angalau itajwe kwamba Sheria fulani imetokana na Tume hii badala ya kusema ni Mwandishi wa Sheria wa Serikali hata kama Sheria zimeandikwa na Tume. Wahenga walisema Mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Kutambua na kuthamini kazi ya mtu (*recognition*), ni kitu kizuri sana katika utendaji. Kwa mfano, naamini Wabunge wengi hawajui Sheria hizi zifuatazo kuwa zimetokana na Tume hii, Sheria ya Walemavu; Sheria ya DNA; Sheria ya Watoto na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana. Hizi ni chache tu kati ya kazi nyingi walizofanya.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (*RITA*). Wakala huu ulianzishwa kwa lengo la kuboresha huduma za Utumishi kwa Umma kwa sababu huduma hizo zilionyesha kuzorota na vile vile kwa kuipunguzia Serikali gharama za uendeshaji kwa kuwa Wakala ungeweza kukusanya maduhuli ya kujiendesha. Hata hivyo, majukumu yameendelea kuwa yale yale kwa kutumia sheria mbalimbali zinazoongoza shughuli za Wakala. Sheria zinaonyesha waziwazi uhusiano baina ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Ofisi ya *RITA*, kwa mfano, Sheria Na. 4 ya 2005, Kifungu Na. 4(3) cha Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu na Tangazo la Serikali Na. 397 la Desemba 2, 2005 kuhusu uanzishwaji wa *RITA*.

Mheshimiwa Spika, *RITA* na Ofisi ya Mwanasheria Mkoo, zote ni Mamlaka za Ajira, lakini kumekuwepo na mkanganyiko wa kiutendaji ambao unahitaji kufanyiwa kazi ili *RITA* iweze kwenda vizuri kwa niaba ya Mwanasheria Mkoo. Tatizo lenyewe ni kama ifuatavyo, Wanasheria wanaofanya kazi chini ya Wakala, wamegawanyika sehemu mbili, wale waliokuwapo chini ya Kabidhi Wasii Mkoo kabla ya kubadilika kuwa *RITA*. Hawa walajiriwa na Ofisi ya AG na wanaitwa Mawakili wa Serikali yaani *State Attorneys* na wanaendelea kufanya kazi *RITA* kwa vyeo vyao walivytoka navyo ofisi ya AG. Kundi la pili, ni wale walioajiriwa na Wakala baada ya *RITA* kuanzishwa. Hawa nao ni Wanasheria na wanafanya kazi zote za Mawakili wa Serikali yaani *State Attorneys*. Lakini kuna kauli kwamba Wanasheria hao eti ni Maafisa Sheria. Kama hivyo ndivyo basi, Maafisa Sheria, hawana *locus standi* yaani hawana uwezo wa kusimama Mahakamani kuendesha mashauri ya Mirathi, Udhamini wa Serikali na Maswali ya Ufilisi na mengineyo. Kama mambo haya hayatawekwa sawa basi upo uwezekano wa hukumu itakayotolewa Mahakamani kwa kuendeshwa na Maafisa Sheria ikadaiwa kuwa hukumu hiyo ni batili kwa vile Mwanasheria aliyeendesa kesi hiyo sio Mwanasheria bali ni Afisa Sheria tu na hivyo hivyo hana *locus* ya kuendesha kesi hiyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo linasikitisha na kukatisha tamaa ni kwa Mawakili hawa walioko *RITA* na wale walioko ofisi ya AG, ni kuwa wana maslahi tofauti sana. Wote ni Wanasheria wanaofanya kazi moja na pengine wameajiriwa siku moja lakini wale walioko kwa AG wanahesimika zaidi kimaslahi kuliko walioko *RITA*. Kambi ya Upinzani inamtaka Mwanasheria Mkoo aliangalie upya suala hili kwani wote wanafanya kazi za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, *RITA* ni sehemu muhimu ya kupatikana habari za vizazi, vifo na za ndoa. Kambi ya Upinzani inauliza kwa nini basi bajeti ya shughuli ya Vitambulisho vya Taifa inayohusiana na kuimarisha mfumo wa takwimu za vizazi na vifo za Watanzania isipelekwe *RITA* badala ya *NIDA*?

Mheshimiwa Spika, umefika wakati sasa wa Wizara ya Sheria na Katiba kutambua kwamba kumweka Mtendaji Mkoo wa Tume yoyote kukaimu nafasi yake kwa zaidi ya miaka miwili ni kumuathiri kisailokojia. Katika Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria na Katiba, suala hili tulilizungumzia. Mfano, taasisi ambazo ziko chini ya Wizara hii, Watendaji wake wakuu wanakaimu nafasi hizo kwa muda mrefu sasa. Mama Massey wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Dr. Ndika wa *Law School of Tanzania* na Ndg. Philip Saliboko wa Wakala wa Vizazi na Vifo na Ufilisi. Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alitolee kauli suala hili linalowaathiri kisaikolojia watendaji hao.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi. Katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, ukurasa wa 132, imezungumzia ahadi ya kulishughulikia suala la Mahakama ya Kadhi kwa ajili ya waumini wa dini ya Kiislamu hapa nchini. Ilani ya Uchaguzi ya kila Chama kazi yake ni kuwaahidi wananchi kwamba chama hicho kitafanya nini endapo kitaingia madarakani. Sasa Serikali hii inakamilisha miaka yake

mitano ya utekelezaji wa Ilani hiyo lakini hakuna ilichokifanya katika ahadi hii na hivyo ni dhahiri kwamba CCM iliwhahada Waislamu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kukosa Mahakama hii, Waislamu wanapata taabu kuamua mambo yao ya kijamii kama vile Mirathi, Ndoa na Talaka. Kufunga ndoa ya Waislamu huwa inafungwa na Mashekhe lakini endapo ndoa hiyo inahitaji kuvunjika basi ni Mahakama ya Kadhi pekee ndio ina uwezo wa kuvunja ndoa ya Kiislamu. Kwa mantiki hiyo basi, Serikali inawatia Waislamu katika dhambi pale wanapowasababisha Waislamu kuvunja ndoa zao katika Mahakama ambazo sio za Kadhi.

Mheshimiwa Spika, upande wa Mirathi, katika Uislamu huwa kuna Sheria zake za kugawa mali iliyoachwa na Marehemu. Ikumbukwe kwamba nchi ya Tanzania haina dini, lakini Watanzania wana dini zao na kuna haki ya uhuru wa kuabudu.

Mheshimiwa Spika, huenda Serikali ya CCM ina dhana kuwa Waislamu ni wachache hapa nchini. Ukweli ni kwamba Waislamu ni wengi. Lakini hata kama ni wachache basi dhana ya demokrasia inahitaji wawe huru na Serikali iwasaide katika hilo. Zipo nchi ambazo zina Waislamu wachache sana lakini Serikali inasaidia kuwawekea Mahakama ya Kadhi kwa mfano, Uingereza, Uganda, Kenya, Afrika Kusini na nyiningezo ambazo zina Waislamu asilimia 10 tu au chini ya hapo.

Mheshimiwa Spika, unapofuatilia mijadala ilijojitokeza kuhusu suala hili, unagundua kuwa kumekuwepo na dhana kwa baadhi ya Watanzania ambaio sio Waislamu kwamba Kadhi anamhukumu mwizi kukatwa mkono na mzinifu kupigwa mawe hadi afariki. Kazi ya Mahakama ya Kadhi sio hiyo. Kazi yake kubwa ni Ndoa na Mirathi. Kwa karne nydingi, upande wa pili wa Muungano yaani Zanzibar kumekuwepo na Mahakama za Kadhi na sijawahi kuona hukumu za ajabu. Hapa Tanzania Bara pia Mahakama ya Kadhi ilikuwepo hadi mwaka 1963 ilipofutwa, lakini hadi leo Waislamu hawajaelezwa kwa nini Mahakama hiyo iliondolewa.

Mheshimiwa Spika, shida kubwa pia hutokea pale binti anapofiwa na wazazi na hana Mawalii, basi ni Kadhi tu ndio anayeweza kufungisha ndoa ya binti huyo. Mheshimiwa Waziri unawaambiaje jumuuya yote ya Watanzania waliopo hapa nchini kuhusu Mahakama ya Kadhi ambayo Chama cha Mapinduzi iliahidi kuishughulikia katika Ilani yake ya mwaka 2005? Hofu yangu ni kwamba inawezekana sasa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 isiitaje kabisa Mahakama ya Kadhi, kosa ambalo litawasikitisha hata wapigakura wake ambaio ni Waislamu.

Mheshimiwa Spika, Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Augustino Ramadhani, alipouliwa swali kuhusu Mahakama ya Kadhi huko Iringa Chuo Kikuu cha *Saint Augustine*, ye ye alisema hana matatizo juu ya uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi. Alisema hivyo kwa sasabu alishafanya kazi pamoja na Makadhi huko Zanzibar mmoja akiwa Kadhi Sheikh Rashid Mohammed, baba yake Kiongozi wa Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Ofisi hii ilianzishwa kwa Sheria Na.1 ya mwaka 2008. Sababu kubwa ya kuanzisha Ofisi hii, ni kutenganisha kazi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa Mashtaka. Uamuzi huo ulipatikana

kutoka Tume ya Msekwa ya 1977 baada ya kugundua kuwa shughuli ya kuendesha mashtaka ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa Ofisi hii imeanzishwa na Sheria Na. 1 ya mwaka 2008 kama ilivyoanzishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkoo kwa Sheria Na. 4 ya 2005 lakini hadi sasa Ofisi ya *DPP* imeendelea kufanywa ni Idara mojawapo chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkoo na hivyo kuwa tegemezi na kupoteza dhana nzima ya kuitenganisha na Ofisi ya Mwanasheria Mkoo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya *DPP* mara nyingi inapata vikwazo vyta kuendesha kazi zao kwa haraka. Kwa mfano, *Vote* 16 na 35 zinaonekana zinatakiwa zikidhi Ofisi ya *DPP* lakini wanapohitaji fedha ni lazima wakaombe kwa AG. Kazi ya kuwaita mashahidi Mahakamani ni kazi ya *DPP*, hivyo ukosefu wa fedha kwa ofisi hiyo ni kuzidisha malalamiko kuhusu ucheleweshaji wa kesi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkoo haijui mahitaji ya Ofisi ya *DPP* juu ya idadi halisi ya Mawakili wa Serikali wanaohitajika. Lakini kwa ilivyo, Ofisi ya *DPP* hawana uhuru wa kuajiri na wanalazimika wakaombe kibali Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali. Sambamba na hilo ofisi ya *DPP* haiwezi kutengeneza mpango mkakati wa maendeleo (*strategic development programme*) ya ofisi hiyo. Hii inazidisha kudumaza Ofisi hii, kwani Kikatiba ofisi hii inatakiwa iwe huru kiutendaji.

Mheshimiwa Spika, katika utafiti niliofanya, nimegundua kuwa wafanyakazi wa AG hawafikii hata 50. Wakati Ofisi ya *DPP* kwa Dar es Salaam tu wapo zaidi ya 50, Mwanza zaidi ya 30 na Mbeya 18. Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba Ofisi ya *DPP* ipewe uhuru kamili, kwa kuwaachia washike *Vote* zao wenye, kwa sababu Ofisi ya Mwanasheria Mkoo ina vipaumbele vyake na pia *DPP* anavyo vyake. Kama Wizara imekwama kwa hili basi Kambi ya Upinzani itafanya Mpango na Ofisi ya *DPP* Zanzibar ili waweze kuwapatia semina namna ya kutenganisha ofisi mbili hizi. Kubakisha Ofisi hizi mbili kama zilivyo basi ofisi ya AG itakuwa ina-*abrogate* na ku-*limit power* za *DPP*.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria Mkoo ndiye Mshauri Mkoo wa Serikali kuhusu masuala yote yanayohusu Sheria. Hivyo basi, usimamizi wa Katiba ya nchi uko chini yake. Ofisi ya *DPP* inatajwa katika Katiba kama Ofisi yake inavyotajwa, Ibara ya 59B inasema kwamba Ofisi ya *DPP* ina mamlaka kamili. Mamlaka kamili maana yake ni kuwa aweze kuajiri, awe na *Vote* yake na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inauliza inakuwaje Ofisi ya *DPP* inakuwa kama Idara katika Ofisi ya AG? Aidha, tunaamini na kutambua jinsi Mwanasheria Mkoo wa Serikali alivyo makini katika kazi zake, lakini inashangaza ni kwa nini anashindwa kuona jambo kama hili linalokwamisha utendaji mzima wa Ofisi ya Mkurugenzi wa

Mashitaka. Kambi ya Upinzani inapendekeza kwamba wakati umefika AG aiachie uhuru wake Ofisi ya DPP kwa kufuata mfano mzuri uliopo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofî*)

SPIKA: Nakushukuru sana Mheshimiwa Fatma Maghimbi kwa kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani. Tunaendelea.

Waheshimiwa Wabunge, walioomba kuchangia ni Waheshimiwa Wabunge wanane lakini kama kawaida tutaanza na wale ambao hawajachangia katika Wizara yoyote, ambao ni Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Janet Mbene na Mheshimiwa Magalle John Shibuda.

Waheshimiwa Wabunge, waliochangia mara moja ni Waheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Diana Chilolo na aliyechangia mara mbili ni Mheshimiwa Said Amour Arfi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mpangilio nilioutaja, tutaanza na Mheshimiwa Ernest Mabina na Mheshimiwa Martha Mlata ajiandaye.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Wizara ya Katiba na Sheria. Kwanza kabisa, nataka kutoa pongozi kwa Wizara hii, kwa kazi kubwa anayoifanya ikiongozwa na Waziri Mathias Chikawe, Mbunge wa Nachingwea pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara hii ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, nimelazimika kusimama hapa kwanza kabisa nianze kwa kutoa shukrani kwa Chama chetu cha Mapinduzi, kikiongozwa na Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuona na kuipa kipaumbele Wilaya ya Geita na kuanzisha Mkoa mpya wa Geita. Nashukuru sana kwa sababu lilikuwa ni lengo letu na madhumuni ya wananchi wa Geita. Kwa niaba ya wananchi wa Geita, tunaishukuru sana Serikali ya CCM kuweza kukubali ombi letu la kutuletea Mkoa mpya wa Geita.

Mheshimiwa Spika, pili, nimshukuru Waziri Mkuu ambaye ameweza kusukuma na kuweza kuleta Mkoa huu wa Geita. Katika kumbukumbu za *Hansard* mwaka 2002 wakati akiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, nakumbuka niliuliza swali la kuanzisha Mkoa wa Geita alijibu kwa kukataa lakini akanipa maelekezo, tumeyafuata maelekezo yale na leo hii kwa ajili ya busara yake na kwa wananchi wa Geita wamemuombea mpaka amekuwa Waziri Mkuu lakini ametimiza ahadi yake ya kutupa Mkoa wa Geita, tunashukuru sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, huo ni mwanzo tu lakini unaweza ukakuta kwamba kuna uanzilishi na hata katika wanyama utakuta kwamba kuna wanyama wanaowinda sana lakini unakuta wanakula kidogo wengine wanakuja kumalizia. Kama simba akiwinda anaweza akapata nyama lakini anayekuja kufaidi ni yule fisi ambaye anakula yale

makombo. Sasa tunaomba tu kwa sababu sisi ndiyo waanzilishi na ukiangalia katika takwimu utaona kwamba kuna vitu ambavyo tuliweza kuviwekea umuhimu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia takwimu za mwaka 2002, utakuta kwamba Geita kulikuwa na watu laki saba na thelathini na tisa elfu (739,000). Jimbo la Geita lina watu (302,000), Jimbo la Busanda lina watu (323,000) Jimbo la Nyang'wale lina watu (159,000). Ukiangalia kuna Wilaya ambazo zimeingizwa katika Mkoa huu. Jimbo la Chato lina watu laki mbili na tisini na nne (294,000). Jimbo la Bukombe lina watu laki nne na themanini na tatu, kwa hiyo utaona kwamba Jimbo au Wilaya ambayo ilikuwa na watu wengi ni Wilaya ya Geita. Itakuwa maajabu wengine wanasema kwamba Makao Makuu yataenda Chato, naomba hilo lifutike kwa sababu walioanzisha ni wengine. Najua kabisa Geita kama Mkoa wa Geita Makao Makuu yatakuwa Geita. Nimelazimika kuyasema haya kwa sababu kuna mtu mwngine anaweza akaingilia hapa ikawa ni tabu tupu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo maneno mazuri ya kupata Mkoa Geita, tumepata Wilaya ya Nyang'hwale, tumepata Halmashauri ya Nyang'hwale, kwa kweli ni faraja kubwa kwa wana Geita na wajue kabisa kwamba kuna wawakilishi wanaosilisha mawazo yao ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kazi kubwa ya kutulea sisi wana Geita, umefanya kazi kubwa sana, katika maelekezo yote uliyotoa tumeyafuatilia, hadi sasa hivi tumepata Mkoa wa Geita, lakini siwasahau Wabunge wa Geita kwa ujumla, namheshimu sana Mheshimiwa Marehemu Faustine Kabuzi Rwilomba alikuwa anaupigania sana Mkoa wa Geita, angekuwepo hapa mngeona cheche zake lakini mahali alipo tumuombnee Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi, niombe familia yake ichukue jukumu hili la kuweza angalau tumheshimu katika familia ile na kuweza kuwa nao karibu kama inavyohitajika. Nimheshimu Mheshimiwa Musalika ambaye amekuwa mpiganaji mkubwa kwa kupata Mkoa huu, Mheshimiwa Lolesia Bukwimba pamoja kwamba amekuja hivi karibuni lakini ameweza kufanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, ninaomba kusema kwamba Wizara ya Katiba na Sheria, pesa iliyotengwa ni kidogo sana, wana kazi nyingi mno ukilinganisha na kazi zilizopo, ni sawa sawa na Wizara ya Elimu, ni sawa na Wizara ya Afya au ni sawa sawa na Wizara ya Mambo ya Ndani. Huwezi ukatenga shilingi bilioni 117 kwa kazi kubwa kama hizi wanazozifanya. Ni Wizara ambayo inategemewa katika kila sehemu, ni Wizara ambayo inategemewa na Chama Tawala na Vyama vya Upinzani. Hawa ndiyo wanaweza kuweka haki katika sehemu hiyo. Lakini tumekuja kuona kwamba wanapewa pesa kidogo mno hata ukipiga mahesabu tu utakuta kwamba kila Mkoa utakuwa unapata bilioni nne, ukigawa kwa kumi na mbili utakuta wanapata milioni mia tatu, milioni mia tatu ukigawa kwa Wilaya zake ni pesa kidogo mno. Unawenza ukaona kwamba ni pesa nyingi ambazo wamepewa, lakini ukijaribu kuzichambua utakuta

kwamba wamepata pesa kidogo mno. Kwa hiyo, naomba kwa sababu tunapitisha basi niombe kwa siku zijazo Wizara hii iangaliwe kwa macho yote.

Mheshimiwa Spika, ninasema haya kwa sababu kuna sehemu ambazo zimekuwa na matatizo makubwa, kuna watu wana kesi wamo mahabusu, watu ambaao wapo mahabusu ni wengi zaidi kuliko waliohukumiwa kesi zao. Kwa hiyo, unakuta pesa waliyopewa ni ndogo sana. Mfano katika Mahakama ya Wilaya ya Geita wameshindwa kuwalipa Wakalimani ambaao wanaweza kufasiri kutoka lugha ya Kisukuma na Kiswahili. Kwa hiyo, kesi nyingi zimebaki pale pale. Huwezi ukasema kwamba watu wote wameshajua Kiswahili au wamejua Kiingereza, hakuna! Zinahitajika pesa za Wakalimani.

Mheshimiwa Spika, kuna kesi moja ambayo nimeifutilia kwa ukaribu zaidi, kuna vijana ambaao wana kesi yao wako mahabusu tangu mwaka jana kesi yao imekosa Mkalimani tu. Kwa hiyo, wamejikuta wamekaa mahabusu muda wote. Tuanzishe utaratibu ambaao utakuwa ni mzuri zaidi. Mtu atakapokuja kuhukumiwa na muda aliokaa Mahakamani basi siku alizokaa Mahakamani zihesabike kama aliquwa amefungwa, ili zipungue katika kifungo chake. Mtu anawenza kuwa mahabusu miaka miwili, mitatu kesi yake haijasomwa Mahakamani sasa utakuwa humtendei haki mtu huyu. Naomba Serikali iwaongezee pesa katika eneo hili ambalo ni zuri zaidi na linaweza likasaidia na hii ni sehemu ambayo inatoa haki kwa kila mtu.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba katika maeneo ya kwetu tumeanzisha Jeshi letu la Sungusungu. Jeshi hili limekuwa na manyanyaso makubwa kwani halijui sheria. Lakini kitu ambacho kinahitajika kuwaelekeza ni sheria ipi ambayo inaweza ikawasaidia. Tupo katika dhana ya ulinzi shirikishi pamoja na Sungusungu, ambaao wameweza kusaidia matukio mengi ya ujambazi ya wizi na mambo mengine mengi ambayo yanaweza yakaleta vurugu katika Serikali yetu, lakini Jeshi hili badala ya kutendewa haki kwa sababu ya kutokujua sheria unakuta limekuwa na manyanyaso. Wengi wamefungwa, kama ndugu zangu wengine pale Kasamwa, Katoro na Nzera na maeneo mengi ya Geita unakuta wamekuwa na matatizo. Leo hii tulikuwa na tatizo moja la Sungusungu walishika majambazi walipotoka kule, majambazi walikuja kuwasizingizia kwamba wameharibu mali zao, wameshaanza kushikwa na Polisi, lakini yote haya ni kwa kutokujua sheria.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. JANET Z. MBENE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Nichukue nafasi hii kuwapongeza Waziri wa Katiba na Sheria na Mwanasheria Mkuu, hotuba aliyoitoa ni nzuri. Vile vile niipongeze Serikali kwa juhudhi ambazo wanazifanya katika kuhakikisha kuwa utawala wa sheria unadumishwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujikita katika masuala mawili yanayohusiana na haki za binadamu na usimamizi wake kisheria. Kutokana na matukio mengi ambayo yanaendelea kuonekana kila siku na mengine yanaripotiwa na mengine hayajari potiwa katika vyombo vya habari, kuna masuala mengi ya haki za binadamu ambayo bado hayajafanyiwa kazi inavyopaswa. Nikiangalia hasa masuala ambayo yanawaathiri watu wa kawaida katika jamii, masuala ya utekelezwaji wa familia, masuala ya ukatili wa kijinsia na mauaji ya wanawake na watoto. Nikiangalia masuala ya ukatili dhidi ya watoto, wanawake na walemvu, inaonekana kuwa kuna upungufu mkubwa katika maeneo manne muhimu ambayo mimi nimeyatambua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kuna suala la uelewa mdogo kwa wananchi kwa ujumla kwa dhana nzima ya haki za binadamu. Pili, kuna suala pia la kutokutilia maanani hii dhana nzima na usimamizi wake kwa wasimamizi wakuu wa haki za binadamu katika ngazi mbalimbali za utawala hasa zile za chini. Tatu, kuna uelewa mdogo wa watawala wa ngazi za chini na kati juu ya wajibu huo kwenye masuala ya haki za binadamu, taratibu zinazotakiwa kufuatwa na hatua gani zichukuliwe wakati madai mbalimbali yanapowafikia. Nne, kwa maoni yangu nafikiri kuna tatizo la utashi wa kisiasa katika suala zima la haki za binadamu kwa maana ya kuwa hatujaonesha kabisa kama kweli tunajali sana mambo ya haki za binadamu. Tusingeendelea kuona wanawake wanapigwa na kuuwawa kila siku na waume zao, watoto wanachomwa na wazazi wao au unakuta watoto wanatelekezwa na baba zao wengine wenye uwezo mzuri tu na bado hakuna kitu kinachofanywa juu ya watu hao. Hata sheria zinavyofuatiliwa hazifuatiliwi kwa ule uzito unaotegemewa.

Mheshimiwa Spika, kuna nchi zingine ile tu kujulikana kuwa fulani amezaa na fulani inatosha kuhakikisha kuwa huyo bwana anamlipia mtoto na anamtunza. Sasa hapa kwetu hata ushahidi ukiwa wa namna gani bado unakuta watoto wanatelekezwa. Kwa hiyo, inaongeza matatizo ya kuwa na watoto wa mitaani, akina mama wanazidi kuhangaika na watoto peke yao wakati wazazi wenzao wapo.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la kutokufuata sheria, tukiangalia hata mijini tu masuala ya matumizi ya barabara, watu wanaendesha magari ovyo ovyo, ajali zinatokea ovyo ovyo lakini sheria zipo hazifuatwi na Askari Polisi (*Traffic*) wapo hapo hapo wamesimama wanaangalia, ajali zinatokea kwa sababu tu ya uzembe unaotokana na kutokufuata sheria.

Mheshimiwa Spika, tukija mitaani masuala ya uchafuzi wa mazingira yetu na uchafu uliozagaa yote hiyo ni katika kutokuzingatia sheria ambazo zipo lakini hazifuatwi na wanaozisimamia hawazifanyii kazi. Sasa haya kwangu mimi ni matatizo na ningependa kuona jinsi gani ambavyo hivi vitu vinatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, nafahamu na ninatambua kuwa bajeti inayotolewa ni ndogo sana hata mimi nimeshangaa kuiona, lakini nafikiri itabidi ifikie mahali tuangalie jinsi gani tutahakikisha hivi vitu vinafanya vizuri. Kwanza, kuna haja sana ya kutoa elimu ya hali ya juu kwa wananchi wote juu ya haki za binadamu na suala zima la kuzingatia sheria na kuzielewa sheria zenewe ili mtu anapoenda kukamatwa kuwa hajazifuata aelewé kuwa amevunja sheria. Lakini vile vile kuna suala zima la kuwawezesha Wizara na vitengo mbalimbali vinavyosimamia hizi sheria kuwa na uwezo wa kifedha ili kuwa na vifaa vinavyohitajika ili kufuatilia haya masuala ya ukiukwaji wa sheria. Napendekeza elimu hii itolewe kwa sehemu zote zinazohusika, siyo lazima iwe Wizara ya Katiba na Sheria peke yake, hata Wizara zingine ambazo zinaguswa na masuala ya kisheria nao pia wachukue jukumu hilo kwa upande wao, ili hili suala lisiachiwe Wizara husika peke yake. Wizara iwe ni mratibu tu.

Mheshimiwa Spika, kuna masuala ya taaluma vile vile ya kukabiliana na matatizo kwa mfano masuala ya kubaka au kubakwa, sina hakika kama Polisi wote wanawenza kushughulikia masuala haya, sijui kama wao wenyewe wanaelewa ni jinsi gani ya kumshughulikia mtu aliyeletwa pale amebakwa au amelawitiwa au pengine amepigwa na Mumewe au Mkewe. Ningependa kuona ni jinsi gani kunakuwa na vitengo maalum vinashughulikia haya masuala katika vituo vyetu vya Polisi au katika Serikali zetu za mitaa katika ulinzi shiriki. Kuna namna ya kushughulikia hivi vitu ili vianze kuwa vinashughulikiwa hata katika ngazi za chini kabla hata havijafika huko juu.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kuna picha iliyojitokeza kuwa sheria inapindwa vyovoyote vile na hakuna mtu anayejali. Sasa sisi kwenye jamii hiyo inatumiza na hasa wanawake na watoto. Unapokuwa unaogopa hata kwenda kushtaki kitu kwa sababu unajua hakuna lolote litakalofanywa, hiyo moja kwa moja inakutia unyonge katika nchi yako.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba niishie hapa lakini nafikiri nimetoa maoni yangu na naunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

MHE. MAGALLE J. SHIBUDA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia fursa hii na mimi niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Sheria. Awali ya yote, nachukua fursa hii, kumpungeza sana Waziri Mathias Chikawe, Mbunge wa Nachingwea kwa juhudhi zake za kuthamini wananchi wa Jimbo la Nachingwea na vile vile naomba niwatendee haki wazazi wa Jimbo la Nachingwea kwa kuwatahadharisha kwamba, kama mtampoteza mtoto huyu majuto ni mjukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mathias Chikawe anaweza kuthaminisha matatizo ya Nachingwea, anaweza kusadikisha taasisi mbalimbali zinazohitaji kutoa huduma mbalimbali kwa ustawi na maendeleo ya Nachingwea. Natambua huu ni msimu wa mazalia ya watu wanaokuja na maono ambayo tunaita mafataki ya kisiasa, wanaoleta kanga, wanaoleta pesa, kwa hiyo nawatahadharisha wananchi msidanganyike, Wabunge waliopo hivi sasa ni watu ambao wana kasi na mwendo ambao umeboreshwa na Bunge la

kisasa chini ya Spika, Mheshimiwa Samuel Sitta, Mbunge na chini ya maangalizi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda.

Mheshimiwa Spika, naomba wananchi mtambue kabisa kwamba unapobadilisha mtu, kasi ya mwendo inabadilika. Kwa hiyo, nawaomba msiwabadiishe, Wabunge wote warejesheni ili kasi iende kwa kasi ya nyongeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani na pongozi hizo, naomba kutambua kwa heshima na taadhima mchango mkubwa wa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Augustino Ramadhani. Kwa kweli Mheshimiwa Jaji Mkuu japo anaelekea kustaafuli, katuachia somo na changamoto moja kwamba uzalendo utangulie masuala ya ubinafsi. Alipewa fedha za kujenga nyumba yake akaamua asijenge nyumba ya ufahari kwa maslahi yake akasema ajenge nyenzo ya Taifa, nyumba ya utawala. Nampongeza sana Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa kutupa funzo ambalo daima ni urithi wa kutambulika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jaji Mkuu vile vile napenda kumpongeza kwamba amekuwa na mlango wazi wa kusikiliza na kuhudumia wananchi ambao ni duni ambao wako katika msako wa maisha yao, wako katika msako wa haki zao. Nampongeza sana na ninaomba kila mtu anayepata madaraka tuache mimi Mkurunene yaani mimi ni mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa pongozi hizo, sasa naomba nijielekeze katika masuala ambayo kwa kweli yanahitaji yatazamwe. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa uteuzi mwingi wa Majaji ili kuimarisha huduma za Majaji katika Mahakama za Rufaa. Lakini naomba jambo moja nitoe angalizo na nimuombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, pamoja na Waziri mhusika, bila uzoefu, ujuzi hupungua. Kwa hiyo, ni muhimu sana sana wanaoteuliwa wakaandaliwa, wawe na watu ambao watavuna kwao, Jaji Mkuu aliyekuwepo alikaa na kiasi fulani akatuachia hekima fulani. Lakini hivi sasa watu wenye siha, wenye akili, wenye busara wenye hekima ambao wana sifa za uadilifu tunawapoteza kwa sababu ya kujiwekeea Sheria ya miaka 60. Mwaka 1962 tulijua miaka 60 mtu anakuuwa mkongwe ambaye sasa yuko alasiri ya kuelekea katika maisha ya Ahera lakini si kweli kwa hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Afrika ya Mashirika, Kenya, Uganda umri wa kustaafuli ni mkubwa kuliko wa Tanzania. Je, wenzetu hao wameona nini kwamba ni hekima wao waongeze umri wao. Hii ni kwa sababu uzee ni dawa. Kwa hiyo, kwa sababu uzee ni dawa ningeomba sana *ku-fast track* tufanye marekebisho katika sheria zetu, tuweze kuongeza umri kama mtu ana matatizo basi kanuni na mabaraza yapo lakini wale ambao wanahitajika kuwa na kazi kwa maslahi ya ustawi wa Taifa letu tusiwapoteze. Naomba sana suala hili litazamwe na kwamba ni kweli liko kwenye Katiba lakini hii Katiba si Msaafuli wa Mwenyezi Mungu. Mnawenza mkaleta hati ya dharura tukafanya marekebisho. Hebu muangalie hawa vijana waliooteuliwa na Mheshimiwa Rais watavuna wapi *legacy*. Kwa kweli hili ni pengo kubwa kama pengo likiendelea kuwa kubwa hata kasi ya ufanisi wa mahali popote

haiendi na kasi kwa sababu watu hawana uzoefu hivyo wanakwenda kwa uangalifu hadi watakapovuna uzoefu. Naomba Serikali ilitazame kwa makini suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kusema jambo lingine kuhusu mfumo wa dhamana. Ninaomba sana pawe na mwongozo elekezi. Kwa kweli ustawi na maendeleo ya kijamii tunatofautiana Mikoa na Wilaya. Mimi kule Maswa watu wangu ni duni sana. Sasa kama patakuwa na mwongozo *standard* tu kwamba dhamana kwa kesi hii ni kitu fulani sasa Wasukuma wangu tuna nyumba za nyasi, hatuna hati za nyumba, hata umilikishaji na urasimishaji bado haujatendeka. Sasa ninaomba pawe na mwongozo ambao umefanyiwa upembusi yakinifu wa kuzingatia kwamba haki ya kupewa dhamana inatekelezeka na inatendeka. Hilo litatusaidia sana kuhakikisha kwamba tunasonga mbele. Hii nimesema kwa sababu asilimia 75 ya Watanzania bado maisha yao ni duni, ni tofauti na Dar es Salaam, Tanga na maeneo mengine ambayo yana ustaarabu wa masuala ya mjini. Kwa hiyo, ninaomba sana suala hili litiliwe mkazo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mlundikano wa kesi katika Mahabusu au katika Magereza yetu, Mahakama imekuwa ni mahali ambapo sasa hivi kesi wanasukumiwa. Kule kwangu Maswa, akiona Askari hii ina utata wanasema mpelekeni Mahakamani. Sasa mtu kwa sababu anatuhumiwa kwa maelezo ya maandishi na Mahakama nayo inasikiliza maelezo ya maandishi hana ufahamu wa jambo lolote anatoa masharti ya dhamana mtu anapelekwa mahabusu. Wakati umefika kwa kweli pawe na ushirikiano wa kuhakikisha kwamba hizi tuhuma zinazotolewa na sheria tunazosema kwamba uchunguzi ufanyike kabla ya mtu kupelekwa Mahakamani na akanyimwa dhamana, naomba utekelezwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba atakuja Maswa, sasa ninaomba Mheshimiwa Waziri, natambua kipindi hiki ni kigumu kwake. Naomba utoe kauli ambayo itasema kwamba utakuja Maswa au ataleta Tume ya Mwanasheria Mkuu apitie Magereza, wakaangalie watu waliopo Gerezani, wengi wao walikuwa na mifugo mingi sana lakini sasa hivi wamebakiza ng'ombe wane au watano tu lakini walibambikizwa kesi za mauaji. Kwa hiyo, ninaomba kwa sababu Mahakama inapelekewa mtu na maelezo na inachukua hatua hizo, lakini uchunguzi na upelelezi haupo, kwa kweli Wasukuma wangu, wameonewa sana. Waganga wa Jadi wameonewa sana kwa sababu anakutwa na mfupa tu anaambiwa aliua mtu na ndiyo maana namwomba aje Maswa. Naomba atoe kauli na kama haiwezekani, naomba ofisi ya Mwanasheria Mkuu ishirikiane na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka waje Maswa watembelee Mahakama waangalie kwa nini watu wamekaa rumande miaka saba.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, nakutakia kila la kheri, karibu sana Maswa. Nawashukuru sana wananchi wa Maswa kwa sababu wananipenda, wana imani na mimi na baada ya kuahirisha kugombea Urais naahidi sasa nguvu zangu zote nitazielekeza katika Jimbo la Maswa, ahsanteni. (*Makofi*)

MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri wa

Katiba na Sheria pamoja na Mwanasheria Mkuu na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Lakini niruhusu nimpongeze Mheshimiwa Jaji Mkuu pamoja na watalaan wake kwa jitihada wanazofanya katika kuhakikisha kwamba mhimili huu muhimu sana bado kazi zinafanya.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ni mhimili muhimu. Mahakama inakamilisha kazi tunazofanya kama Bunge, inakamilisha kazi zinazofanywa na Serikali. Inapokuwa kwamba mhimili huu muhimu ni kama amenyongwa kwa sababu ya kutopatiwa rasilimali za kutosha ni wazo kwamba athari zitakuwepo katika mihimili ili mingine miwili kwa maana ya Bunge na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu Mahakama imekuwa ikipewa fedha chache sana na kwa kweli kwa watu wa Kamati yangu waliotembelea Mahakama za Wilaya, Mwanzo katika maeneo kadhaa ukitembelea kila Mahakama, unaona athari ya kutopewa fedha za kutosha. Maana ukiangalia kwa kweli mengi yanashindikana kutekelezwa, ofisi nyingi za Serikali kwa sasa ukiingia hali ni nzuri sana, *furniture* za hali ya juu na za gharama, *computer* ni nyingi lakini Mahakama nyingi ukienda hasa katika ngazi ya Wilaya ikiwa kilomita 50 kabla hujaingia ndani unachosikia ni wimbo wa *typewriter* ya Olivet ikiimba tatata tatata na hii ni ishara ya kiasi cha fedha kinachotengwa kwa ajili ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Mahakama iko katika Mikoa yetu yote na katika Wilaya zote na Mahakama za Mwanzo lakini pamoja na kwamba hatua rasilimali za kutosha bado ninadhani binafsi kwamba Mahakama wangeweza kupewa fedha zaidi kwa sababu Mikoa kadhaa kuna Mikoa zaidi ya saba ambayo imepatiwa katika bajeti na ni zaidi ya Mahakama chombo ambacho kipo katika nchi nzima. Nadhani ni vizuri kujaribu kuwa na utaratibu wa kuona kwamba hata tujifunze kutoka kwa wenzetu kwamba ni *share* kiasi gani cha bajeti yetu kitaifa ndiyo tungelipaswa kutoa kwa mhimili huu muhimu ili dira pamoja na *vision* yao iweze kubaki kama wanavyosema wenyewe kwamba ni kutoa haki sawa kwa wote tena kwa wakati maana hii inashindikana kutekelezwa kwa sababu ya uhaba wa hizo fedha.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine linalojitokeza vizuri utaona kwamba kuna shughuli nyingi zinazosubiriwa kupokea fedha kutoka kwa wahisani. Nadhani kwa mhimili muhimu kama huu si vizuri kuacha maeneo kadhaa yasubiri fedha za wahisani. Maana nina hofu huenda mambo mengi muhimu katika kutoa haki ambayo hayatatekelezwa kwa sababu fedha za wahisani hazikupatikana ama za kutosha, ama hazikupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watumishi Mahakama ni ndogo, tumepata malalamiko mengi kutoka kwenye Mahakama za Mwanzo, Mahakama za Wilaya, Mahakama Kuu kwamba hawatoshi. Lakini hata wale wachache waliopo kunakuwepo na tofauti kwamba inategemeana kwamba mmoja kaajiriwa katika ofisi ipi na malipo yanaendana zaidi na mahali walipoajiriwa zaidi kuliko kazi wanayoifanya. Kwa hiyo,

wakati umefika nadhani Wizara ijitazame, Mahakama ijipange vizuri zaidi na kuzingatia kwa watazingatia *equal opportunity policy* kwamba kwa watu wanaofanya kazi sawa, malipo yawe sawa bila kujali kwamba faili la ajira kwa mtu huyu lipo katika ofisi fulani. Kwa sababu hii inawavunja moyo baadhi ya watu na kumekuwepo nadhani na kutegeana katika maeneo fulani kwamba hawa wanaolipwa vizuri zaidi wenye maslahi mazuri zaidi, tutaona watakavyotekeleza majukumu yao bila mchango wetu sisi tunaolipwa fedha kidogo zaidi. Kwa hiyo, kuna haja ya kutazama kwa uhakika ili angalau *moral* iweze kuwepo na jitihada ziwepo za kuhakikisha kwamba haki inatolewa na iwe haki sawa kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, malalamiko yanayotokea mara nyingi, mengine ndiyo hayaeleweke sana maana kuna maeneo mengi wanalamika kwamba wameshindwa kukata rufaa wengine kufuutilia haki zao kwa sababu tu ya kukosa nakala ya hukumu. Hili pamoja na uhaba wa rasilimali huenda kuna ukosefu pia wa utashi wa kisiasa. Kwa hiyo, ningeshauri Mheshimiwa Waziri pia aketi pamoja na *team* zake kuona ni kwa jinsi gani yale yanayowezekana yafanyike kwa sababu kwa kufanya haya watu wataguswa zaidi na nafasi ya Mahakama na watakuwa watetezi wazuri wa Mahakama pamoja na Wizara nzima katika kuhakikisha kwamba wanaongezewa rasilimali kwa kupata bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kucheleta kusikiliza kesi pamoja na kuamua hili pia limechanganyika maana ni kweli rasilimali zinachangia kwa uhaba kwamba wanashindwa kuwaleta mashahidi lakini pia kuna maeneo mengine ambayo labda pia linatumika kama kisingizio kwa baadhi ya kesi kuwanyima watu haki. Ni vizuri jitihada ziwepo ili watu wanaotafuta haki waweze kuona kwamba jitihada hizi zipo na kuona kwamba pale wanapokwama watu wanakwama kwa sababu ya uhaba wa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, chini ya Wizara hii, kuna Tume muhimu sana. Kama vile Tume ya Haki za Binadamu, Tume ya Kurekebisha Sheria na hizi ni Tume muhimu moja katika kuhakikisha kwamba kwanza haki inatolewa lakini pili kuhakikisha kwamba tunachokazania kuimba kila siku utawala bora, haya hayawezekani kama kuna ukiukaji wa haki za binadamu. Lakini na wao pamoja na kwamba ni Tume kubwa wanashindwa bado kufanya kazi zao kwa sababu ya ukosefu wa rasilimali. Nadhani tujaribu tena kuzingatia na kuona kwamba kuna haja gani ya kuwa na Tume nyingi na kubwa endapo tunashindwa kuiziwezesha zifanye kazi hizi zilizokusudiwa. Tume hizi ni muhimu hasa katika kipindi hiki ambacho tunaona maadili katika jamii yetu yamezidi kumomonyoka. Tunaona watu wanavyouwawa, wanavyonyongwa kiajabuajabu na ni vizuri kama Taifa, Tume hizi ziweze kufanya kazi ya kutuhabarisha ili kuweza kutafuta suluhu katika matatizo yanayotukabili sasa.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kupendekeza tu kusema kwamba kwa muda mrefu wimbo umekuwepo kwamba Mahakama watapewa mfuko wao ili wasimamie mambo yao wenyewe. Namuomba tu Waziri kwamba kwa kipindi kinachokuja, ajaribu kuweka mpango kazi kuhakikisha kwamba hili linafanyika. Lakini watumishi pia wanaojiriwa katika maeneo tofauti, wote wanaofanya kazi chini ya Mahakama, ningeshauri wote wawe chini ya ajira moja ili usimamizi uweze kuwa rahisi na taratibu

pia za kinidhamu ziweze kuchukuliwa kwa urahisi ikiwa watakuwa chini ya mwajiri mmoja.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia kwamba Mahakama ijaribu kuwa na kitengo chake cha mipango chenyeye watalaam wa uchumi, watakaowasaidia hawa waliobobeia katika sheria, wafanye maandalizi ni nini hicho kinachotakiwa kwa maana ya mipango kwa maana ya bajeti ili Mahakama iweze kufanya kazi vizuri na kutimiza lengo lake na kutoa haki sawa kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie hapo, kwa kuunga mkono hoja nashukuru.
(*Makofi*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Singida pamoja na Mkoa wa Singida kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kueleza mambo ambayo napenda kumueleza Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, kwanza nitumie nafasi hii, kumshukuru yeeye mwenyewe Mheshimiwa Chikawe pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu wa Wizara hii, Watendaji wote walioshiriki kuandaa hotuba hii. Ni hotuba nzuri, hotuba ambayo imejali sana taasisi zote, ndani ya Wizara hii, ni matumaini yangu kwamba vipaumbele vyote vilivyoainishwa katika hotuba hii vitatekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, vile vile nimshukuru Mheshimiwa Rais, jinsi ambavyo ameendelea kujenga imani na akina mama wa Tanzania, amewateua wanawake Majaji wengi. Ni wazi kwamba Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, anatambua jinsi ambavyo akina mama wanajituma, jinsi ambavyo wamekuwa wawajibikaji wazuri. Nashukuru sana, tena yumo dada yangu Mheshimiwa Jaji Fatma Masengi, nilimtabiria siku moja atakuwa Jaji na kweli amekuwa Jaji. Hili nilimtabiria kwa sababu niliona utendaji kazi wake kwa miaka yote toka akiwa Hakimu wa Mahakama ya Wilaya, Mahakama ya Mkoa baadaye akawa Mkurugenzi wa Mahakama za Mwanzo Tanzania. Baadaye Mheshimiwa Rais alimteua kuwa Jaji wa Mahakama Kuu, Mungu ambariki sana. Ni matumaini yangu ataitumia nafasi yake vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kazi hiyo nzuri ya kuwatambua akina mama wenye uwezo wa juu. Ni imani yangu kwamba Watanzania watampa kura za kishindo ili aendelee kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aendelee kutambua akina mama wenye uwezo wa juu na vipaji vya juu ili tuendelee kushirikiana na wenzetu akina baba katika kuitumikia nchi hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi, nitumie nafasi hii pia niwashukuru akina mama wa Mkoa wa Singida, jinsi ambavyo wameendelea kuonyesha imani kwangu, imani ambayo imeendelea kunitia moyo ndiyo maana nimekuwa na nguvu ya kuchangia

hana Bungeni na kuwatumikia huko Jimboni. Ni imani yangu kwamba akina mama wa Mkoa wa Singida wataendelea kuonyesha imani hiyo kwangu na mwaka kesho naamini utaniona hapa. Nawashukuru sana akina mama wa Mkoa wa Singida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizi, sasa nijikite katika kuonyesha kero mbalimbali ambazo zipo Mkoani kwetu Singida.

Mheshimiwa Spika, la kwanza nilishawahi kuongea mara kadhaa hapa katika kuomba ujenzi wa Mahakama huko Singida. Nashukuru Serikali ilipokea maombi yangu na kazi hiyo ya ujenzi ilishakubalika, eneo tulishapata, lakini toka tumekubaliwa kujenga Mahakama bado hakuna fedha. Sielewi kigugumizi cha kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama kinatokea wapi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi huu wa Mahakama Mkoani Singida ulihainishwa toka enzi za Dr. Mary Nagu alipokuwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, na baadaye kaka yangu Mheshimiwa Chikawe ameipokea Wizara hii naye aliendelea kujenga imani ile ile ya Mheshimiwa Nagu kujenga Mahakama Singida. Sasa niombe katika bajei hii, hivi kuna hela yoyote iliyotengwa katika kujenga Mahakama Singida? Maana nimepitia kitabu cha pili, nimepitia kitabu cha nne siaona mahali ilipoandikwa ujenzi wa Makao Makuu Singida. Ninaomba sana Mheshimiwa kaka yangu, Mheshimiwa Chikawe wakati atakapokuwa anatoa majumuhihisho ya hotuba yake, basi atuambie Singida ametutengea shilingi ngapi ili wana-Singida tuendelee kufarijika katika kupata huduma katika Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza hili, niongelee suala la Mahakama ya Mwanzo Mkoani Singida. Naishukuru sana Serikali kwa jinsi ambavyo inajitahidi kukarabati Mahakama za Mwanzo. Najua ni nchi nzima, lakini mimi naongelea za Singida pamoja na kujenga Mahakama za Mwanzo pale anapoona kwamba majengo hayapo kabisa au yamechoka kiasi kikubwa. Kwa mfano, Mkoani Singida, Singida mjini tumejengewa Mahakama ya Mwanzo Utetmini. Mahakama ya Mwanzo ina majengo mazuri sana, naishukuru sana Serikali. Lakini cha kusikitisha, majengo haya mazuri yaliyotumia mamilioni ya Serikali kwa kipindi cha mwaka mzima hayajaanza kutumika. Mimi sielewi tatizo ni nini.

Hivi kama Serikali imeweza kujenga majengo mazuri hayo kwa thamani kubwa ya mamilioni ya pesa, hivi kweli Serikali hii ninayojua mimi ya CCM inaweza kushindwa kutoa fedha kwa ajili ya kununua samani tu? Ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wakati anatoa majumuhihisho yake atuambie kama atawenza kutuletea samani katika majengo haya haraka iwezekanavyo ili majengo haya yaliyotumia mamilioni ya pesa yaanze kutumika. Majengo mazuri ambayo anaweza akayafanya yakaja yakawa Mahakama ya Wilaya kabisa. Lakini yako tu yamekuwa nyumba za popo! Inasikitisha sana! Ninaamini kwa tabia ya Mheshimiwa Waziri, atasema lolote katika hili kwa sababu hili ni jambo dogo sana kwake, haliwezi likamharibia hata bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, sio hivyo tu, pamoja na jitihada za kukarabati Mahakama za Mwanzo, tumekarabatiwa Mahakama ya Ipembe, Mjini pale, Mahakama ya Shelui, Mahakama ya Ikungi lakini bado tunakabiliwa na Mahakama nyingi za Mwanzo ambazo

zinahitaji ukarabati. Sasa sijui Mheshimiwa Chikawe katika hili, kwa sababu sijaona kama ana mwendelezo wa kutosha katika kukarabati Mahakama za Mwanzo. Kwa mfano, ukienda Manyoni Mjini kwa kaka yangu Mheshimiwa Chiligitati ndio mambo haya ya kum-promote ndugu yako. Mheshimiwa Chikawe, Mahakama ya Mwanzo yaani ni duni kabisa. Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo Manyoni Mjini anaamulia kesi kwenye ofisi yake jambo ambalo kwa kweli halimpi tija wala hatumtendei haki. Tunaomba kabisa Serikali iangalie uwezekano wa kukarabati Mahakama ya Mwanzo hii ya Manyoni Mjini pamoja na Mahakama nyingine za Mwanzo ambazo nazo zinatishia maisha katika Wilaya zote za Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, vile vile Mkoa wa Singida hauna Mahakama ya Wilaya hata moja. Manyoni haina Mahakama ya Wilaya, Wilaya ya Singida haina Mahakama ya Wilaya, Iramba haina Mahakama ya Wilaya, yaani Wilaya zote hizi tatu, tena Mkoa mzima ulikuwa na Wilaya tatu tu. Tumeshindwa kuzijenge Mahakama ya Wilaya. Leo hii, Waziri Mkuu juzi katusomea Wilaya nyingine mbili, tunamshukuru Mungu tunasema Alhamdu-lillah, sasa hivi tuna Wilaya tano.

Sasa kama hizo tu Wilaya tatu mpaka leo hii hazina Mahakama za Wilaya: Je, tumeongezewa hizi mbili, Serikali haiyoni kwamba kulimbikiza matatizo kama haya ni kujibebesha mzigo mzito? Hivyo naomba basi, angalau leo tuambiwe kwamba tutaanza na Mahakama ya Manyoni ya Wilaya, tutapita labda Iramba, tutajenga labda ya Singida kwa sababu Mahakama ya Singida Wilaya hamna, kesi zao wanasikilizia kwenye majengo ya Mkoa. Hizi Wilaya nyingine, kesi zao wanasikilizia kwenye Mahakama hizi zilizokuwa Mahakama za Mwanzo, ambazo hazina tija wala hazimpi motisha kabisa, Hakimu kufanya kazi zake na zinatishia kabisa maisha hata ya watu wanaosikiliza kesi zao pale. Tunaomba sana katika Mkoa wa Singida tunahitaji maendeleo pamoja na majengo mazuri ya kufanya kazi. Mgetufanya haya, kwa kweli wanasingida tutaendelea kufarijika na tutaendelea kuwa Mkoa wa CCM siku zote na mwaka huu kwa kura za kishindo Singida tutaongoza.

Mheshimiwa Spika, vile vile Singida tuna kero ya gari. Mahakama ya Mkoa haina gari, tulishawahi kuletewa gari, lakini gari hilo kwa kweli lilifanya kazi kwa muda mfupi sana likaharibika. Mimi sielewi mlitolea wapi hayo magari. Magari ambayo nimefuatilia naambiya karibu nchi nzima yamekufa. Ni miaka miwili sasa Singida haina gari la Mahakama ya Mkoa. Hakimu, dada mmoja msomi mzuri, anachapa kazi vizuri anakosa gari, Watendaji wake wa chini wana magari. Hivi kweli huyu Hakimu tunamtendea haki kweli?

Mimi naomba huyu Hakimu asije akachukia Singida kwa sababu ya gari tu. Singida tunahitaji Watendaji, tena huyo mama ni Mtendaji mzuri. Tunaomba sana Mheshimiwa Martha apewe gari ili aweze kufanya kazi zake vizuri kwa sababu bado ana kazi kubwa, anatembelea Mahakama za Wilaya, anatembelea Mahakama za Mwanzo, atazungukaje huyu kama hana gari? Miaka miwili hana usafiri. Naomba tumhurumie sana tumpatie gari huyu Mheshimiwa Hakimu.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

MHE. SAID AMOUR ARFI: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami nitoe mchango katika hoja iliyoko mbele yetu. Uvumilivu daima huwa una kikomo. Hata mpira ukiuvuta sana, ufikia mwisho utakatika. Tumekuwa tukipigia kelele sana Idara ya Mahakama iweze kupewa hadhi na haki inayostahili kwa mujibu wa Katiba yetu tuliyojiwekea kama muhimili unaojitegemea kama ilivyo mihimili mingine, Bunge na Serikali, lakini bado hakijasikiliza. Hofu yangu tu isije kuchelewa sana ikaanza kuleta misuguano kati ya hii mihimili mitatu.

Ni dhahiri kabisa inaonekana muhimili huu ambao una umuhimu sana katika ustawi na maendeleo ya Taifa letu unapuuzwa. Nilikuwa naiomba Serikali ijitahidi kuhakikisha kwamba na muhimili huu unapata haki zinazostahili na kuwa na mfuko wake wa kuijendesha yenewe. Wenzangu waliotangulia wamesema matatizo kadhaa ambayo yanawakumba Idara ya Mahakama na hususan yamechangiwa kwa ukosefu wa rasilimali fedha. Fedha wanazotengewa ni kidogo sana, hazitoshelezi na zinapelekeea kazi za Idara hii kuwa ngumu zaidi na malalamiko na kero kutoka kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, wamezungumzia mlundikano wa mahabusu walioko katika Magereza yetu hali mbaya iliyoko katika Magereza na kadhalika. Lakini yote haya yanachangia kwa sababu muhimili huu unashindwa kufanya kazi zake kama inavyotakiwa ikichangiwa sana na ukosefu wa fedha. Lakini hata hali za hao Watendaji wenye we katika muhimili huu wa Mahakama inasikitisha sana, posho stahili na makazi ya watumishi wa Mahakama iko katika hali mbaya sana. Mahakimu wengi hawana makazi mazuri na ya uhakika na ya usalama kutokana na kazi zao wanazozifanya. Baadhi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wanaishi katika nyumba za kupanga, nyumba ambazo hazina hadhi na pengine niliwahi kumwona wakati fulani Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo, amepanga katika nyumba ya nyasi ambapo alikuwa pia anahatarisha pia maisha yake, angeweza kuchomewa wakati wowote.

Kwa hiyo, ni lazima sasa tuangalie ni namna gani tunaweza tukaboresha makazi ya watumishi wa Mahakama. Lakini pia haki zao za msingi nazo ni lazima ziangaliwe. Hali ya Mahakimu hususan Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo inasikitisha sana. Pamoja na kwamba ni haki yao ya msingi kupewa *court attire*, yaani posho kwa ajili ya mavazi, lakini hawapewi. Unakuta Hakimu ana koti moja tu, tena analazimika kulitundika ofisini, anaogopa hata akienda nalo nyumbani litazidi kuchakaa maana hana koti lingine. Kwa hiyo, *court attire* zao walipwe kwa wakati. Pia *case disposal* ambayo ni haki yao ya msingi katika masharti ya ajira zao na yenewe inachelewa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini sio Mahakimu tu, pia hata Wazee wa Baraza ambao wanalipwa kiwango kidogo sana, lakini bado hata hicho kiwango kidogo kinachelewa kufika kwa wakati. Mtu anakusanya Sh. 8,000/= lakini miezi mitatu hajalipwa Sh. 8,000=/. Inasikitisha sana na inawavunja moyo sana hawa wazee ambao wanawasaidia Mahakimu wetu katika Mahakama za Mwanzo. Lakini pia nilikuwa nataka kuiomba Wizara ijitahidi sana kufanya Semina elekezi zifanyike mara kwa mara kuhusu marekebisho na maboresho ya sheria kwa Mahakimu wetu kwa sababu katika Mahakama nyingi sasa hivi, bado wanaendelea kutumia sheria zilizokufa, sheria zilizopitwa na

wakati kwa sababu maboresho ya sheria hayawafikii katika Mahakama zao kwa wakati na pengine hawapati kabisa.

Kwa hiyo, naiomba Idara ya Mahakama ijitahidi sana kuhakikisha kwamba marekebisho yote ya sheria yanayofanywa, basi yawe yanafikishwa katika Mahakama zote, katika ngazi zote kwa wakati na pia kuhakikisha kwamba Mahakimu mara kwa mara wanapata maelekezo juu ya mabadiliko ya sheria ili kuendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, aidha, kumekuwa na matatizo makubwa sana hasa kwenye migogoro ya ardhi. Migogoro ya ardhi imepelekea wakati mwingine kuongeza kesi Mahakamani kwa sababu kutokuwepo na mabaraza ya usuluhishi pamoja na kwamba yapo katika ngazi za chini, lakini katika ngazi ya Wilaya hakuna, wanalazimika watu waende Mikoani kwa kukwepa gharama za kwenda kwenye mabaraza ya usuluhishi ya Mkoa. Kwa hiyo, wanalazimika kwenda Mahakamani na kuongeza idadi ya kesi. Ni vizuri sasa kukawepo na Baraza la Usuluhishi la migigoro ya ardhi katika ngazi ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, nimezungumzia pia majengo ya Mahakama kwamba yapo katika hali mbaya katika kipindi changu chote ambacho sasa kinaendea ukingoni. Nimekuwa nikilalamikia juu ya majengo ya Mahakama katika mji wa Mpanda. Mahakama ya Wilaya na Mahakama ya Mwanza. Lakini pamoja na matumaini ambayo nimekuwa nikipewa mara kwa mara na Mheshimiwa Waziri, lakini hata katika hotuba yake ya leo hakuna dalili yoyote katika mwaka huu wa fedha 2010/2011 kwamba Mahakama ya Wilaya ya Mpanda imetengewa kujengewa upya.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri umepita mara kadhaa Tabora, unaifahamu Mahakama ya pale Mjini Tabora. Basi ndivyo ilivyo Mahakama yetu ya Wilaya ya Mpanda na Mahakama hiyo Mheshimiwa Jaji anakuja pale kusikiliza kesi ambazo anatakiwa azisikilize katika kijumba kinachofanana na kile unachokifahamu pale Tabora mjini. Ni aibu! Ni fedheha kwamba kwa kipindi cha miaka 50 toka tumepata uhuru tunaendelea kutumia Mahakama iliyokuwa Mahakama ya Liwale. Naiomba sana Serikali iangalie ni namna gani pamoja na hali ngumu inaboresha Mahakama ya Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumzia hayo, nijikite sasa katika eneo la utawala bora. Uawala bora ni pamoja na kuheshimiwa sheria zilizopo na inasikitisha sana pale inapotokea Serikali kuwa ndio wa kwanza kuvunja sheria ambazo imejiwekea. Inasikitisha sana hasa pale taratibu na kanuni zinapovunjwa zinazohusu usalama na ustawi wa Taifa letu.

Tunazo sheria kuhusu uraia. Inasikitisha sana, ni namna gani Serikali hii ilivyotoa uraia kwa wakimbizi walioko katika makazi ya Katumba, Namishamo, sijui Bulianghulu, lakini inasikitisha sana. Utaratibu haukuatuwa, ada stahiki haikulipwa, sijui kwa sababu ya umasikini, sijui kwa sababu ya misaada tunayopewa na Kamisheni ya Umoja wa Mataifa ya Wakimbizi, tumelegeza masharti ya uraia, watu wamepewa uraia bila kuwepo na uhakiki wa kutosha. Ninazo taarifa kwamba baadhi ya hao wakimbizi waliopewa uraia

katika makazi ya Katumba mionganini mwao wako gerezani, wako waliofungwa, wako majangili hata wale wadhamini wa hao ambao walipewa fomu hawakuulizwa. Walichoambiwa ni kutia sahihi. Huu sio utaratibu mzuri, sio utawala bora na ni hatari kwa Taifa hili, hata katika eneo la kuwapa uraia watu ambao hatuna uhakika nao.

Mheshimiwa Spika, aidha, athari nyingine za kiusalama zinafahamika sana Serikalini, lakini nina hakika maadam tumeshawapa uraia wale jamaa Wazungu watakacha kuwahamisha wakimbizi hawa na itakuwa ni mzigoo juu ya Serikali hii ambayo ni masikini na tuna matatizo kadhaa. Sijui lakini. Hofu yangu kubwa ambayo nimeona niiseme ni juu ya utaratibu uliotumika wa kutoa uraia kwa wakimbizi. Sheria hazikufuatwa. Taratibu haikufuatwa na bahati mbaya sana hata hao wadhamini hawakupewa fursa ya kutoa maoni yao zaidi ya kuweka sahihi zao, huu sio utawala bora na ni hatari kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia angalau mawili, matatu kwenye hoja hii ya Wizara ya Katiba na Sheria. Kwanza kabisa, bado naendelea kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kipindi chote cha miaka mitano kuwepo hapa Bungeni. Lakini niwaombee sana wanawake wa Mkoa wa Singida kwa kuendelea pia kunipa imani na kunitia nguvu ya kuwatumikia.

Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mwanasheria Mkuu, lakini nimpongeze sana Jaji Mkuu ambaye yuko hapa, anaonesha uungwana wake wa kufika hapa Bungeni kuweza kushuhudia bajeti ya Wizara yake. Nampongeza sana. Lakini nawapongeza na Majaji wote walioko hapa, lakini niwapongeza zaidi Majaji wanawake. Ninasema wanawake tukaze buti, wakati ni wa kwetu sasa na mambo yatakwenda barabara, mtuwakilishe vizuri kwenye nafasi mlizoaminwiwa mkapewa na Mungu awasimamie na kuwabariki sana.

Mheshimiwa Spika, lakini mimi nataka uniruhusu niweze kumwonea huruma sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria kwa sababu mambo mengi ambayo yameombwa hapa na Wabunge wengi yanaashiria kwamba ni mzigoo mzito sana ambao anaupata. Lakini hivi karibuni tumepitisha bajeti kuu, tumeona kwamba Wizara hii imepewa pesa ndogo sana. Kwa hiyo, nataka nimwonee huruma sana kwa sababu sielewi atayatekeleza vipi. Hivyo basi, niendelee kuiomba Serikali iweze kuiangalia kwa jicho la huruma sana Wizara hii kwa sababu ina mambo mengi sana mbele yake ili iweze kuyatekeleza. Nashukuru kwa hatua za awali. Mahakama Kuu katika Mkoa wa Singida, naamini mambo yatakwenda vizuri. Naipongeza tu kwa mikakati yote iliyopo japokuwa bajeti inazidi kuwa ndogo mwaka hadi mwaka lakini mambo yatukuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudi hasa kwa kuwapongeza kwamba wanaendelea katika kurekebisha ile sheria ya ndoa na mirathi. Hivi karibu nilikuwa nimefanya ziara katika Kata ya Mgari, Wilaya ya Singida Vijiji. Nilikutana na mwanamke mjane ambaye ameteseka sana kwa muda mrefu, alikuja mbele yangu akilia kutokana na

kwamba sheria iliyopo haitendi haki kwa wanawake wajane pamoja na watoto yatima. Lakini bado naweza kusema kwamba hata hii iliyopo haijafanyiwa kazi ipasavyo, haijatekelezwa ipasavyo kwa sababu ukiangalia sheria inavyosema na mambo yanayotendeka kwa wanawake wajane wanaoachwa na waume zao pamoja na watoto yatima wanapata shida sana.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sheria hii iliyopo kabla ile haijaletwa, hebu na hii basi ifanyiwe kazi, iangaliwe kwa kina, itende haki, kwa sababu utakuta mwanamke labda amefiwa na mume wake wanaishi Mwanza, lakini yeye kwao ni Singida, mwanaume labda anatoka Rukwa. Basi pale kunakuwa na mchanganyiko kiasi kwamba watoto hawaelewii wafanye nini. Anapokwenda huku anaambiwa nenda huku, katika kufuutilia hata zile gharama za kufuutilia inakuwa bado ni mzigo mzito sana kwa mwanamke huyu na wengine wanaishia kukata tamaa, wanabaki wakiteseka. Watoto kama ilikuwa waende shule, basi hawaendi, ambao wame-*hold* mali hizo za Marehemu, basi wao wanaendelea kunufaika na familia zao. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana sheria hii pamoja na kwamba tunasema italetwa hapa Bungeni, lakini bado hata iliyopo tunaomba itende haki.

Mheshimiwa Spika, lakini bado hata katika masuala ya sheria ya ndoa, mimi naomba sana ndio maana nimesema Wizara hii iangaliwe kwa jicho la huruma, iongezewe pesa kwa sababu sheria ya ndoa bado haijapelekwa Vijijini. Wanawake walio wengi Vijijini, waliopo ndani ya ndoa hawajui haki zao. Unakuta mwanamke anateseka ndani ya ndoa, anatishiwa ukienda Mahakamani wewe ndio utanilipa mimi ukitaka kunipa talaka. Mwanamke anakaa anaanza kufikiria nitakwendaje sasa? Basi acha nifie hapa.

Ninaomba elimu hii ipelekwe Vijijini ili wanawake na watu wote waweze kujua haki zao, wajue sheria inasema nini. Lakini bado sheria hii ya ndoa wanapotengana na penyewe inakuwa ni patashika nguo kuchanika, basi ili mradi mwanaume ndio anakuwa amehodhi madaraka yote, unakuta mwanamke anaondoka kama alivyokuja, kwanza sio kama alivyokuja kwa sababu alivyokuja alikuja na vifaa, lakini wakati wa kuondoka anaweza akaondoka hata nguo hana, hata watoto hana. Sheria ya ndoa iliyopo sivyo inavyosema.

Mwanamke anapokwenda Mahakamani sheria hii inakuwa ya upande mmoja, inatetea upande mmoja kwa sababu mwenye nacho ndio ataongezewa kwa maana ya kwamba mwanaume sheria hii anainunua kwa kutumia rushwa, mwanamke anabaki akihangaiaka kwa sababu waathirika wako wengi. Waathirika tuko wengi, sheria inabaki inamlinda mwanaume kwa sababu ndio mwenye pesa.

Kwa hiyo, tunaomba sana sheria iliyopo ifuate mkondo wake. Sheria iliyopo itetee, itende haki kabla haijaja ile, maana tunadai sheria nyininge: Je, hii imefanya nini? Hii sheria iliyopo bado inaendelea kuwakandamiza wanawake pamoja na wanaume wengine wamekandamizwa pia na sheria hii maana tunapozungumza kuna wanawake wengine pia ni wababe, mwanaume naye anaondoka kama alivyoingia pale. Kwa hiyo, sheria hii iweze kutenda haki.

Mheshimiwa Spika, lakini bado nataka kusisitiza kwenye kupeleka elimu Vijijini. Elimu Vijijini maana yake kuna wanasheria wengine, mimi sielewi Mahakimu walioko Vijijini wanafanyaje kazi? Maana wewe kama Mbunge unapofika Kijijini ndio unatakiwa sasa ufanye kazi kama mwanasheria, ufanye kazi kama Jaji ili uweze kuwaamua watu ambao wanapingana katika masuala ya ndoa, wanapingana katika masuala ya mirathi, maana mwananke anapoingia pale anaambiwa wewe hukuja na kitu chochote, lakini ana haki mle ndani kwa sababu na yeye amefanya kazi, yeye ameshiriki katika kufanya kazi, yeye amelima. Kwa hiyo, naomba sana sheria hii Mheshimiwa Chikawe sheria ipelekwe Vijijini na elimu ipelekwe Vijijini.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka pia niombe Mahakama za Mwanzo ambazo Msemaji mmoja kutoka Mkoa wa Singida, dada yangu alikuwa amezitaja, lakini niongezee kwamba kuna Mahakama nyine za Mwanzo ambazo hazijafanya ukarabati. Ni Mahakama ya Mgandu pamoja na Mwamagemb. Baada ya kusema hayo, mimi sitakuwa na mengi sana, niwapongeze na niwatakie heri japokuwa bajeti ni ndogo lakini naamini kabisa mambo yenu yatakuwa ni mazuri kama mlivyofanya katika kipindi cha miaka mitano. Mimi ningeingia hapa, tulipoanza mpaka tulipofikia kwa kweli matunda yanaonekana, tunasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Kazi mliyofanya ni nzuri, hivyo mwendelee hivyo na sisi tutazidi kuwatetea, mtuombee huko tunakokwenda ili Mungu aweze kunyoosha mkono wake wa baraka tupate kurudi ndani ya Bunge. Ahsante sana. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. DR. JAMES A. MSEKELA: Mheshimiwa Spika, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Mathias Chikawe - Waziri wa Katiba na Sheria, pamoja na Watumishi wote katika Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya katika miaka hii mitano wakishirikiana kwa karibu na Idara ya Mahakama na Wadau mbalimbali nchini katika masuala ya kudumisha utawala wa sheria na kuimarisha utendaji wa haki kwa msingi wa Sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya vyombo vyahisilishi na Sheria na utoaji haki nchini bado vinahitaji kuboreshwa na kusogezwa karibu zaidi na wananchi. Bajeti ya Wizara hii haiwezi kumudu kasi ya ongezeko la idadi ya watu na kupanuka kwa makazi sehemu mbalimbali nchini. Serikali, kwa kushirikiana na wananchi, imekusanya uzoefu mzuri wa kupanua na kuboresha huduma za jamii kuitia mipango ya MMEM, MMES na sasa MMAM. Katika kutekeleza mipango hii, OWM TAMISEMI wamekuwa kiunganishi kizuri sana na kupelekea mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, ili tupate kasi nzuri hata katika kupanua na kusogezwa miundombinu ya vyombo vyahisilishi na Sheria na haki nchini, tujifunze kutoka katika mafanikio ya miundo na mipango niliyoitaja hapo awali ikiwa ni pamoja na utekelezaji ulivyofanyika kiasi cha kupelekea mafanikio yaliyopo. Pia changamoto zilizoonekana katika mipango ya MMEM, MMES na MMAM ikizingatiwa, tunaweza tukapata mpango mzuri sana na utakaotekelzeka tena kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, huduma za kisheria katika maeneo yetu, kama zinapatikana, basi ni katika ngazi ya Halmashauri tu na kidogo sana katika baadhi ya Tarafa. Haishangazi kuona *WEOs* na *VEOs* wao ndio wanajigeuza na kuchukua nafasi ya *ombuds* linalojitokeza kutokana na kutokuwepo kwa huduma za sheria na utekelezaji wa haki katika maeneo ya vijiji/vitongoji vyetu. Ni muhimu kuwa na *program* itakayokuwa shirikishi, hasa kwa masuala ya kupanua na kusogeza miundombinu ya sheria na haki huko vijjni hata kama kuna *NGOs* ambazo nazo nydingi huonekana kupwaya sana.

Mheshimiwa Spika, maisha ya Mkulima na Mfugaji sasa yanaongozwa na taratibu nydingi sana kwa mujibu wa sheria za nchi kuliko awali. Sababu zipo na ni muhimu sana hasa tunapojielekeza katika kuboresha kilimo, ufügaji, uvuvi, makazi na mambo mengine mengi kwa wananchi wetu walio wengi nchini, wale walioko vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, niipongeze Mahakama na hasa jopo la Majaji saba lililotoa maamuzi ya kihistoria hivi karibuni katika shauri la kuwepo ama kutokuwepo kwa mgombea binafsi.

Inafurahisha kuona kuwa sote tunatambua mipaka na misingi ya mipaka yetu ya kisheria kama ilivyo, huku tukiheshimu mgawanyo wa kazi wa mihimili ya dola tulivojivekea kwa mujibu wa Katiba yetu hapa nchini. Tunahitaji kuelewa siku zote kwamba, sheria kama ilivyo na kama tulivyo zitunga kwa urasmi wote, ndiyo barabara yetu rasmi ya mapito na siyo vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, nimalize kwa kuelezea matumaini yangu kwa kuendelea kuboresha kwa huduma za sheria na haki katika mwaka wa fedha 2010/2011 chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. CELINA O. KOMBANI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kutoa pongezi kwa Wizara hii kwa kufanya mabadiliko makubwa kuanzia ngazi ya Mahakama ya Mwanzo hadi ngazi ya juu. Naomba Wizara yako kama ilivyoboresha mishahara na marupurupu ya Wanasheria wengine wa Serikali yaani chini ya Wizara yako, waangalie na Wanasheria wa Wizara nydingine na wale Wanasheria wa Halmashauri muwaangalie pia hasa katika maboresho ya sekta ya Sheria.

Nawatakia kila la kheri na Mungu awabariki.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwashukuru sana kwa kukubali kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali Wilaya ya Nzega. Tayari Ofisi inafanyiwa marekebisho ya mwisho, ninaomba Watumishi wapelekwe mapema.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko la watu na matukio, nashauri Mahakama zenyé hadhi ya Wilaya zijengwe (hasa Nzega) kwani kwa sasa Mahakama ipo Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

MHE. MARIA I. HEWA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja na kuipongeza hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, Mahakama pamoja na kufanya kazi nzuri zina changamoto zifuatazo:-

Kuchelewesha malipo/posho za Wazee wa Mahakama. Taarifa hizi ni sahihi kwa sababu yalizungumzwa na wenyewe wahusikika Wazee wa Mahakama. Wazee hawa huchukua muda mrefu kulipwa, aidha, kulipwa nusunusu na pengine hakuna kabisa.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu uchakavu wa majengo. Tunampongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kujali wanawake katika uteuzi wake kwenye ngazi mbalimbali za uongozi wa juu mfano Majaji na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, Majaji hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu yakiwemo Majengo. Ombi langu ni kuyakarabati ili yaendane na heshima zao.

Mheshimiwa Spika, kupanga ni kuchagua lakini ombi langu ni kuchagua majengo kukarabatiwa kwa awamu na mambo mengine baadaye.

MHE. LUCY F. OWENYA: Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia hapa Tanzania kila baada ya Uchaguzi, Rais anayepata nafasi huwa anaunda Wizara kwa uamuzi wake. Hii inasababishia Taifa matumizi makubwa kwa kuwa na Baraza kubwa la Mawaziri. Nchi kubwa kama *America* ina Mawaziri 15 tu na kazi zinafanyika bila matatizo.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya kuangalia ni jambo gani Katiba ibadlishwe ili idadi ya Mawaziri ioneshwe katika Katiba ili pasiwepo na namba tofauti za Wizara kila baada ya uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tume ya Haki za Binadamu imekuwa ikifuatilia mambo mengi yahusuyo haki za binadamu kwa mfano, yale mauaji ya Serengeti na kadhalika, Tume hii haina meno ya kuchukua hatua zote zaidi ya kuyapeleka Serikalini ili yafanyiwe kazi. Hivyo inawavunja moyo sana waliopo katika Tume hii. Ni wakati muafaka sasa Tume hii kupewa fungu la kutosha kufanya kazi na wapewe nguvu ya kuweza kuwachukulia hatua wavunjaji haki kwa kuwapeleka Mahakamani moja kwa moja ili haki itendeke kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uhaba wa Mahakimu Tanzania: Je, Serikali haioni tija kuwaajiri wahitimu wa *Law School* ambao wengi wao baada ya kuhitimu wamekuwa wazururaji?

MHE. MWADINI A. JECHA: Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inasimamia pia Tume ya kurekebisha Sheria. Tume hii imeanzishwa kwa mujibu wa sheria iliyopitishwa na Bunge. Madhumuni ya Tume hii ni kuzipitia na kuziangalia kwa undani sheria zilizopo ili kuona kwamba bado zinafaa kuwepo au kwa sasa hazifai na kwamba zifutwe au kufanyiwa marekebisheso.

Mheshimiwa Spika, Tume hii imefanya kazi kubwa. Imeainisha Sheria ambazo zinaonekana kuwa na mapungufu, ama zimeonekana zinakandamiza. Aidha, imependekesa sheria ambazo zinafaa.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kuanzishwa kwa Tume hii ni jambo moja, lakini kuzifanya kazi ripoti zake ni jambo lingine. Kwa bahati mbaya sana yale madhumuni ya uanzishaji wa Tume hii bado hayajafikiwa kikamilifu. Hali hii inatokana na sababu kwamba ripoti za Tume hii ambazo zimetolewa miaka mingi iliyopita bado hazijafanyiwa kazi. Miiongoni mwa mifano hai ni ile sheria "*Delay of Disposal of Civil Suite*" ya mwaka 1986. Ni dhahiri kwamba kesi za namna hii huchelewa sana na baadhi ya wakati hata zikimalizika, basi hatua ya kukaza hukumu inachukuwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri Serikali iwe inazifanya kazi ripoti za Tume hii kwani kwa kufanya hivyo tutakuwa tunaimarisha utawala bora na haki za binadamu.

MHE. JANETH M. MASSABURI: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Katibu Mkuu, Jaji Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi chote cha miaka mitano, ni dhahiri mabadiliko makubwa na mazuri yameonekana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba Mahakama Kuu za Kanda ziimarishe ili kuweka mazingira mazuri ya kuharakisha kesi na pia itasaidia kupunguza mlundikano wa mahabusu katika Magereza yetu.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Mahakimu wawe na adhabu mbadala kwa kesi ndogo ndogo kwa kuhukumu adhabu za kifungo cha nje ambacho kitaambatana na usafi wa mazingira, kutumika kwa kulima mashamba, kupanda miti na kusimamia kwa kumwagilia miti hiyo. Kwa hatua hiyo, itasaidia sana kupunguza gharama kubwa ambayo Serikali inatumia kwa kulisha mahabusu hao chakula na matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwateua Majaji wengi katika kipindi cha miaka mitano ya utawala wake na pia kuongeza idadi kubwa ya Majaji wanawake.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Jaji Mkuu kwa maboresho makubwa katika Idara yake na kazi nzuri inayoendelea kufanywa.

MHE. DR. CHARLES MLINGWA: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na Wakuu wote chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri zinazozieleza katika hotuba ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuhakikishiwa kuwepo kwa bajeti ya kukamilisha ujenzi wa Jengo la Mahakama Kuu pale Shinyanga Mjini. Jengo hili limesimama kujengwa na hivyo kuanza kuwa kituo cha vibaka pale Mjini.

Mheshimiwa Spika, yawezekana fedha hizi zimetengwa kuitia *Vote 40, item 6314*, (ukurasa wa 65 wa Bajeti ya Maendeleo) ambapo kuna jumla ya shilingi bilioni 1.8. Naomba uhakikisho wa Mheshimiwa Waziri wakati anajibu hoja.

Mheshimiwa Spika, narudia kuunga mkono hoja. Ahsante.

MHE. IDDI M. AZZAN: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Katiba, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa jitihada kubwa wanazofanya kuboresha Mahakama na Utendaji mzima wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, naomba sana Wizara/Mahakama wachukue hatua za makusudi kumaliza mlundikano wa kesi katika Mahakama ya Rufaa, kesi ambazo ziko kwa muda mrefu na mpaka sasa hazijatolewa maamuzi na cha kushangaza zipo kesi za Rufaa za hivi karibuni zimetolewa uamuzi lakini zile za zamani hadi leo hazijatolewa maamuzi. Zipo kesi za Rufaa tangu mwaka 1997 hadi leo hazijatolewa maamuzi. Kuchelewa kutoa haki ni kutomtendea haki anayestahili.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba nimpe pongezi zangu za dhati Hakimu Mfawidhi wa Mkoa wa Pwani Ndugu Sekela Mwaiseje kwa jinsi anavyofanya kazi kwa umakini mkubwa na jinsi anavyopambana na uonevu unaofanywa na Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Mkoani Pwani. Mungu ambariki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE: Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii kumpongeza sana Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Mathias Chikawe kwa hotuba yake nzuri ya makadirio ya matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, pili, Wilaya ya Makete ilianzishwa mwaka 1979, hadi leo ni miaka yapata 31, Wilaya hii haina Mahakama ya Wilaya. Wananchi wa Makete wanalazimika kusafiri hadi Njombe ili kupata huduma hii. Kutoka Njombe hadi Makete ni umbali wa kilomita 110.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya tayari imekwishatenga eneo, lakini hadi sasa hakuna ujenzi unaoendelea katika eneo hili. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri

aelezee ni lini ujenzi wa Mahakama hii utaanza? Serikali ina Mikakati gani ili kuharakisha ujenzi huu?

Mheshimiwa Spika, Mahakama za mwanzo zilizopo Makete zinahitaji matengenezo. Toka zilipojengwa hazijapata kutengenezwa. Mahakimu pia hawatoshi na hii inasababisha ucheleweshaji wa haki kutolewa. Tunaomba Serikali iajiri Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo wa kutosha ili na Makete nayo ipate.

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inafahamu kuwa gharama katika Mabaraza ya Ardhi ni kubwa sana kiasi kwamba wananchi wengi wanashindwa kufungua kesi au kufuutilia haki zao? Mathalan kufungua shauri ni kati ya Sh. 10,000/= mpaka Sh. 20,000/= wakati kufungua *file* Mahakamani ni kama Sh. 1,500/= tu. Kwa maana hii, hata nia na lengo la kuanzisha Mabaraza haya inapoteza kabisa maana. Serikali inatoa kauli gani, hasa ikizingatiwa kuwa pale Baraza linapohamia kwenye eneo la ardhi ya mgogoro, walalamikaji na walalamikiwa ndio wanaolipa gharama ambazo mara nyingi ni zaidi ya Sh. 100,000/= kiasi kwamba Mabaraza haya sasa yamebaki ya matajiri.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itoe tamko bayana ili Mabaraza hayo kweli yawe mkombozi wa mwananchi kama yalivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mabaraza haya, baadhi ya wenyeviti wamekuwa “Miungu Watu”. Mfano ni Baraza la Karatu. Je, kwa kuwa muda wao kisheria umekwisha, kabra ya kuteuliwa, Serikali iko tayari kufanya uchunguzi wa kina wa maadili na mienendo yao ili haki za wananchi zisiendelee kunyongwa?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali Mahakama ya Wilaya ifunguliwe Wilayani Karatu katika jengo jipya, naomba kumpongeza yeye binafsi na Wizara yake kwa kusikia kilio cha wananchi wa Karatu ambao wameumia sana kwa kutokuwa na Mahakama ya Wilaya. Je, katika Bajeti hii ni fungu gani hasa limetengwa kwa ajili ya Mahakama mpya ya Wilaya ya Karatu ambayo bado inahitaji samani, nyenzo na bila shaka gari ili kumwezesha Mheshimiwa Hakimu atakayeteuliwa kufanya kazi yake vizuri?

Mheshimiwa Spika, je, ni lini sasa Hakimu atateuliwa na kupelekwa Karatu ili mahakama hiyo iweze kuanza kazi na kuwawezesha wananchi wa Karatu kupata haki zao kwa haraka?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006 Bunge la mwezi Januari - Februari niliuliza swali kuhusu uwezekano wa Serikali kuona Uchaguzi Mkuu wa Rais unafanyika siku iliyotumia kati ya wiki ambayo siyo ya ibada kwa madhehebu ya dini yanayotambulika hapa kwetu. Waziri wa Sheria wa wakati ule alijibu kuwa suala hilo litafanyiwa kazi sasa.

Kwa kuwa tarehe 31 Oktoba, 2010 iliyotangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi ni siku ya Jumapili ambayo ni siku waumini wengi wanaenda kusali na hivyo kuchelewa kwenda kwenye vituo vya kura jambo linalosababisha msongamano vituoni na pia kusababisha kura kuhesabiwa usiku sana. Je, ni kwa nini Serikali haikufanya kazi pendekozo hilo na kufanya siku ya katikati ya wiki na kuitangaza siku hiyo kuwa siku ya mapumziko kwa vile ni zoezi la kidemokrasia, linatokea mara moja tu katika miaka mitano na kuna nchi nydingi zinafanya hivyo.

Kwa kuwa katika siku za karibuni madhehebu karibu yote yametoa kauli kuitaka Serikali katikati ya wiki na kwa kuwa Serikali inaleta marekebisho ya sheria katika Bunge hili, ni kwa nini Serikali isisikilize kilio hicho cha Watanzania wengi na kama ni lazima kuleta marekebishi ya kisheria kama yatahitajika pamoja na marekebishi yaliyopangwa kuletwa katika Mkutano huu wa Bunge hili la Ishirini.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

MHE. DR. RAPHAEL CHEGENI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Sheria na Katiba, na nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuwasilisha bajeti yenyewe mwelekeo.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imewasilishwa kukiwa na hali ya changamoto nydingi kwa Wizara hii za kibajeti, kitu ambacho kinapelekea nitoe mapendekozo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama nydingi za Mwanzo hazina majengo maalum ya Mahakama na Mahakimu wa kutosha. Hii imepeleka shughuli za kimahakama kuendeshwa kwenye *magodown (store)* au maghala hivyo kutotoa ufanisi wa kisheria. Mfano Mahakama ya Mwanzo ya Mkula, Magu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kuna Wilaya nydingi ikiwemo ya Magu, hazina magari (gari) hivyo kupelekeea ugumu sana wa ki-utendaji ikiwemo ukaguzi wa shughuli za Mahakama. Naomba kuwepo na mpango, mkakati wa kuzipatia Wilaya zote usafiri ili utekelezaji wa shughuli za kimahakama ziweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, ukosefu wa *stationery* za kufanya kazi ni tatizo kubwa kwa baadhi ya Mahakama kwa kushindwa kufanya kazi kikamilifu.

Msheshimiwa Spika, nashuri, mafunzo yanayotolewa kwa ajili ya kazi hiyo iongezwe ili shughuli za kimahakama zianze kutolewa kiufanisi.

Mheshimiwa Spika, nashauri pawepo na uwezesho wa vitendea kazi kwa Mahakama hizi ili kuepusha vishawishi vya rushwa na pengine kutolewa kwa haki bila mizengwe.

Mheshimiwai Spika, rushwa ni ugonjwa mkubwa katika utendaji wa haki. Nashauri Serikali kupitia Wizara hii, iboreshe maslahi ya watumishi wa Mahakama na Mahakimu ili kuepusha ushawishi usio wa lazima na kupelekea kupo tosha haki kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. JUMA H. KILIMBAH: Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mathias Chikawe - Waziri wa Katiba na Sheria, Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, pia niwapongeze Jaji Mkuu - Mheshimiwa Augustino Ramadhani, Mwanasheria Mkuu wa Serikali - Mheshimiwa Jaji Werema, niwapongeze pia wakuu wote wa taasisi zinazohusu Wizara hii kwa kazi nzuri ya mara kwa mara inayohusu utoaji haki na sheria.

Mheshimiwa Spika, misingi ya sheria ni suala muhimu sana kwa wananchi kwani katika taratibu za uendeshaji, nchi inaendeshwa kwa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, bado inaendelea kusisitiza juu ya Katiba ya nchi. Kwa idadi kubwa ya wananchi nchini mwetu hawaijui vizuri Katiba ya nchi hii, inatokana na kukosa misingi mizuri ilioandalowi ili wananchi kuifahamu Katiba ya nchi yao.

Tatizo hili ni kubwa kuwa na wananchi wasioifahamu Katiba ya nchi yao. Ni makosa makubwa! Ni sawa na wanafunzi ndani ya darasa wasiojua maana ya uwepo wao darasani. Kwa hali hiyo, mwenye wajibu wa kuwafahamisha uwepo wao ni mwalimu anayewafundisha.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo basi, ni wajibu wa Serikali kutoa elimu ya kutosha juu ya Katiba ya nchi. Umuhimu huu utasaidia kujenga uzalendo miongoni mwa Watanzania hasa kwa nyakati za sasa wakati Tanzania imeingia katika ushirikiano wa kikanda ule wa Afrika Mashariki (*EAC*).

Mheshimiwa Spika, napendekeza Katiba ya nchi, maeneo muhimu yachapishwe kwenye vijarida vidogo vidogo na kusambazwa maeneo mbali mbali Vijijini ili wananchi wapate fursa za kuelewa baadhi ya mambo muhimu na hivyo suala la upotoshaji wa Katiba kuondoka kwani uzoefu unaonesha maeneo mengi. Upo upotoshaji kwa kuwa walio wengi katika maeneo hayo (wananchi) hawana uelewa wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, Tume ya kurekebisha sheria (*Law reform*) sheria nyingi zinazorekeblishwa na Tume hii bado hakujawekwa utaratibu wa kuorodhesha marekebishi hayo jambo ambalo mara nyingi matumizi ya sheria zilizopitwa na wakati kuendelea kutumika jambo ambalo mara nyingi linanyima haki au kupoteza misingi ya sheria kutoana na marekebishi kutokuwa bayana.

Mheshimiwa Spika, Mahakama eneo la kutoa haki, namshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Jakaya Mrisho Kikwete kwa uteuzi wa Majaji wa mara kwa mara. Tatizo lililopo ni uchache wa Mahakimu kwenye Mahakama za Mwanzo na Wilaya. Naomba Wilaya ya Iramba tuongezewe Hakimu wa Mahakama

ya Wilaya kwani Hakimu mmoja hatoshelezi kulingana na idadi ya kesi zilizopo Mahakamani.

Pia ongezeko la Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo. Sambamba na hilo, naomba Wizara ijenge Mahakama ya Wilaya ya Iramba kwani Mahakama inayotumika sasa ni jengo la Mahakama ya Mwanzo. Katika kufanya hivyo, suala la ucheleweshaji wa kesi halitakuwepo tena (msongamano wa majalada utapungua) hivyo msemo wa *Justice delay, justice denied* halitakuwepo tena.

Mheshimiwa Spika, naomba tamko la Serikali juu ya uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi. Mahakama hii ni muhimu kwa desturi ya itikadi ya Kiislamu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. CHARLES M. KAJEGE: Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Chikawe kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuhakikisha kuwa haki inatolewa kwa kila mwananchi bila upendeleo ama ubaguzi wowote, pia kwa ushirikiano wake mkubwa anaotupa kila tunapofika katika Wizara yake, kwa masuala ya kiofisi.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kutoa pongezi nyingi kwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Augustino Ramadhani na Mahakimu kwa ujumla kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya licha ya kukabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo mazingira yasiyo endelevu ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, ningependa kupata taarifa kuhusiana na maamuzi yaliyofanywa na Mwanasheria Mkuu wa Mwanza ya kumfutia mashitaka ya mauaji yanayomkabili Ndugu Mtesigwa Nyanguli. Ndugu Nyanguli anatuhumiwa yeye na wenzake kumuua Ndugu Ndalo tarehe 30 Juni, 2009, katika Kijiji cha Kibara, Jimbo la Mwibara, Bunda.

Mheshimiwa Spika, kulingana na ushahidi uliotolewa kwa maandishi katika Kituo cha Polisi cha Bunda, Ndugu Nyanguli ndiye aliemuua Ndugu Ndalo kwa kumpiga na jiwe kubwa kichwani. Pia ni yeye aliyemchukua Ndugu Ndalo kutoka nyumbani kwake na kumpeleka katika eneo la tukio.

Mheshimiwa Spika, wakati wa kuwakamata watuhumiwa, Ndugu Nyanguli alitoroka na kujificha kwa zaidi ya miezi tisa (Julai, 2009 – Machi, 2010). Pia, alipokuwa amekatwa na Polisi, vijana wengi walilizunguka gari la Polisi wakiwa na silaha mbalimbali na hivyo kuachiwa.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza ni kuwa Ndugu Nyanguli yuko mitaani akidai kuwa Polisi pamoja na Mwanasheria Mkuu wamemfutia mashitaka yote wakati hajawahi hata kufikishwa Mahakamani. Mheshimiwa Waziri atokapokuwa akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, jina la Marehemu, Ndugu Zacharia Msonge Ndalo na jina la Matuhumiwa ni Ndugu Mtesigwa Philemon Nyanguli.

MHE. SALIM HEMED KHAMIS: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayofanya ili kuielekeza nchi yetu iendeshwe kwa mujibu wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, naamini katika kutekeleza hayo, kuna changamoto nyingi ikiwemo ufinyu wa bajeti na ikifuatiwa na uhaba wa watendaji, Mahakimu na Majaji, uchakavu wa majengo na vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi, Serikali sasa imeondoa kabisa Mahakama ya Kadhi baada ya kuwa na kigugumizi kwa miaka mitano iliyopita. Pamoja na kuiondoa Mahakama ya Kadhi Serikalini ni budi ielewewe kuwa hayo ni matakwa ya Watanzania walio wengi na hata kama Serikali haiungi mkono. Bado tunaamini iko siku haki itatendeka.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutunga sheria nyingi hapa nchini. Tunaamini sheria hizo zinatungwa kwa ajili ya watu. Jambo la kusikitisha ni kuwa watu wengi hawazielewi sheria ambazo wanatakiwa wazitekeleze. Ingawa wanasheria wanasesma kutokujua sheria sio sababu ya kuvunja sheria, lakini hii sio njia ya kuwaonea Watanzania kuwashukumu bila ya kuwaelimisha kosa kabla ya kufanya kosa?

Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kongwe, imechakaa na ina viraka vingi sana. Hoja ya kuwa na Katiba mpya imejitokeza wakati wote sio tu kwa vyama vya upinzani, lakini hata kwa wale ambao hawana vyama. Haipendezi kuona kila mara Katiba yetu inachezewa chezewa kwa kutiwa viraka. Hata shati likiwa na viraka vingi linapoteza haiba yake.

Katiba hii iliyoandikwa wakati wa chama kimoja ni dhahiri kuwa haikidhi hali ya sasa ya vyama vingi. Lakini tuna mifano ya hivi karibuni ya hoja ya kuwa na mgombea binafsi. Pamoja na kuonekana haja ya kuwa na mgombea binafsi, lakini Katiba yetu inawataka wagombea wote wa nafasi ya kisiasa (Urais/Ubunge/Udiwani) wapitie vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, hapa Katiba yetu inamnyima Mtanzania ambaye hana chama cha siasa haki ya kuchaguliwa. Hili ni tatizo la kikatiba ambayo haikuwa na uono mpana wa mambo ya siasa za uchaguzi

Mhehsimiwa Spika, bado Mahakama zetu zinalalamikiwa ni vyanzo vya rushwa. Mtanzania mnyonge anakwenda Mahakamani kutafuta haki, lakini inapobidi kuwa haki hiyo lazima ainunue ni tatizo. Hivyo basi, Serikali ichukue hatua za kusafisha Mahakama zetu ili picha ya Mahakama zetu ipendeze.

MHE. JOEL N. BENDERA: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Wakurungenzi na watendaji mbalimbali wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayofanya lakini katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana hotuba kwani imesheheni mambo mengi ya kuleta mapinduzi ya kuendeleza mhimihi huu muhimu sana katika Taifa letu pamoja na mambo mazuri yaliyoandikwa katika hotuba, naomba kuchangia mambo ya msingi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, posho za wazee baraza, napendekeza ziongezwe na zipatikane kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, vitendea kazi duni jambo hili linalosikitisha sana, jambo hili lipatiwe uzito wa kipekee kwa kuhakikisha vitendea kazi vinapatikana, *uniform*, usafiri na nyumba za mahakimu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitoe pongezi kwa Korogwe Mjini kwa kujengewa Mahakama ya kisasa pale *Old Korogwe*. Mahakama hiyo imekamilika toka mwaka 2009 mwishoni. Ni zaidi ya mwaka sasa mahakama hiyo haijaanza kutumika, naomba kupata majibu leo. Kwanza ni lini mahakama hiyo itaanza kutumika na pili, ni sababu zipi za msingi zinazofanya mahakama hiyo kutofanya kazi?

Mheshimiwa Spika, wasiwasi wangu ni kwamba majengo sasa yanaanza kuharibika, aidha, kutotumika kwa mahakama hiyo ni kuleta msongamano katika mahakama ilioy MJINI Manundu. Naomba sana mahakama hiyo ianze kazi.

MHE. MAGDALENA H. SAKAYA: Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri na wataalamu wake wote kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Ardhi inafanya kazi zake kwa viwango vya chini sana! Kesi za ardhi ni nyingi sana na zikifika kwenye mahakama hii hazisikilizwi na kumalizika kwa muda. Kuna kesi ya mwaka 2003 ya wananchi wa Kata ya Kaliua – Urambo walibomolewa nyumba zao kwa madai kwamba wanapisha barabara kumbe ni shinikizo la wanasiaya, baada ya nyumba zao kubomolewa zimejengwa nyumba za viongozi fulani tena mwakilishi.

Kesi ya wananchi hawa ilifunguliwa mahakama ya Tabora mwaka 2003 kwa miaka mitano hadi mwaka 2009 haikuwahi kusikilizwa kwa madai kwamba Mahakimu wa Ardhi ni wachache, mwaka 2008 kesi ilihamishiwa Mahakama ya Ardhi Dar es Salaam hadi leo 2010 hajasikilizwa. Inasikitisha sana haki inatafutwa kwa muda wote huo hata tumaini hakuna, hata kesi 5250 zilizofika mahakamani kwa mwaka 2009/2010 ni kesi 1,109 tu zilizoshughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa pia ni Bajeti ndogo inayotolewa kwa Wizara hii ambayo haiendani na mahitaji halisi na umuhimu mkubwa wa kujali haki za utawala bora kwa Watanzania. Kiasi kilichotengwa kwa Fungu 90 kwa Wizara hii ni ndogo sana shilingi 1,618,701,000 hazitoshi chochote.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume hii ina majukumu makubwa sana ya kuangalia Haki za Binadamu nchi nzima ndilo jukumu lao. Wananchi wengi wanaonyimwa haki na utawala bora wako vijijini, vitendo vingi vya ukiukaji wa haki za binadamu ziko Wilayani, Tarafani, Katani na Vijiji. Tatizo kubwa kwa Tume hii upungufu wa wataalam kukosa vyombo vya usafiri na kukosa fungu la kuwawezesha kwenda vijiji kukaa na kufanya uchunguzi kwa malalamiko yanayofikishwa kwao.

Mheshimiwa Spika, Serikali iiwezeshe Tume hii kufanya kazi kwa ufanisi, hawawezi kushughulikia matatizo malalamiko wakiwa ofisini pale Dar es Salaam. Lazima watoke waende *site*, wafanye uchunguzi wa kutosha ili haki ipatikana Tume hii ni kimbilio la wanyonge.

Mheshimiwa Spika, pia Tume hii ifungue ofisi zao mikoani ili waweze kufikiwa kwa urahisi wananchi wengi wanateseka, suala la mauaji ya watoto wadogo wasio na hatia linalofanywa na watu wasiokuwa na maadili na wamekuwa wanyama halikubaliki na likemewe kwa nguvu zote ili kutoa fundisho na kuokoa watoto wetu kesi zote na mauaji ya watoto zipelekwe kwenye mahakama maalum ilishughulikia mauji ya *albino* ili ziendeshwe haraka sana na watuhumiwa washughulikiwe wa sheria, hapa Serikali ichukue maamuzi magumu ili kuokoa watoto kwani hawana mtetezi zaidi ya haki ipatikane, wahusika wote wanyongwe hadharani hii ndio dawa ya kutibu ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo kwa maeneo mengi uwezo ni mdogo kuweza kuendesha kesi kwa kasi na viwango, hakuna vitendea kazi, hakuna pesa za kuhudumia kesi za Watanzania. Ni aibu na imekuwa ni kawaida mtu anapopeleka mashaka yake *police either* kaibiwa au kavamiwa anaambiwa, analazimika atoe pesa, aweke mafuta kwenye gari ili mtuhumiwa akakamatwe kwa kipindi akiwa rumande amhudumie chakula kweli? Mtu anatafuta haki yake aliyonyang'anywa kwa gharama zake.

Mheshimiwa Spika, ikiwa huduma hizi za msingi zinazoangalia haki za wananchi hazitaboreshwu kuna dalili za amani tuliyonayo kupotea wananchi watachoka kuteseka, watachoka kusubiri haki kwa muda mrefu, watachoka kugharamia kutafuta haki yao, wataamua kuchukua sheria mkononi na hili ni hatari sana, dalili zinaonekana wananchi wanavamia vituo vya polisi, Mahakama na kadhalika, huko nyuma haya hayakuwepo.

Mheshimiwa Spika, imefikia hatua mtu anashtakiwa analazimika kulipa pesa ili *summons* ziweze kufikishwa kwa watuhumiwa, usipotoa pesa na kupeleka *summons* haipelekwi hivyo haiitiwi mahakamani kwa maana hiyo kesi haisogei, haisikilizwi. Tunajua hali ya wananchi wa vijiji kipato ni kidogo, hali ya maisha ni ngumu, ameonewa, ameibiwa, amevamiwa, amejeruhiwa na analazimika kutoa tena pesa ili mtuhumiwa ashughulikiwe, hapa haki haiwezi kupatikana hata siku moja na huyu maskini ataendelea kuumia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

MHE DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Mathias Chikawe, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote, walioshirikia kuandaa Bajeti vizuri nikiwa na imani taasisi zote zilizotengewa fedha zitatekeleza majukumu yao vyema kwa maslahi ya Watanzania wenye kero mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo mkoani Singida, naishukuru Serikali kuwa jitihada zake za kujenga Mahakama za Mwanzo Utmini na Iguguno pia kukarabati Mahakama za Ikungi, Ipembe na Shelui. Swali ni lini Mahakama ya Utmini itaanza kutumika kwani tangu imekamilika hadi sasa ni mwaka mzima, hivi Serikali itaweza kujenga majengo yenyе thamani kubwa halafu ishindwe kununua samani za majengo hayo?

Mheshimiwa Spika, ni kweli inasikitisha sana, naomba maelezo ya Serikali lini samani zitanunuliwa ili mahakama hiyo ianze kutumika?

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudhi hizo za Serikali za kukarabati au kujenga mahakama bado kuna mahakama nyingi mkoani Singida ambazo zina hali mbaya, zinahitaji ukarabati mkubwa, mfano Mahakama ya Mwanzo ya Manyoni Mjini, Mtinko, Mungaa na kadhalika. Ningependa kujua ni fedha kiasi gani zimetengwa kwa ajili ya kuendeleza kazi ya kukarabati Mahakama za Mwanzo mkoani Singida.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa mahakama za wilaya za mikoa wa Singida, napenda kuipongeza Serikali kwa kuwa huwa inasikia maombi ya wananchi wake pale wanapoona ni kero, hivyo napenda kuiarifu Serikali kuwa hivi inafahamu kuwa mkoa wa Singida hauna Mahakama za Wilaya? Endapo inajua, ina mpango gani wa kujenga Mahakama za Wilaya. Singida tulikuwa na wilaya tatu, sasa tuna wilaya tano.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Chikawe, Waziri mwenye dhamana awaeleze wananchi wa Singida huruma yake inasema nini ataanza na wilaya zipi ili tuwe na majengo ya mahakama ya wilaya yenyе tija.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Mahakama Kuu Singida, napenda nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dr. Mary Nagu kukubali kujenga Mahakama Kuu mkoani Singida alipokuwa Waziri mwenye dhamana, vilevile nimshukuru kaka yangu Mheshimiwa Mathias Chikawe alipopokea kijiti kutoka kwa Mheshimiwa Dr. Nagu aliendelea kuridhia ujenzi wa Mahakama Kuu mkoani Singida.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kutenga fedha za ujenzi wa Mahakama Kuu katika Bajeti hii ya mwaka 2010/2011 baada ya kukwama Bajeti iliyopita ya mwaka 2009/2010. Je, kwa ahadi ya Serikali kupitia Bajeti tumetengewa fedha kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, napenda kuikumbusha Serikali ombi langu la gari la mahakama ya mkoa kwani sasa ni miaka miwili mahamaka ya mkoa haina gari, hii ni

kwa miaka Mahakama ya Mkoa haina gari, hakimu ataratibu vipi mahakama za mwanzo na wilaya wakati gari la zamani liko juu ya mawe takribani miaka miwili?

Mheshimiwa Spika, nategemea majibu ya Serikali yene nia ya kurahisishia utendaji kazi wa Hakimu Mfawidhi wa Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Spika, Mahakama kuwa na mahabusu, napenda kuikumbusha Serikali kuwa Mahakama za Mwanzo za Mkoa wa Singida na wilaya hazina vyumba vya mahabusu suala ambalo ni tatizo kwani tunawapa kazi ngumu askari wetu kulinda watuhumiwa wanapoletwa mahakamani kwani huwekwa eneo la wazi wakati wakisubiri kutajwa kesi zao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ujenzi wa mahakama uende sambamba ya vyumba vya mahabusu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudzi za Serikali kusomesha Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo bado kuna upungufu mkubwa wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo mfano Ilongero, Mtinko, Mungaa na kadhalika hakuna mahakimu hutokea mahakama zingine suala ambalo linachelewesha sana kesi.

Mheshimiwa Spika, ni lini Serikali itatupa mahakimu kwa mahakama ambazo hazina mahakimu ili kesi zisichelewe na wananchi kuona kero?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Haki za Binadamu kufanya kazi mikoani, ninampongeza Mheshimiwa Japhet Sagasii kwa kazi nzuri anayofanya na watendaji wote katika kutoa elimu kwa jamii kujua haki zao pamoja na kusikiliza matatizo yao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kuwa kumekuwa na tatizo la kutenga fedha ndogo sana katika Tume hii suala ambalo linawafanya washindwe kwenda kutoa elimu juu ya haki za binadamu na kusikiliza matatizo ya wananchi huko waliko mikoani, hii itasaidia sana wananchi kuwa na uelewa juu ya haki mbalimbali za binadamu hususan wanawake.

Mheshimiwa Spika, suala la posho za wazee wa mahakama kuna tatizo, bado katika posho za wazee wa mahakama hasa utaratibu wa kulipwa posho hadi kesi anayoisikiliza iishe pia posho yenyewe ni ndogo sana. Naishauri Serikali kuweka kiwango cha posho kwa siku sio kwa kesi moja hadi imalizike.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kumaliza kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuongeza idadi ya Majaji wanawake, vilevile niwapongeze Majaji wanawake kwani wameonyesha uwezo mkubwa wa utendaji ndio sababu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete anawateua akiwemo dada yangu mpandwa Mheshimiwa Fatma Masengi ambaye uwezo ulionekana miaka yote ya utumishi wake nami siku moja nilimtabiria kuwa iko siku Mheshimiwa Rais atakuona.

Mheshimiwa Spika, sasa nitamke rasmi kuwa naunga mkono hoja hii nikiwa nasubiri ufanuzi wa Mheshimiwa Mathias Chikawe kwa maeneo yote niliyohitaji majibu ya Serikali.

MHE. KHADIJA S. AL-QASSMY: Mheshimiwa Spika, kwa uwezo wa Karima amenipa uzima leo hii na kuweza kuchangia hoja hii iliyoko mbele yetu ya Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, sina budi kukupongeza wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wote kwa umahiri wenu mkubwa kwa kuweza kuliendesha Bunge hili kwa viwango vikubwa Mungu awabariki.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kumpongeza Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa jinsi alivyowasilisha hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho na kwa umuhimu mkubwa napenda kumpongeza Waziri na watendaji wake wote kwa jinsi walivyoandaa hotuba hii ambayo ni nzuri, ninachoomba ni utekelezaji tu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada kubwa za Serikali bado mahakama nydingi nchini haziko katika hali nzuri, hali hii inawakatisha sana tamaa wafanyakazi kufanya kazi katika mazingira magumu, naiomba Serikali ijithahidi sana kuweka mazingira mazuri ili Mahakimu na Majaji wafanye kazi katika mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, Serikal inaleta sheria nydingi na Bunge kuzipitisha lakini la kusikitisha sheria hizo wananchi wengi hawazifahamu na kubakia kwenye makabrasha, kwa hiyo, naiomba Serikal itoe elimu ya kutosha ili wananchi wazifahamu sheria za nchi yao.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wanafanya makosa bila ya kufahamu kwamba wanatenda kosa kutokana na kutofahamu sheria hizo.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2009/2010, Waziri wakati wa kujibu alisema Katiba ya nchi inaweza kubadilishwa ikiwa watu wengi watapeleka malalamiko yao kwani kipindi hicho kilikuwa hajapokea lalamiko lolote ndio maana hakuna umuhimu wa kurekebisha Katiba.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki kuna wananchi wengi, vyama vya siasa na wanaharakati wengine wamefanya maandamano kuomba kurekebishiwa Katiba, je, leo hii anasemaje kuhusu jambo hili ambalo wananchi wengi wanalamika kuhusu Katiba hii? Naiomba Serikakli ione sasa kuwa kuna kila sababu ya kubadilisha Katiba hii ili iendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kusikia kuwa Mahakama ya Kadhi inashughulikiwa, lakini ikumbukwe kama sasa hivi ni miaka mitano bado mambo

yanashughulikiwa naiomba Serikali iharakishe shughuli hizi ili nae muislam apate miongozo yake. Nashukuru sana.

MHE. SAVELINA S. MWIJAGE: Mheshimiwa Spika, kwanza mimi napenda kupongeza kwa kujenga Mahakama Kuu Bukoba Mjini, ombi langu ni kuwa Bajeti hii itenye fedha za kuimaliza mahakama hiyo kuondokana na majengo yanayotumiwa, kwa sasa ni machafu, yameja popo, yamebomoka, mabovu hata mafaili yanakaa matatani, ni aibu, yako katikati ya mji, matatizo yaliyoko mkoa wa Kagera ubambikizwaji kesi unakuwa kama kasumba au kama sheria.

Mheshimiwa Spika, mtua anakuchukia na kuamua kukuzushia kesi na hila, nashukuru kesi kuzirudisha kwa wanasheria wa Serikali itapunguza rushwa, uonevu na chuki binafsi. Kuna matatizo kwenye Gereza la Bukoba mrundikano wa kesi unashangaza, watu wanamaliza miaka mitano hadi saba na zaidi.

Kuna Mahakimu ambao wamekuwa kero Bukoba, wananchi wanalamika sana sijawa na uhakika kwamba Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo kuna tabia mbaya sana pana nuka rushwa hasa tabia hii ya Mahakimu kuhamahama hasa katika Mahakama zilizoko vijijini mahakimu wanatoka Bukoba Mjini kila siku au kwa wiki mara moja inafanya mlimbikizo wa kesi au maisha ya mahakimu kuwa matatani kama hivi juzi hakimu alikatwa katwa mapanga.

Naiomba Wizara pamoja na Serikali kuwajengea nyumba huko huko kwenye Mahakama kulinda maisha yao kama Wizara inavyojuua. Mahakimu wamemaliza kutoa hukumu kwa mshitakiwa atakayeshindwa anakua na hasira hasa mahakama zifuatazo; Maruku, Katerero, Katoro, Katoma, Kalabagaine, Ibwera pamoja na nyingine na hizo ziko sehemu mbaya sana ambayo miundombinu sio mizuri, naomba Wizara iwaangalie kwa maisha yao na wananchi wapate haki sawa na kila mwaka huwa nachangia matatizo hayo sioni ufumbuzi, leo hii naomba nipate ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sheria ya Uchaguzi wananchi wengi hawajui mambo yaliyo kwenye sheria hiyo, naomba isambazwe ili watu wajue haki zao na sheria nyingi zimeandaliwa kwa lugha ya Kiingereza na wananchi wetu uelewa wao ni mdogo sana na kupata haki zao ni shida, ni lini Wizara hii sheria zinazohusu wananchi zisichapwe kwa Kiswahili ili wananchi wajue haki zao na hivi tunaelekeea kwenye Uchaguzi Mkuu wananchi wote waelewe na wasikilize sheria hiyo mapema kabla ya uchaguzi waondokane na unyanyasaji wakielewa sheria hawatanyanyawa sana.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa vijijini watakua wanaelewa sheria, naomba tabia ya mahakimu kukaa sehemu moja zaidi ya miaka miwili na zaidi inasababisha rushwa, sio kusema nahisi, mimi nimeshaona Bukoba mahakimu ambao wamekaa zaidi ya miaka mitano ndio wanaongoza kwa rushwa, hili ni ombi langu maalum.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, idadi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Kongwa ni ndogo sana, jambo hili liangaliwe. Mji wa Kibaigwa hauna Mahakama ya Mwanzo kuna

masuala mengi yanayohitaji ufumbuzi wa kimahakama pale Kibaigwa. Tunaomba Bajeti kwa suala hilo.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo za Zoissa, Mkoka, Pandambili, Mlali, Sagara na Kongwa zimechoka sana, panahitajika ukarabati mkubwa sana, tupeni Bajeti mwakani. Bunge na Mahakama kama nguzo zitengewe Bajeti kwa asilimia ya Bajeti ya nchi na wapewe kipaumbele ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko makubwa katika Gereza la Kongwa kutoka kwa mahabusu kwa kutopelekwa mahakamani siku za kesi zao kutajwa hasa wale wa Mpwapwa pia Wilaya ya Kongwa hatuna Baraza la Ardhi na Nyumba.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ijengwe nyumba japo tatu kwa Hakimu Mfawidhi wa Wilaya ya Kongwa na watumishi wa Mahakama. Wananchi wanalamikia sana tatizo la rushwa katika Mahakama za Mwanzo na Wilaya nchini, juhudzi za kipekee zifanyike kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. HEMED MOHAMED HEMED: Mheshimiwa Spika, kwa kuanza ni vyema nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia siku ya leo kufika Bungeni hali nikiwa mzima.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hotuba ya Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe kama ni mwelewa utafahamu Wizara ina wataalam waliobobeaa kwa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nchi yetu inakwenda kwa misingi ya sheria na inahitaji utawala bora, Serikali ni watu, ndani ya nchi yetu kuna tatizo kubwa juu ya elimu ya sheria kwa wananchi wetu. Jambo hili hupelekea wananchi hufanya makosa bila ya kujua, mara nyingi wananchi wanafahamu kosa kutokana na vitabu vya dini zao, lakini sheria za nchi yao hawazijui.

Mheshimiwa Spika, kuna sababu nyingi elimu kutowafikia ama lugha inayotumika Serikali itoe taaluma kwa wananchi ili wajue haki zao za kisheria.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mahakama zetu hali sio nzuri, majengo ya mahakama ni mabovu sana jambo ambalo hupelekea mahakimu kukosa imani ya kazi zao, kuwepo majengo ya watumishi wa Mahakama. Ni vizuri kumuandalia mazingira mazuri mfanyakazi ili awe na furaha katika kutenda kazi yake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu haki za binadamu, iko haja Serikali iwe na umakini katika kusimamia haki za wananchi wao (Haki za Binadamu) chombo hiki kinafanya kazi sana, lakini mawazo na fikra zinazotolewa na Tume hii Serikali zinazidharau.

Mheshimiwa Spika, Tume ilipendekeza kuanzishwa kwa mahakama maalum kama vile Mahakama ya Biashara, Ardhi na Kazi. Serikali inaelewa umuhimu wa

mahakama hizi lakini hadi hii mikoa iliidhinishwa ni mitatu tu. Je, Serikal inasema nini juu ya suala hilo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama ya Kadhi, nchi yetu imegawika watu wa kidini, kuna waislamu wengi ambao wanahitaji haki zao kwa dini yao. Kuna mambo kama ndoa ama mirathi, maeneo hayo kwa waislamu kila leo yanahitaji maamuzi ya kidini. Muislamu hakuanzishiwa sheria na nchi mambo mengi yamo ndani ya kitabu kitakatifu cha Mwenyezi Mungu (*Quran*). Serikali imedirika kuzuia haki kwa waislamu kuzuia Mahakama ya Kadhi nchini ni kumzuia muislam haki zake alizopewa na Mwenyezi Mungu baada ya maelezo yangu hayo nasema. Ahsante.

MHE.BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Kwanza kabisa napenda kumpongeaa Waziri wa Katiba na Sheria kwa kazi nzuri anayofanya hasa katika kuisimamia Wizara hii inayolinda haki za Watanzania, aidha, nawapongeza watendaji wote kwa jitihada zao zote za kudumisha haki kwa wananchi wa Taifa letu.

Pili naomba sana nipate maelezo ya uhakika juu ya Wazee wa Mabaraza wa Mahakama ya Mwanzo ya Mwanjelwa – Mbeya na Mahakama ya Mwanzo Mbeya Mjini. Wazee hawa wanaongozwa na Mzee Mwakyololo mpaka leo hawajalipwa stahili zao za kesi ambazo zimeshafanyiwa uamuzi takribani miaka miwili sasa. Je, nini chanzo cha ucheleweshwaji huu?

Pia ningetaka kujuu ni lini Serikali itamaliza tatizo la malipo ya wazee hawa wa mabaraza? Ni vyema Serikali ikaendelea kuwakopa wazee hawa. Nini mpango endelevu wa kuhakikisha Wazee wa Mabaraza wanalipwa kwa wakati.

Tatu, viwango wanavyolipwa Wazee wa Mabaraza kwa kila kesi ni kidogo sana, je, kuna mpango gani wa kuinua viwango hivyo ili wazee hawa waendelee kutenda haki zaidi bila kuwa na vishawishi vyovyote?

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

MHE. DEVOTA M. LIKOKOLA: Mheshimiwa Spika, napongeza Wizara na wafanyakazi wote kwa kuimarisha sekta ya sheria na kuleta haki kwa wananchi, naunga mkono hoja.

Natambua kuwa Wizara hii inashikilia mhimili wa tatu wa dola hivyo mafanikio ya awamu hii ni kutokana na mchango wa mhimili yote mitatu. Mahakama nyingi zimeboreshewa majengo, watumishi na vitendea kazi, aidha, bado kazi kubwa inatakiwa ifanyike.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mahakama iongeze kwani ofisi za mahakama nyingi bado zina Bajeti ndogo, Serikali pia iongeze Bajeti na utashi wa kutekeleza

mapendekezo ya Tume ya Haki za Binadamu. Tume hii ni jicho muhimu kwa Serikali, hivyo yale yanayoonekana basi ni vyema yafanyiwe kazi na Serikali.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikal kutoa tafsiri na mafunzo ya sheria mbalimbali hasa zile zinazowahusu sana wanawake na makundi maalum.

Mheshimiwa Spika, wanawake wengi wanahitaji kujua Sheria za Mirathi, Sheria za Ndoa, Sheria na Itifaki mbalimbali za kuzuia ukatili wa binadamu hususan ukatili kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Majaji na Mahakimu kwani wengi wanatoa mfano bora kwa maadili kimatendo yao, Mungu awabariki sana kweli wengi ni waadilifu. Ahsante.

MHE. CHARLES N. MWERA: Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kumpa nafasi. Pili, nawashukuru Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mathias Chikawe (Mb), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Jaji Frederick Mwita Werema na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Wizara haya yafuatayo:-

(1) Serikali iandae na kujenga majengo mbalimbali ya Mahakama hasa maeneo ya Vijiji ili majengo hayo yalingane na hadhi ya Mahakama. Haki ni muhimu itolewe kwenye jengo nzuri sio kwa majengo machakavu.

(2) Ni muhimu kuwa na Mahakama Maalumu inayoshughulikia masuala yanahusu rushwa. Tatizo kubwa ambalo tunalo Tanzania ni rushwa. Watumishi wanapenda kupokea rushwa na wananchi nao ni mabingwa wa kutoa rushwa. Elimu iendelee kutolewa kwa wananchi na katika shule pamoja na vyuo mbalimbali.

(3) Serikali iwe makini sana wakati inapoingia mikataba mbalimbali. Tuna Wanasheria wazuri wenye elimu ya kutosha, sifahamu ni kwa nini tunaingia kwenye mikataba ambayo haina manufaa kwa wananchi. Tuwe na watendaji (Wanasheria) wenye uzalendo.

(4) Uvunjaji wa haki za binadamu na misingi ya utawala bora, imekuwa ikiongezeka kwa kasi kubwa. Naomba kuishauri Serikali kushughulikia malalamiko hayo na kuyatolea maamuzi haraka ili wananchi wawe na imani na Serikali.

(5) Naomba Serikali iunde Tume ya kuchunguza idadi kubwa ya watuhumiwa wengi katika Magereza ya Tarime, kwa namna wananchi wengine walivyobambikiziwa kesi za mauuaji na watuhumiwa wengi wamekuwa rumande kwa muda mrefu sana. Kuna watahumiwa wamekuwa ndani zaidi ya miaka kumi (10). Nashauri Serikali ipange Majaji kusikiliza kesi hizi ili kumaliza msongamano.

(6) Naishauri Serikali kurekebisha mishahara ya Mahakimu wa Mwanzo, mishahara iongezwe ili pengine kuepuka Mahakimu hao kutopokea rushwa.

(7) Mahakimu wengi hupokea rushwa na kama Mahakimu wanapokea rushwa wakati Mahakama ndicho chombo cha kutoa haki: Je, ni chombo gani sasa kiundwe kama watendaji wa Mahakama wanaomba na kupokea rushwa? Nashauri Serikali wale watendaji washughulikiwe maana sheria ni msumeno na Mahakama ipewe fedha za kutosha ili kuweza kutekeleza majukumu yao.

(8) Haki itendeke bila upendeleo, bila kujali ubaguzi wa dini, ukabila na Vyama.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii. Mungu ibariki Tanzania.

MHE. DR. IBRAHIM S. MSABAHA: Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, pili, uboreshaji wa majengo ya Mahakama. Hali za Mahakama za Mwanzo katika Jimbo la Kibaha Vijijini, ni mbaya. Majengo mabovu, hayaendani na hadhi ya Mahakama kama chombo cha kutoa haki. Mahakama za Soga, Ruvu, Kwala, Magindu na Mlandizi, zote ziko katika hali mbaya. Huko Ruvu, Mahakama haifanyi kazi kabisa. Jengo la Mahakama limevunjika kabisa, kiasi kwamba Hakimu na wengineo, hawawezi kukaa kwa amani wakafanya kazi. Napendekeza sekta ya Mahakama iwekewe mpango kabambe wa kujenga upya majengo mabovu na kufundisha na kutawanya Mahakimu. Aidha, wakati umefika sasa kuanza kutayarisha Mahakimu wa ngazi ya Shahada kwa ajili ya Mahakama za Mwanzo. Aidha, hili likifanyika, Serikali iruhusu Mawakili kufanya kazi katika Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, tatu, kesi baina ya wakulima na wafugaji, kuna malalamiko hasa kutoka kwa wakulima kwenye Kata zenye jamii mbili za wafugaji na wakulima kuwa kesi za uharibifu wa mashamba, wakulima hawashindi. Malalamiko haya hasa yapo katika Kata ya Magindu. Kwa kuwa malalamiko haya ni mengi, ni bora Wizara/Idara ya Mahakama ichunguze na kufuatilia ili kujuu ukweli. Malalamiko haya yanaambatana na tuhuma za rushwa na ukiukwaji mwagine wa maadili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Naipongeza Wizara na Waziri kwa kazi nzuri na nawatakia kazi njema.

MHE. JOHN PAUL LWANJI: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dunia ya leo utawala bora ndiyo kigezo muhimu ambapo Serikali yoyote hupimwa na Jumuia ya Kimataifa, fedha zilizotengwa kwa Wizara hii ni kidogo mno. Hata Mheshimiwa Jaji Mkuu amenukuliwa akilalama kuhusu fedha kiduchu zinazotolewa/tengwa kwa mhimili wa tatu wa utawala. Napendekeza fedha za kutosha zitengwe kwa kila bajeti kwa ajili ya kazi muhimu za mhimili huu na kwa Mahakama zote nchini, ili zipambane na uhalifu na kuutokomeza na kuleta haki kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora iimarishe we kwa kupewa fedha za kutosha kadri inavyoomba. Kutokana na umaskini wa wananchi wetu, wanashindwa kumudu gharama za Mahakama ili kuendesha kesi zao na kupata

haki. *Quasi-Judicial bodies* kama hizi (Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora), zinarahisisha sana kazi ya kutafuta haki na imetokea kupendwa sana na wananchi kwa sababu hufanikiwa kupata haki mapema, pamoja na ushauri. Kuzikaba kwa kuzipa bajeti finyu, ni sawa na kuzizua zisifanye kazi kwa ufanisi kwa kushindwa kuwafikia wananchi walio wengi. Tume hii ina-compliment vizuri sana kazi na wajibu wa Mahakama. Nawapongeza sana timu nzima ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Wangewezeshwa vizuri, bila shaka wananchi wengi wangepata haki kwa wakati na kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009/2010 zilitengwa Shs.70m/= kwa ajili ya ukarabati wa Mahakama ya Mgandu (Ukimbu) na tuliahidiwa na Mkurugenzi wa Mahakama kwamba kazi ingeanza baadaye mwaka 2010. Mpaka sasa hakuna dalili ya ukarabati kuanza. Fedha hizi Shs.70m/= zimeishia wapi? Nini sasa kinafanyika?

Mheshimiwa Spika, mbali na Mahakama ya Mwanzo ya Mgandu, tulipata pia ahadi ya kukarabati Mahakama ya Mwanzo ya Mwamagembe. Nayu ahadi hiyo imeyeyuka. Mahakama mbili hizi zilikuwepo toka Ukoloni na zilisimama baada ya kukosa Mahakimu kwa zaidi ya miaka kumi (10), lakini sura ya Mahakama hizo ni mbaya sana, zote ni “completely dilapidated”. Dari zinaporomoka na kadhalika. Naishauri Serikali ichukue hatua za haraka kuzikarabati Mahakama hizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea Mahakimu wawili (2) wa Mahakama za Mwanzo za Ukimbu (Mgandu) na Mwamagembe, yule wa Itigi akastaafu. Sasa badala ya Mahakimu watatu (3) tuna wawili (2) tu wanaozunguka na wamepiga kambi Itigi badala ya vituo vya Ukimbu na Mwamagembe (wamepata sababu). Naomba Serikali ipeleke Hakimu Itigi.

MHE. JACOB D. SHIBILITI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Nianze kwa kumpongeza Waziri, Katibu Mkuu, Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu na Naibu Mwanasheria Mkuu kwa maandalizi ya hotuba yao nzuri iliyojaa changmoto nydingi, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kati ya Wizara zenye majukumu mazito lakini bado zinapata pesa/bajeti ndogo, ni pamoja na Wizara hii, kwetu sisi Wabunge tunashindwa kujua ni sababu zipi Serikali haiangalii Wizara hii yenye dhamana ya kusimamia haki. Bunge linatunga Sheria kama mhimili unavyosema na Mahakama ndiyo yenye dhamana ya kutafsiri Sheria hiyo pindi utekelezaji wa Sheria uletapo utata.

Mfano Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo hawatoshi na hata hao waliopo wanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Ofisi zao yaani majengo la Mahakama ni machakavu, hawana nyumba za kuishi, vitendea kazi vikiwemo vyombo vya usafiri, lakini kazi yao ni ya msingi kama ilivyo Shule za Msingi, ni kwa nini Serikali isiwe na mpango maalumu wa kuboresha Mahakama hizi?

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Misungwi inazo Mahakama za Mwanzo zenye majengo mabaya sana. Inonelwa ni moja ya Mahakama zilizo na hali mbaya sana.

Niiombe Serikali na Mahakama pamoja na uhaba wa fedha basi iangalie Mahakama hii katika bajeti yake hii.

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Wilaya ni sehemu ambayo pia imesahaulika sana. Wilaya ya Misungwi ni moja ya Wilaya zilizoanzishwa mwaka 1997 lakini bado haina jengo lenye hadhi. Sambamba na hilo, ni vyema tukashukuru kwa kuwa na Hakimu wa Wilaya lakini utendaji wa kazi wa Hakimu huyu, anafanya kazi katika mazingira magumu sana. Serikali itoe pesa za ujenzi wa ofisi inayoendana na hadhi ya Wilaya. Eneo la kujenga yaani *plot* ipo kilichobaki ni fedha za ujenzi kwa kufuata ramani za Mahakama. Naiomba sana Wizara iwatendee haki watumishi wa Mahakama ya Wilaya ya Misungwi kwa kuwajengea ofisi yao.

Mheshimiwa Spika, mishahara ya watumishi kuwa midogo, iliyozungukwa na matumizi yanayozidi mshahara, ni kukaribishwa kwa rushwa. Kuipiga vita rushwa ni pamoja na kuboresha mishahara kwa watumishi wote. Ni jambo la ajabu kuwalipa mishahara uliyo chini sana wakati ndio wasimamizi wakuu wa haki, si sahihi. Boresheni mishahara ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, Mawakili ni watumishi muhimu sana. Hawa ndiyo watumishi au Wanasheria ambao husaidia jamii kupata haki yao. Serikali iendelee kuwaajiri Wanasheria hao kadri Sheria za Ajira zinavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa matatizo yaliyo katika Wizara hii ni mengi na ufumbuzi wake ni fedha, Serikali katika bajeti yake ya mwaka 2011/2012, iweke kipaumbele katika Wizara hii iliyo nyuma sana. Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mwanasheria Mkuu, niwaombe sana katika vikao vyenu vya maandalizi ya bajeti, fanyeni juu chini bajeti ya Wizara yetu hii ijibu mahitaji ya umma wa Watanzania, Wizara iko nyuma sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ni vyema niunge mkono 100% ili hicho kidogo mllichopewa mkakitumie vizuri. Nawatakia kazi njema kwa utendaji wa umma.

MHE. MCH. DR. GETRUDE P. RWAKATARE: Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, kwa utendaji bora na maboresho mengi walijitahidi kuyafanya. Ningependa nitoe ushauri na mapendekezo ili kuimarisha majumuisho ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, kesi bado zinachelewa kutolewa hukumu. Jitihada zifanyike ili watu wasio na hatia wasikae mahabusu muda mrefu. Nashauri waajiri Mahakimu wengi na kuongeza idadi ya Majaji ili kesi zisikawie.

Mheshimiwa Spika, majengo mengi ya Mahakama za Mwanzo yako katika hali mbaya, mengine hayana vyoo. Jitihada zaidi zifanyike kukarabati majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, nashauri kuwe na Mahakama Maalum kwa makosa nyeti kama watoa rushwa au wala rushwa.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu waongezewe bajeti maana pia wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, pongezi kwa kazi nzuri mnayofanya, Mungu awabariki. Amini.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono, nampongeza Waziri kwa kuisimamia vizuri Wizara hii nyeti, yenye kutoa haki. Nawaomba wapigakura wake wamrudishe tena Bungeni ili tuendeleze gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri kwa kutoa pikipiki kama nilivyomuomba kwa Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Nyambiti. Lakini ipo ahadi ya siku nyingi ya ukarabati au ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo ya Nyamikoma Wilaya ya Kwimba tangu enzi za Waziri Mwapachu, akaja Mama Nagu na leo wewe Mheshimiwa Shikawe, hali ya jengo hilo si ya kuridhisha hata kidogo. Naomba ahadi hiyo itekelezwe. Lakini siku zote muungwana hutekeleza yale aliyoahidi.

Mheshimiwa Spika, najua kuwa nchi yetu ina upungufu wa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo. Naomba mara Mahakimu watakapopatikana, Wilaya ya Kwimba ipangiwe Mahakimu wa kutosha ili wananchi wanaosotea haki zao Mahakamani waweze kupatia suluhu zao.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kujua, ni kwa nini Mahakama Kuu ya Biashara iko Dar es Salaam peke yake na kwa nini isiwekwe kikanda yaani Mwanza na Mbeya ili kuondoa adha ya Majaji wanaolazimika kwenda Mikoani kusikiliza kesi hizo na wakati mwingine kucheleweshwa na kuwanyima haki ya kutendeka mapema "*Justice Delayed is Justice denied*". Kwani kuna tofauti gani kati ya kesi za nyumba na biashara ambapo imeamuriwa kesi zote za nyumba zisikilizwe na Jaji wa Mahakama Kuu, je, kwa nini kesi za biashara usitumike utaratibu kama huo wa kesi za nyumba?

Mheshimiwa Spika, yapo matukio mengi ya maamuzi ya Mahakama yanayopingana na Sera za Serikali hasa ilipojitokeza Mkuu wa Wilaya na Mkoa kusimamisha amri halali ya Mahakama. Mfano Mahakama ya Biashara iliamua Nyanza wahamishwe katika jengo lao kutokana na kesi ya *BP (TLD)*, ambapo ilimuriwa jengo liuzwe ili kufidia deni la mafuta. Mahakama Kuu ya Biashara ikatoa amri ya kumwomba *Court Broker* kuwatoa katika jengo hilo lakini baadaye ikatoka amri ya *Regional Commissioner* kusimamisha zoezi hilo na *Court Broker* yeoyote atakayetekeliza amri hiyo, atawekwa ndani. Nchi yetu katika ule utatu wa nguzo tujuavyo huwa haziingiliiani na siku zote amri za Mahakama haziingiliwi, je, kuingiliwa na watendaji wa Serikali tafsiri ya kisheria inasemaje?

Mheshimiwa Spika, mwisho, tunawashukuru Wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, kwa kuridhia baadhi ya Sheria zitumike kwa nchi zilizomo kwenye

Jumuiya. Naomba niulize, je, ni Sheria zipi zilizotiwa saini ili zitumike na Jumuiya lakini zitaanza kutumika lini hapa nchini? Tunaomba Serikali itoe elimu ya Sheria hizo kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

MHE. DR. MZERU O. NIBUKA: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wengine ambao wamehusika kwa namna moja au nyingine katika kuandaa bajeti hii ambayo imewasilishwa kwa makini na utulivu wa kutosha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, hongera saana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nitakuwa sijatenda haki kama sitachukua nafasi kuwapongeza wafuatao, Jaji Mkuu na wenzake, kwa changamoto wanazopambana nazo. Lakini pia nampongeza Jaji Werema (Mwanasheria Mkuu wa Serikali) na msaidizi wake Jaji Masaju, kwa utiifu na uaminifu wake kwa jinsi anavyotekeleza majukumu yake, nafikiri ni mfano wa kuigwa kwa Wanasheria wengine.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kujikita kwenye bajeti ya Wizara hii muhimu sana kwa kufafanua Sheria mbalimbali lakini pia kulinda na kutekeleza Sheria kama inavyopaswa, ni jukumu zito. Naomba kuishauri Serikali kwamba Wizara hii kwa umuhimu wake, ni vizuri kama bajeti yao itaboreshwa ili iweze kukidhi mahitaji ya Wizara hii angalau kwa kiasi cha kuridhisha, kwani tumeona watumishi wa Wizara wanashindwa kupata stahili zao ikiwa ni pamoja na nyumba za kulala, lakini maeneo ya kufanya kazi hayatoshi. Naomba nitoe mfano katika Jimbo langu la Morogoro Mjini, Mahakama ya Mkoa ni finyu mno, kiasi kwamba anapokuja Jaji kwa kesi za muuaji, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mkoa lazima ahame kwenye ofisi yake ili kumpisha Jaji, hii ni haki kweli? Hebu jaribuni sana kuliangalia jambo hili hasa kwa kuzingatia Morogoro ni njia panda, hii ni aibu kubwa sana. Hata Mahakimu wengine, lazima wapokezane wakati wa kuendesha kesi hizo, jambo ambalo linapunguza sana ufanisi, katika kuendesha kazi zao.

Mheshimiwa Spika, naomba kushauri pia Wizara iwaendeleze wale watumishi ambao wana uwezo wa kujiendeleza ili wakati wa uchujaji wasipambanishwe na wale wapya waliotoka vyuoni kwani kwa kufanya hivyo ni kuwanyima haki ya kupata nafasi hawa ambao wapo kazini kwa muda mrefu. Hivyo basi, makundi haya mawili yatenganishwe wakati wa udahili wao.

Mheshimiwa Spika, mwisho, pamoja na kazi nzuri sana zinazofanywa na Wanasheria hawa, lakini bado wapo wachache ambao hilitia doa bayaa sana Wizara hii. Wapo watumishi ambao sio waaminifu katika utunzaji fedha za umma. Pili, wapo wachache ambao hutoa siri za Mahakama kwa wadau kwa ajili ya visawishi vidogo vidogo. Lakini lililobaya zaidi ni pale Mwanasheria anapobatilisha Sheria kwa makusudi

kwa sababu ya adha ya rushwa au chuki binafsi. Hapa naomba viongozi wahusika waliangalie jambo hilo kwa macho mawili ili Wizara hii iwe na hadhi inayostahili.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa 100%.

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mwanasheria Mkuu, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Mabaraza ya Kata, Mfumo wa Sheria na haki unashuka hadi ngazi ya Mabaraza ya Kata. Katika mfumo wa uongozi wa Wizara na Mahakama, mara nyingi Mabaraza ya Kata hayapewi uzito unaostahili. Mara nyingi wanakuwa kama vile hawapo au kutambuliwa rasmi katika mfumo huo. Nashauri mtazamo wa mfumo huu uboreshwe ili Mabaraza ya Kata yapate hadhi zaidi kwa kuainishiwa majukumu yao na wapewe stahili za malipo (mishahara na posho) zinazostahili kwa mfumo bora wa ajira.

Mheshimiwa Spika, pili, ukarabati na ujenzi wa Mahakama na Mabaraza ya Kata. Ukarabati katika Wilaya ya Muheza bado unakwenda taratibu sana na hali ya majengo yaliyopo kule Kilulu, Kicheka, Ngomeni ni mbaya sana. Tulenge kuwa na ofisi za Mahakama za Mwanzo katika kila Tarafa, Tarafa ya Amani, Wilayani Muheza ambayo iko mbali zaidi ya kilomita 40, inastahili kuwa na jengo la Mahakama na Hakimu katika eneo la Tarafa hiyo.

Mheshimiwa Spika, tatu, ofisi za Mabaraza ya Kata zipo katika nyumba binafsi na ziko katika hali ya chini. Ulipaji wa kodi katika ofisi hizo hauna mpangilio na Serikali katika mfumo wake wa Sheria, hauwajibiki katika ulipaji wa kodi. Ni dhahiri ipo haja ya Serikali kutekeleza wajibu wake na hivyo kuboresha mfumo huu wa Sheria kwa kuelekeza nguvu kwa kujenga ofisi za Mabaraza ya Kata. Serikali lazima itambue kwamba kwa kuipatia Wizara hii fungu dogo la bajeti ya mwaka, ndio kikwazo cha kufanya sekta hii kubaki katika mfumo wa kizamani ambapo ni mfumo duni sana.

Mheshimiwa Spika, nne, usafiri, kutohana na upungufu wa Mahakimu, watendaji hulazimika kutoka eneo moja kwenda kutoa huduma mara moja au mara mbili kwa wiki katika Mahakama ndogo katika maeneo ya Kata. Hali duni ya usafiri inachangia katika kuhatarisha maisha ya watendaji hao wanaosimamia utoaji wa haki.

Mheshimiwa Spika, tano, uteuzi wa Majaji na kuongezeka kwa Mahakimu, Mheshimiwa Rais, Dr. Jakaya Mrisho Kikwete, anastahili pongezi nyingi kwa kuongeza uteuzi wa Majaji nchini na pia kuzingatia jinsia katika uteuzi wake. Kutohana na upungufu wa Mahakimu lazima Wizara ijenge mkakati maalumu wa kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo ili kuweza kuongeza idadi ya Mahakimu kukidhi mahitaji yanayoongezeka kwa kasi. Vijiji vimeongezeka na vitazidi kuongezeka, Kata zimeongezeka, Wilaya zimeongeka na Mikoa imeongezeka. Hii ni dhahiri kwamba

Mahakama katika ngazi zote hadi Mabaraza ya Kata zitaongezeka hivyo hivyo kwa lengo la kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Spika, sita, kumekuwa na utungaji wa sheria na zinapitishwa katika ngazi zote ikiwa ni pamoja na kutiwa saini na Mheshimiwa Rais, lakini Sheria nyingine bado hazijaanza kufanya kazi kwa zaidi ya miaka miwili kwa sababu “Kanuni” hazijakamilishwa. Je, Mheshimiwa Waziri anatoa kauli gani kuhusu mfumo huu unaochelewesha utekelezaji wa sheria zilizotungwa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. BERNADETA K. MUSHASHU: Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, kwa kuandaa hotuba nzuri inayokidhi haja. Nampongeza Mwanasheria Mkuu, kwa kazi nzuri anayofanya hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sasa tangu tuelezwe kuwa Serikali inafanya marekebisho ya sheria zinazomkandamiza mwanamke kama Sheria ya Ndoa na Mirathi. Je, ni kitu gani kigumu kiasi hicho ambacho kinafanya urekebishaji wa sheria hizi ushindikane?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuanzisha Divisheni ya Huduma za Kisheria kwa Umma (*Public Legal Service Division*) kwa ajili ya kuratibu utoaji huduma za ushauri wa kisheria kwa jamii ya watu wasio na uwezo wa kulipia huduma hizo. Ninafahamu kuwa kuna *NGOs* nydingi wameanzisha *Paralegals*, je, hizi *NGOs* zimeweka utaratibu gani wa kushirikiana na *Public Legal Service Division*?

Mheshimiwa Spika, gharama za kumlipa *Advocate* ni kubwa sana, watu hukosa haki zao kwa kukosa fedha za kugharimia *Advocate*, je, ni kitu gani kinasababisha gharama hizi kuwa juu sana? Kwa nini hakuna *Regulatory Authority* ya kuweka viwango vya gharama hizi?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kuanza kukarabati Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Katoma, Bukoba Vijijini, jengo la Mahakama linasikitisha, linatia aibu, ukiliona huwezi kuamini kuwa kuna kazi inaendelea pale ndani. Usalama wa wafanyakazi na watu wanaoingia mle ndani ya jengo uko hatarini, paa nusu limeanguka na Mheshimiwa Waziri wananchi wa Katoma, Bukoba Vijijini wanauliza, Mahakama hii itakarabatiwa katika bajeti hii?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

MHE. RUTH B. MSAFIRI: Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Nimevutiwa na staili ya uandishi wa kitabu cha bajeti, kina mpangilio mzuri. Aidha, nimefurahishwa na mtindo wa kujibu hoja za mwaka mzima kwa kuizingatia Ilani, hongereni sana, Mheshimiwa Waziri na wote waliomsaidia nawapongeza.

Mheshimiwa Spika, naendelea kuiomba Serikali iongeze kasi katika ujenzi wa Mahakama za Mwanzo nchini. Kwanza, ndilo eneo la mwanzo lililo karibu na mwananchi kulifika kimahakama. Likiwa na mazingira mazuri, eneo la Mahakama ya Mwanzo, naamini hata watendaji na watoa haki amba ni Mahakimu na wasaidizi wao watatulia kufanya kazi hii ya kutoa haki katika mazingira tulivu. Aidha, utaratibu wa kuwapeleka Mahakimu wenye Digrii ya Kwanza katika Mahakama za Mwanzo itafanikiwa sana.

Mahakimu wa Digrii ya Kwanza, ni wale amba wameishi na kusomea katika mazingira safi na salama kwa muda mrefu, kuwapeleka kufanya kazi katika mazingira magumu na mabovu na machafu (yalijoja majengo yenye nyufa na mavi ya popo), si kuwatendea haki. Haki izingatie pia mazingira bora kwa Watanzania bora hasa wataalam wanaoajiriwa. *Off course*, najua hii ni changamoto yetu wote, ila naamini inawezekana.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ijenje Mahakama ya Mwanzo Muhutwe, iliyoko Tarafa ya Izigo na Jimbo la Muleba Kaskazini, ukweli haifai. Ni mojawapo ya zile chakavu na mbovu zilizo ni makazi ya kudumu ya popo. Paa linavuja, mvua zikinyesha *session* huahirishwa ili majalada yasinyeshewe.

Mheshimiwa Spika, suala la kuzifanyia kazi ya kuzirekebisha Sheria za Mirathi na Sheria zote zinazowakandamiza wanawake lionezwe kasi. Wanandugu na jamaa wasiohusika wanawahi kujipenyeza kwa familia ya marehemu wa kiume na kujifanya wao ndio wasemaji wakuu badala ya marehemu kwa kuwa tu ni wanaume. Hali hii kwa vyovyote ni kandamizi kwa wanawake wajane na watoto wa marehemu hasa pale ambapo marehemu hakuacha wosia. Ugandamizaji huu unaumiza moyo hasa unapoonaa mali za familia ya marehemu zanafujwa na ndugu walio hai wakati familia ya marehemu inateseka. Watoto wananyimwa elimu, wananyimwa mali na mjane au wajane wananyimwa usemi, hii ni ukiukaji wa haki za binadamu. Naishauri Serikali iharakishe hatua hii.

Mheshimiwa Spika, nakipongeza CCM kwa kuona mbali na kuzingatia Katiba kwani masuala ya kidini vema wayashughulikie wenye imani, zile gharama za uendeshaji na mamlaka za uteuzi ziendelee kuwa zao wenywewe. Hii inaonyesha ukomavu wa CCM na uzoefu wa uendeshaji nchi kimaadili. Naipongeza tena CCM na naitakia mema, neema na ushindi mkubwa katika Uchaguzi Mkuu ujao wa Oktoba 2010.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautuwezeshi kupata zile dakika 40 za Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Katiba na Sheria. Kwa hiyo, hilo tutalifanya baadaye. Nimeombwa nisahihishe kwamba wale watoto pale wenye sare kama nyekundu hivi, sio chekechea, ni watoto wa *Sunday School* ya Kanisa la *Catheral Azania Front, Lutheran*. Karibuni sana, lakini hata kama sio chekechea, yale niliyowatakia mema yanabaki pale pale. Tunawatakia mema, ahsante sana.

Kwa hiyo, kwa shughuli zilizopangwa sasa zimefikia hapo. Basi nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa kumi na moja jioni.

(*Saa 6.45 Mchana Bunge lilisimamishwa
mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilipositisha shughuli za Bunge pale saa 7.00 mchana takribani saa 7.00 tulibaki na kuwasikilisha wawakilishi wa Serikai ili hatimaye Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu nadhani atapata yeye dakika 15 na Mheshimiwa Waziri dakika 25. Lakini kwa sasa kabla ya hao namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, aweze kutoa ufanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo yalizungumzwa asubuhi. Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuchangia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Katika mchango wa Mheshimiwa Said Arfi - Mbunge wa Mpanda Kati, alieleza kwamba uraia ulikuwa umetolewa kwa wananchi wa Burundi takribani 162,000 kiholela na kinyume na utaratibu na sheria za nchi hii.

Awali ya yote, kwanza ningependa kutoa angalizo muhimu sana kwamba suala la kutoa uraia kwa mkupuo kama tulivyota huu haukuwa mara ya kwanza kwa Serikali yetu.

Mwaka 1978 Baba wa Taifa - Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitoa uraia kwa wakimbizi takribani 36,000 kutoka Rwanda waliokuwa wanaishi kwenye makazi ya Mwose, Wilayani Mpanda na Kimuli, Wilayani Karagwe. Kumekuwepo na sababu maalum ambayo sisi imelazimu Serikali kufikia maamuzi ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, msingi wa kutoa uraia mwaka huu 2010 kwa wakimbizi 162,156 kutoka Burundi wanaoishi kwenye makambi ya Katumba na Mishamo, Wilayani Mpanda na Ulyankhulu Wilayani Urambo umetokana na sababu tatu za msingi.

Moja, nchi yetu imeridhia Sheria za Kimataifa za Wakimbizi ikiwemo ile ya *Geneva Convention* ya mwaka 1951 ambayo inatutaka kama Taifa kushiriki katika mchakato wa kutafuta suluhisho la kudumu kwa tatizo la wakimbizi walioishi nchini kwa muda mrefu bila kuwa na matarajio ya kurudia kwao.

Pili, wakimbizi hao wamekuwepo nchini kwa takribani miongo minne bila suluhisho la kudumu la tatizo la ukimbizi wao.

Tatu, asilimia 80 wamezaliwa Tanzania kulingana na sensa ya mwaka 2007 na wamekuwa wakiiona Tanzania kama nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sababu hizi za msingi, Serikali yetu iliamua kushirikiana na jumuiya ya kimataifa kutafuta suluhisho la kudumu la wakimbizi hawa mwaka 1972.

Mheshimiwa Spika, tarehe 15 Juni, 2007, Kamati ya Nje, Ulinzi na Usalama na Baraza wa Mawaziri ilimwagiza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kutafuta suluhisho la kudumu kwa wakimbizi hawa. Katika sensa iliyoofanyika mwezi Oktoba, 2007 ilibaini kuwepo wakimbizi 218,000 katika makambi ya Katumba, Mshamo na Ulyankhulu. Aidha, matokeo ya sensa yalionyesha kuwa asilimia 79 waliomba wapewe fursa ya kuomba uraia ya kuomba uraia wa Tanzania wakati asilimia 21 waliomba kurudi kwenye nchi yao ya asili, yaani Burundi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupatikana kwa matokeo ya sensa, Kamati ya *NUU* ilipendekeza kwa Mheshimiwa Rais kuwa wakimbizi walioonyesha nia ya kuomba uraia wa Tanzania waruhusiwe kuomba uraia kwa mujibu wa Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 na taratibu zake. Aidha, Kamati ya *NUU* ilielekeza Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kufanya utaratibu wa kuwarudisha makwao wakimbizi walioomba kurudi kwao.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais aliridhia pendekezo la Kamati ya *NUU* la kutoa uraia kwa wakimbizi wa mwaka 1972 kutoka Burundi. Lakini akasisitiza kwamba baada ya kupewa uraia, raia hao wapya wahamishiwe kwenye maeneo mengine yasiyokuwa na mazingira ya ukimbizi.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa kuomba uraia kwa wakimbizi hao wa mwaka 1972 ulianza rasmi Mei, 2008 kwa kufuata Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 na taratibu zake zote. Hakuna Sheria wala taratibu zilizokiukwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria Na. 6(viii) ya Uraia ya Tanzania ya mwaka 1995, mtu ye yeyote asiyeha raia wa Tanzania anaweza kupata uraia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa njia ya tanijisi, yaani *naturalization*. Kifungu cha 9(i) cha Sheria hiyo ya Uraia kinamtaka mtu ye yeyote anayeomba uraia wa Tanzania kupeleka maombi yake kwa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya uraia ambaye kwa sasa ni Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, kifungu 23 cha Sheria hiyo kinamatka kwamba Waziri hatawajibika kutoa sababu yoyote ya kukubali au kukataa ombi lolote kwa mujibu wa Sheria hii na uamuzi wa Waziri kuhusu ombi lolote hautakuwa na rufaa au kuhojiwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, maombi ya uraia wa wakimbizi wa makazi ya Ulyankhulu, Tabora, Mishamo na Katumba Mkoani Rukwa yalifuata taratibu zote za kuomba uraia kwa kujadiliwa kwenye vikao vya Ulinzi na Usalama za Wilaya na Mikoa. Maoni yalidhaminiwa na Wakuu husika wa makambi hayo ambao ni Maafisa wa Serikali wanaoaminiwa na ambao wapo karibu na wakimbizi hao na hivyo kuwafahamu vizuri. Kwa kufuata utaratibu huo, jumla ya maombi 164,312 yalipokelewa ambapo maombi yaliyokubaliwa ni 162,156. Jumla ya maombi 2,152 yalikataliwa. Hawa wakiwemo

watu ambao walikuwa wanahisiwa kujihusisha na ujambazi na kadhalika. Kwa mantiki hiyo, hakuna mhalifu au mfungwa aliyepewa uraia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, ni vema kutambua kuwa katika Sheria ya Uraia na Kanuni zake hakuna kipengele kinachomtaka Waziri kutumia utaratibu huu kwa kupitia Wilaya au Mkoa. Mamlaka yote ya kutoa au kutokutoa uraia amepewa Waziri mwenye dhamana ya masuala ya uraia. Utaratibu huu uliwekwa na Waziri mwenyewe katika kushirikisha ngazi mbalimbali za Serikali kwenye suala hili nyeti la kutoa uraia kwa wageni ili kuwachuja wale wote wasiofaa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kuhusu malipo ya ada, Waziri anayo mamlaka kisheria kwa mujibu wa Kanuni 16(iii) ya Uraia ya mwaka 1997 kumpungumzia au kumsamehe mwombaji yeoyote kulipa ada.

Katika maombi haya ya wakimbizi Waziri wa Mamlaka alipunguza ada kutokana na uwezo mdogo wa kifedha wa wakimbizi hao na ilibidi fedha hizo zilipwe na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani *UNHCR*, badala ya kulipa fedha taslimu, Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani kwa makubaliano na Wizara lilikubali kutoa vitendea kazi kwa Wizara hususan magari ambayo yanahitajika katika vyombo mbalimbali za dola vilivyo chini ya Wizara hii. Takribani magari 200 yalitolewa na kugawanywa kwa vyombo hivyo.

Kwa mfano, katika Wilaya ambapo anatoka Mheshimiwa Mbunge, Wilaya ya Mpanda imepatiwa *Land Rover STK 8183* la Uhamiaji ambalo limefika kule wiki iliyopita. Vile vile katika mwezi Agosti mwaka huu gari moja *Toyota Land Cruiser FFU* itapokelewa na magari mengine mawili, pia yatapokelewa kwa ajili ya matumizi ya Mkoa huo.

Mwisho, napenda kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla kwamba kwa mujibu wa kifungu 15 cha Sheria ya Uraia, Waziri anayo mamlaka ya kuwaondolea haki ya uraia, mtu yoyote aliyepata uraia kwa tajinisi iwapo itadhihirika kwamba hana manufaa kwa Taifa letu au anahatarisha usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tofauti pekee ambayo imejitokeza katika utoaji wa uraia kwa wananchi hawa ni uharaka ambao umetumika na hii imetokana na kwamba kwa sasa hivi *Citizenship Processing Unit* ambayo ipo pale Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ina mtandao wa kompyuta na hatujafanya hii kazi *manually* kama ilivyokuwa zamani.

Mheshimiwa Spika, kimsingi tofauti ni kwamba Wizara imefanya kazi kwa ari zaidi, nguvu zaidi na kasi zaidi. Naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

SPIKA: Ahsante sana, ila tu naona Waziri amesahau kupeleka gari Ulyankulu, sijui yote manne yanakwenda Mpanda! Ooh, lakini ukitaja Mpanda ni hatari. Basi tafadhali namwita sasa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Anazo dakika zake 15. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI: Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote 43 waliochangia hotuba hii kwa maandishi na kwa kusema. Sitawataja majina, lakini Waziri atawataja. Aidha, nampongeza Waziri wa Katiba na Sheria kwa uwasilishaji wake murua wa hotuba na kwa kutuongoza sisi vyema katika mambo ya Sera yanayogusa Wizara yetu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kukushukuru wewe kwa umahiri wako katika kufanya maamuzi. Nafasi hiyo inahitaji uamuzi wa haraka bila kuyumbishwa na kazi hiyo ngumu umeifanya vizuri sana. Ninakutakia kila la kheri katika kuomba ridhaa ya wananchi wa Urambo ili ifikapo tarehe 30 Oktoba, 2010 saa 12.00 jioni ufanikishe azma tena ya kuwa Mbunge wao. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba bajeti hii ni ndogo sana kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema. Lakini sisi tunaamini kwamba kikombe kilicho nusu ni kikombe kilichojaa nusu. Au kwa Kiingereza *the half empty cup is also half full*. Kwa hiyo, tunategemea kwamba hizo fedha kidogo tunazoziomba hapa mkishatupatia tutazitumia ile *half full* kufanya mambo ambayo tutaweza kuyafanya.

Mheshimiwa Spika, ninafahamu kwamba huu ni mwaka wa uchaguzi na ninawatachia Waheshimiwa Wabunge wote kheri na wote wale ambao wanataka kutumia haki yao ya kuomba uongozi katika ngazi hiyo, nawatachia kila la kheri. Tusiitane majina kwa sababu Katiba yetu inaheshimika kwa njia hiyo. Baada ya kusema hayo, naomba sasa nirudi katika michango ya Waheshimiwa Wabunge. Ni wengi wametoa michango yao, lakini ningeanza kwanza na Mheshimiwa Fatuma Mussa Maghimbi, Msemaji au Waziri Kivuli wa Kambi ya Upinzani.

Mchango wake ni mzuri sana na ninafahamu kwamba yeye ni mdau mkubwa katika sekta hii na amesema mambo ambayo pengine ni vizuri tubadilishane naye mawazo. Kwanza kuna moja amesema la uchapaji wa Katiba ile ya Kiingereza. Kwa kweli ni ukweli kwamba hili jambo tuliligundua zamani na tulipoligundua mara moja tulimwandikia Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na nahakikisha kwamba nakala zitakazotoka safari ya pili hazitakuwa na makosa ya uchapaji ambayo yamo kwenye nakala zilizopita. Kosa hilo halikutokana na Ofisi yangu, isipokuwa ilitokana na uchapaji.

Mheshimiwa Maghimbi pia amezungumzia kuhusu Tume za Haki za Binadamu na Utawala Bora. Ninaomba kuungana naye kwa msingi kwamba Tume hii ambayo imeundwa Kikatiba ni lazima iruhusiwe kufanya kazi zake kwa mujibu wa Katiba na kwa mujibu wa Sheria. Serikali iko makini kwenye hilo na siamini kwamba Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inakwazwa na Serikali isipokuwa pale ambapo bajeti inakuwa ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo uamuzi wa Tume siyo wa mwisho katika utoaji wa haki. Kama Tume itafanya maamuzi ambayo Serikali hairidhiki nayo, upo utaratibu ambao umeainishwa kikatiba na sisi Serikali tunaweza kutumia nafasi hiyo kwenda kwenye chombo ambacho kina mamlaka ya mwisho katika maamuzi, yaani Mahakama. Katiba yenye inaturuhusu kufanya hivyo.

Hoja yake ya pili kwamba taarifa za Tume hazifanyi kazi ya Kurekebisha Sheria. Mimi nadhani hilo Mheshimiwa Mbunge hatutendei haki, kwani ukurasa wa 14 wa hotuba yake, ye ye mwenyewe ametaja sheria nne na anafahamu kwamba ziko nyingi ambazo tayari zimeletwa Bungeni hapa na zikapitishwa kama Sheria. Mara tu baada ya kuteuliwa kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kazi yangu ya kwanza ilikuwa ni kusoma taarifa hizo kuanzia mwaka 1986 mpaka sasa na nitaendelea kuitumia Tume kufanya kazi katika mambo mengine ambayo ni muhimu na kila itakapobidi tutaleta mapendekezo ya kutungwa Sheria mpya au kurekebisha Sheria zilizopo. (*Makof*)

Mheshimiwa Maghimbi pia amezungumzia suala la mgawanyiko wa Mawakili wa Serikali na Maafisa wa Sheria. Ninaomba kulizungumzia suala hili kwa ufupi. Suala hili linahusu miundo ya Idara za Serikali ambalo kwa kweli liko chini ya mamlaka ya Rais anayesimamia muhimili huo wa *Executive* na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Iko chini ya utaratibu huo.

Lakini hata hivyo sio vizuri kulinganisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Tanzania Bara na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwani sisi hapa Ofisi za Mikoani za Mwanasheria Mkuu wa Serikali haziendeshi mambo ya mashitaka peke yake, bali pia zinaendesha mambo ya kesi za daawa yaani *civil cases* na mambo mengine kwa mfano kushughulikia malalamiko ya wananchi ambayo yanaletwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Kwa hiyo, tofauti ipo kubwa sana na ukifanya kama walivyofanya Zanzibar pamoja na udogo wao utafanya kazi nyingine ya kuongeza gharama ya uendeshaji wa Serikali. Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Fatuma Maghimbi kwamba Ofisi ya *DPP* haiingiliwi kwa aina yoyote na Mwanasheria Mkuu wa Serikali isipokuwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashitaka ni Idara moja kati ya Idara nne ambazo ziko chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na hii haiwanyimi uhuru watendaji wake wa kazi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala lingine la sungusungu. Naomba tena kurudia kwamba suala la utoaji wa haki halipo katika chombo chochote ambacho hakikutamkwa kwa mujibu wa Sheria na chombo ambacho kina mamlaka ya utoaji wa haki ni Mahakama. Sungusungu au wasalama na vikundi vyta aina hiyo viliingizwa katika Sheria ya Mgambu kwa mujibu wa Sheria Na.9 ya mwaka 1989 na wakapewa mamlaka ya kukamata kuhusiana na mkesi za jinai.

Mamlaka yao yanaishia hapo tu na haitakuwa vyema kuwapa sungusungu au wanaussalama, mamlaka zaidi ya hayo. Naomba kusisitiza kwamba sungusungu wafanye kazi kwa mujibu wa sheria hiyo na madaraka yao sio kuhukumu. Madaraka yao ni kukamata wahalifu na wawakamate vizuri, wasiwatendee kama ni watu ambao tayari wamehukumiwa.

Mhweshimiwa Spika, kulikuwa na swali lingine la Mheshimiwa Charles Mwera, ameiomba Serikali kama inaweza kufanya uchunguzi kuhusiana na watuhumiwa

wanaobambikizwa kesi za mauwaji Tarime. Tunapokea ushauri wake na tutafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, suala lake la pili lilikuwa ni kuwapa uwezo mawakili wa Serikali, kuandaa mikataba. Kama ilivyosemwa hapo mwanzoni na Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake, hii ni kazi ambayo tunaendelea kuifanya na ninadhani tunaifanya kwa nguvu sana sasa hivi kuwa-*expose* Mawakili katika maeneo ambayo ni mapya pamoja na maeneo ya zamani.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salim wa Chambani, alizungumzia kuhusu Mgombea Binafsi.

Mheshimiwa Spika, suala hili limeamuliwa hivi karibuni na Mahakama ya Rufani, na ninaona kuna mazungumzo mengi kulihusu. Mimi ninashauri kwamba, tusome ile hukumu ya Mahakama na wakati utakapofika Waheshimiwa Wabunge wakiona ni muafaka, basi hoja iletwe hapa Bungeni, itaamuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na maslahi ya wanasheria wa Tume ya Kurekebisha Sheria, timesikia ushauri wa Mheshimiwa Maghimbi, tutayafikiria. Kuhusiana na kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali anazuia maoni ya Tume ya Haki za Binadamu, kama vile ripoti ya Nyamumo na mengineyo, kwa kweli sio kweli. Hatuwezi kufanya hivyo. Tukifanya hivyo, upo utaratibu wa kisheria wa kutushughulikia sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi sina kingine zaidi cha kusema, isipokuwa tu kuwaomba kwamba mtupe hizi fedha, pamoja na udogo wake ili tuweze kufanya kazi. Kwa sababu tunaamini kwamba kikombe kilicho nusu ni kikombe kilichojaa nusu pia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kufika muda huu. Aidha, nakushukuru wewe binafsi kwa umahiri wako wa kusimamia kwa uzuri mjadala na pia kwa kunipa fursa hii ya kuhitimisha hoja yangu niliyoitoa leo asubuhi, kwa kutoa maelezo kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza na yaliyozungumziwa na Waheshimiwa Wabunge.

Kwa kuzingatia kuwa Waheshimiwa Wabunge ni wawakilishi wa wananchi, ni wazi kuwa yote walioyasema hapa wameyasema kwa niaba ya wananchi wanaowawakilisha na hivyo na mimi nitakuwa ninawajibu wananchi ambaa ndio wote tunawawakilisha hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu hoja mbalimbali, ni vyema niwatambue wote waliochangia ambaa wapo katika makundi makubwa mawili. Kwanza, wapo wale waliochangia kwa kuzungumza humu Bungeni na wapo wale waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni ni hawa wafuatao:- Mheshimiwa George Lubeleje - Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Fatma Maghimbi - Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Ernest Mabina - Mbunge wa Geita, Mheshimiwa Janet Mbene - Mbunge wa Kuteuliwa, Mheshimiwa John Shibuda - Mbunge wa Maswa, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro - Mbunge wa Kiteto, Mheshimiwa Diana Chilolo - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Martha Mlata - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Said Arfi - Mbunge wa Mpanda Kati, Lawrence Kego Masha - Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na hatimaye Mheshimiwa Jaji Frederick Werema - Mwanasheria Mkuu wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Dr. Wilbroad Slaa Mbunge wa Karatu, mara mbili; Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha – Mbunge wa Kibaha Vijijini, Mheshimiwa Devota Likokola - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa John Paul Lwanji - Mbunge wa Manyoni Magharibi, Mheshimiwa Lucas Selelii - Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Jacob Shibiliti - Mbunge wa Misungwi, Mheshimiwa Savelina Mwijage - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Charles Kajege - Mbunge wa Mwibara na Mheshimiwa Juma Killimbah - Mbunge wa Iramba Magharibi. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Richard M. Ndassa - Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Janeth Massaburi - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. James Msekela - Mbunge wa Tabora Kaskazini, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni - Mbunge wa Busega, Mheshimiwa Lucy Owenya - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Omar Nibuka - Mbunge wa Morogoro Mjini, Mheshimiwa Dr. Getrude Rwakatare - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Maria Hewa - Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Captain John Chiligati - Mbunge wa Manyoni Mashariki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Mwadini Jecha - Mbunge wa Wete, Mheshimiwa Benson Mpesya - Mbunge wa Mbeya Mjini, Mheshimiwa Celina Kombani - Mbunge wa Ulanga Mashariki, Mheshimiwa Khadija S. Ally Al-Qassmy - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa - Mbunge wa Shinyanga Mjini, Mheshimiwa Charles Mwera - Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Job Ndugai - Mbunge wa Kongwa, Mheshimiwa Ruth Msafiri - Mbunge wa Muleba Kaskazini, Mheshimiwa Diana Chilolo - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Hemed M. Hemed - Mbunge wa Chonga na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge - Mbunge wa Makete.

Wengine ni Mheshimiwa Magdalena Sakaya - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Idd M. Azzan - Mbunge wa Kinondoni, Mheshimiwa Joel Bendera - Mbunge wa Korogwe Mjini, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis - Mbunge wa Viti Maalum na hatimaye Mheshimiwa Herbert Mntangi - Mbunge wa Muheza. (*Makofi*)

Kama wapo Wabunge ambao sikuwataja kwa kuwasahau, basi naomba niletewe majina yao, nitawatamka hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja yangu. Kimsingi, wametoa michango mizuri sana yenye lengo la kuimarisha utekelezaji wa majukumu katika Wizara yangu. Hii inaonesha ni kwa namna

gani Waheshimiwa Wabunge, wapo tayari kutoa michango ya kimawazo kwa minajili ya kuendeleza sekta hii muhimu ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, michango ambayo Waheshimiwa Wabunge wameitoa ni mingi na ni wazi kuwa kwa muda huu ambao ninao sio rahisi kutoa maelezo na kujibu hoja zote zilizotolewa. Nieleze tu kuwa michango yote iliyotolewa tunaithamini sana tena sana na kwamba tutaifanyia kazi kikamilifu. Kama ilivyo ada, tutawaandalia majibu ya hoja zote kwa kina na tutawasambazia Waheshimiwa Wabunge kabrasha lenye majibu hayo kabla hawajaondoka kutoka katika kikao hiki.

Katika kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, ni vyema nikaanza kwa kujibu hoja za jumla kwanza ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge, pamoja na Kambi ya Upinzani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na kuheshimu sana umuhimu wa muhimili wa Mahakama katika kujenga Taifa imara kijamii, kisiasa na kiuchumi. Mahakama ina jukumu kubwa katika kukuza na kulinda demokrasia katika jamii inayostaarabika kama ya kwetu hapa nchini. Kwa kutambua ukweli huo, siku zote Serikali imekuwa ikiheshimu na kulinda uhuru wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu mazito ya Mahakama, muhimili huo umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo Waheshimiwa Wabunge katika michango yao wameeleza kwa kina. Baadhi ya changamoto hizo ni ufinyu wa bajeti, upungufu wa majengo ya Mahakama na idadi ndogo ya Mahakimu na Majaji.

Kama nilivyoleze Bunge lako Tukufu katika hotuba yangu, Serikali inalitambua tatizo la upungufu wa majengo ya Mahakama na idadi ndogo ya watumishi wa Mahakama wakiwemo Majaji. Hivyo basi, Serikali imekuwa ikichukua hatua madhubuti na za makusudi za kuongeza idadi ya watumishi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, tuliajiri Mahakimu 126 wa Mahakama za Mwanzo, Mahakimu 53 na kuteuwa Majaji wa Mahakama Kuu 20, kujaza nafasi zilizoachwa wazi na Majaji ambao walistaafu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2010/2011 Serikali inakusudia kuajiri Mahakimu 150. Labda pia nichukue nafasi hii kutambua mchango wa Eng. Stella Manyanya, ambaye kwa bahati mbaya nilimsahau, ninauthamini sana mchango wake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya leo asubuhi, Serikali kwa kushirikiana na progarmu ya maboresho ya sekta ya sheria, imeendelea kujenga Mahakama na kukarabati Mahakama zilizopo kwa kadiri ya uwezo wa fedha ulivyoruhusu. Mathalani katika mwaka ujao wa fedha, jumla ya Mahakama 20 za Mwanzo, zitajengwa na ujenzi wa Mahakama Kuu Shinyanga, utakamilishwa. Hii inadhihirisha nia ya dhati ya Serikali ya kukabiliana na uhaba wa watumishi pamoja na kuongeza idadi ya majengo ya Mahakama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko ya ucheleweshaji wa kesi Mahakamani. Ucheleweshaji huu kwa kiasi kikubwa umechangiwa na uhaba wa Majaji na Mahakimu, mazingira ya upelelezi na upungufu wa vitendea kazi na miundombinu duni.

Kwa kutambua tatizo hilo, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali ili kutatua tatizo hilo. Mojawapo ya hatua hizo kama nilivyokwishaeleza ni kuendelea kuongeza idadi ya Majaji, Mahakimu, Mawakili wa Serikali na Watumishi wengine. Aidha, kupitia programu ya maboresho ya sekta ya sheria, wapelelezi wa Jeshi la Polisi wamekuwa wakipatiwa mafunzo katika medani ya upelelezi ili kuimarisha uwezo wao na hivyo kuharakisha upelelezi.

Kadhalika, programu hiyo imekuwa ikitoa kwa Jeshi la Polisi, vifaa mbalimbali, kama pikipiki na vyombo vyta mawasiliano, kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa upelelezi. Katika ngazi ya Mikoa na Wilaya, kumekuwa na vikao vyta kusukuma kesi ambavyo huchangia kwa kiasi kikubwa kupunguza mlundikano wa kesi katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali imekubali kuanzishwa kwa Mfuko wa Mahakama, yaani *Judiciary Fund*, kama ilivyo kwa mhimiili wa Bunge. Mchakato wa kuanzishwa mfuko huu unaendelea kama nilivyooleza katika hotuba yangu. Kimsingi tunakubaliana na maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu rai kwa Serikali, iongeze kasi ya mchakato wa kuanzisha mfuko huu.

Hivi ninavyozungumza *Cabinet Paper* iko tayari na tunakusudia ifikishwe *Cabinet*, ipitishwe halafu baadaye katika Bunge la Mwezi wa Nne, tulete Sheria ya Kuanzisha Mfuko huu, ambayo basi katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha, mwaka 2011/2012, suala hili litazingatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijaribu kuzungumzia hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge, hasa kwa kuwataja majina na hoja walizozisema. Kuna hoja moja ambayo imezungumzwa na Wabunge wengi sana ambayo ni kuhusu ujenzi, ukarabati na umaliziaji wa majengo ya Mahakama.

Waliochangia hoja hii ni pamoja na Mheshimiwa Shibili - Mbunge wa Misungwi, Mheshimiwa Dr. Msabaha, Mbunge wa Kibaha, Mheshimiwa Selelili - Mbunge wa Nzega, Mheshimiwa Dr. Charles Mlingwa - Mbunge wa Shinyanga Mjini, Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge - Mbunge wa Makete, Mheshimiwa Dr. Getrude Lwakatare - Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Capt. John Chiligati - Mbunge wa Manyoni, Mheshimiwa Savelina Mwijage – Mbunge wa Viti Maalum na Mheshimiwa Ndugai - Mbunge wa Kongwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua ukubwa wa tatizo la miundombinu ya Mahakama za Mwanzo za Wilaya na za Kanda. Kihistoria, Mahakama za Mwanzo zilikuwa ni Mahakama ambazo zilikuwa zinaitwa *Native Courts*. Kwa hiyo, hata majengo yao yalikuwa yamejengwa na zile Serikali za Mitaa. Sasa baada ya Serikali kuanzisha Mfumo wa Mahakama mwaka 1963 ambao tunao sasa, Mahakama zile zikahamia Serikali Kuu na mpaka sasa ziko Serikali Kuu.

Lakini kama nilivyosema, tunajitahidi na tunawaomba hasa Halmashauri zetu ziweke kama ni mkakati katika bajeti zao na katika mipango yao, kujenga angalau Mahakama moja ya Mwanzo na nyumba ya Hakimu, kila mwaka. Tuamini wanafanya vizuri katika ujenzi wa shule, wanafanya vizuri katika ujenzi wa Zahanati, lakini bado hawajaanza kuchangia katika ujenzi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ni Wizara yangu na Mahakama peke yake ndio tunaohangaika kuzijenga Mahakama hizi. Bado uwezo wetu ni mdogo, lakini kama Halmashauri zitakubali kuchangia kujenga Mahakama hizi, nadhani suala la kuwa na Mahakama mbovu au zisizofaa litakwisha. Sasa hivi tuna Mahakama 1,050 za Mwanzo na katika hizo ni Mahakama 250 tu ambazo ndio kidogo ukiingia unasema umeingia Mahakamani. Sasa hili sio jambo zuri. Kwa mwendo huu kama tukiiachia tu Mahakama ndio ifanye kazi hii, basi itachukua miaka mingi sana ili tupate Mahakama ambazo zinaridhisha.

Kwa upande wake, Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba tunajenga Mahakama Kuu katika kila Mkoa, kama tulivyolahidi. Leo asubuhi nimesema tutajenga katika Mkoa wa Singida, Mara na Mtwara, kama tulivyosema na mwaka huu wa fedha tutaanza ujenzi wa Mahakama hizo.

Mheshimiwa Spika, lingine kubwa lililosemwa ni kuhusu ajira za Mahakimu na hili limesemwa na wengi kidogo. Lakini ni kweli kwamba kutokana na ongezeko kubwa sana la idadi ya watu kwa kasi, ni dhahiri kwamba uhalifu pia umeongezeka. Wahalifu wamekuwa wengi na sisi Mahakimu hawajaongezeka kwa kiwango ambacho tunataka. Tumekuwa tukiajiri Mahakimu kila mwaka, lakini bado hawatoshi, sasa ndio maana tumefikia hatua kwamba angalau katika Mahakama za Mwanzo, tuanze na utaratibu wa kupeleka Mahakimu ambao wana shahada ya kwanza. Hawa tunao wengi kwa sasa.

Kila mwaka kuna Vyuo Vikuu 10 ambavyo vinatoa wanasheria na hawa wanakuwa wengi. Kwa hiyo, sasa nasema Idara Kuu ya Utumishi ikishatutengenezea muundo stahili, ambapo tunadhani watamaliza kazi hiyo mapema, basi utaratibu huu utaanza.

Mheshimiwa Spika, tukianza utaratibu huu tutaanza katika sehemu za Mijini, halafu baadaye kidogo kidogo kwa jinsi tunavyojenga Mahakama zetu nzuri kule Vijijini, tutawapeleka Mahakimu hawa amba ni *Graduates* na tunadhani kwanza itafanya mambo mawili, itaondoa tatizo la upungufu wa Mahakimu kwa sababu Mahakimu tutakuwanao, lakini pia itauboresha utoaji wa haki na hasa katika sera nzima ya uwakilishi. Maana atakapokaa Hakimu *Graduate*, pale pia tunategemea atakwenda Wakili kutetea na atakwenda Mwanasheria wa Serikali kuendesha kesi hizo.

Mheshimiwa Spika, lingine lililozungumzwa, sio kubwa sana, lakini ni kubwa, nalo ni posho za Wazee wa Baraza kwamba zinachelewa kufika.

Mheshimiwa Spika, hizi zinatolewa kulingana tu na *OC* inavyokwenda. Mwaka huu tumezipandisha na tumezibajeti kutoka Sh. 1,500/= kwa kesi mpaka Sh. 5,000/=. Ni asilimia kubwa sana kwa kupanda, lakini bado tunajua kiwango hiki nacho sio kikubwa sana. Tutakachofanya ni kujitahidi kuhakikisha kwamba pesa hizi zinawafikia wazee hawa kwa wakati. Ndio maana kila tunapopeleka pesa kwenye Kanda zetu, tunahakikisha kwamba *first charge* iwe angalau basi ni kwa kulipa posho hizi za Wazee wa Baraza ili waendelee kutoa msaada ambaa wanautoa katika kutafuta haki katika Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, lingine kubwa lililozungumzwa na karibu watu wengine wote ni kwamba kuna ufinyu wa bajeti, kwamba bajeti ya Wizara hii na ya sekta nzima kwa kweli ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, mimi ninakubaliana kwamba ni bajeti ndogo, lakini kama alivyozungumza Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tukiwa *positive*, basi tutaona kwamba ni glasi imejaa nusu na tukiwa *negative*, basi tutasema glasi hii iko tupu nusu. Kwa hiyo, tuwe *positive* na tuseme glasi imejaa nusu. Hiki tulichokipata kwa mwaka huu, tukitumie vizuri.

Ninazo ahadi nyingi kwamba tutaiangalia tena bajeti hii katika *mid year review*, mwezi Januari na pia kuna mpango wa Serikali kuitizama upya na kui-*revamp* kabisa bajeti ya sekta ya sheria katika mwaka ujao wa fedha. Kwa sababu, tumeona umuhimu wa sekta hii, huu ni muhimili muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa John Shibuda alitoa hoja mbili. Moja, alizungumzia kuhusu umri wa Majaji kustaifu.

Mheshimiwa Spika, nataka tu kueleza kwamba jambo hili na sisi tumelifikiria, kwa kweli ukiangalia katika eneo hili la Afrika Mashariki na Kati, sisi labda ndio Majaji wetu wanastaifu wakiwa vijana sana, miaka 65. Kenya nafikiri ni miaka 70, Uganda ni miaka 72. Kwa hiyo, sisi tulikuwa tunaangalia tufanyeje angalau tufike kwenye *average* ya wenzenzu ili basi tulingane lingane katika sekta hii. (*Makofsi*)

Ni kweli kwamba jinsi watu wanavyokaa katika kazi zao, ndio jinsi wanavyozidi kuzimudu, zile sheria, sasa badala ya kutizama vitabu zinakuwa zinamtoka tu kwa sababu

keshazoea sana. Tunategemea basi Serikali tutakapolipeleka jambo hili kwa wenzetu tutaliangalia vizuri na pengine tutafanya mabadiliko katika muda ambao sio mrefu kuanzia sasa.

Mheshimiwa Shibuda pia alikuwa ameeleza matatizo ya upatikanaji wa haki kule kwake Maswa na akaniomba kweli aliwahi kuniomba niende na mimi niliahidi kwenda lakini aliniomba wakati huu ambao Mheshimiwa Spika mwenyewe unaelewa si rahisi sana lakini nimewaelekeza watendaji. Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali na *DDP* wenyewe wataondoka mara tu baada ya Bajeti hii kama mtaipitisha, ikishapita wataondoka waende huko Maswa wakaangalie matatizo hayo na wayatolee maamuzi hapo hapo Maswa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Janet Mbene, alitoa mchango mzuri sana na mimi nauheshimu kama nilivyokuwa namheshimu yeye mwenyewe, siku zote ameeleza kwamba kulikuwa na uelewa mdogo wa masuala ya haki za binadamu kwa watendaji wa Serikali wenyewe yaani ndani ya Serikali wale watendaji wenyewe hawaelewi haki za binadamu na ndiyo maana wamekuwa wakizivunja na kuzifinyanga.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema Tume ya Haki za Binadamu imejitahidi sana kutengeneza jukumu lake hasa kwa kutoa elimu kwa umma na imetoa elimu kuhusu utawala bora kwa maafisa watendaji wa ngazi za kata na vijiji, maana kule ndiyo hasa haki hizi zinafinyangwa. Wamefanya kampeni kuhusu haki za watu wenyе ulemavu wa ngozi katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa na mauaji ya wanawake na uchunaji ngozi, wamefanya kampeni hizi, wamefanya semina, wamefanya mikutano ya hadhara ili kuelimisha wananchi kuhusu madhara ya vitendo vyao hasa katika imani zao hizi za kuwachuna wenzao ngozi.

Mheshimiwa Spika, mikutano wa wadau mbalimbali kujadili utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Binadamu na watu wenyе ulemavu wamefanya mikutano hii na wameshirikisha wadau mbalimbali ili wapate uelewa angalau basi tujaribu kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, elimu kuhusu haki za binadamu imetolewa kwenye jeshi la polisi katika utekelezaji wa kazi zao na nimesema katika hotuba yangu kwamba tumetoa elimu kwa polisi wenyewe na wakufunzi wao ili waendelee kila mara kukumbushana na kuwaeleza polisi kuhusu haki za binadamu katika utendaji wao wa kazi. Pia tumetoa elimu kwa Magereza 53 Tanzania Bara.

Mheshimiwa Fatma Maghimbi, pia Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, walizungumzia kuhusu ripoti hii ya Tume ya Kurekebisha Sheria ambayo inaitwa *Delay of Disposal Civil Suit 1996* hii ilikuwa ripoti ya mwanzo kabisa na iliandikwa na Marehemu Jaji Mwakasendo kama kumbukumbu zangu ziko sawa. Lakini kuitia ripoti hii Serikali imeshakufanya mabadiliko mengi sana, Serikali ilibadilisha mwaka 1986 Sheria ya Mwenendo wa Madai (*CPS*) ilibadilishwa imefanyiwa marekebisho, hapo hapo tuka-introduce ule utaratibu wa *ADR* yaani *Alternative Dispute Resolution Mechanism*

tulifundisha Majaji, tulifundisha watu wa mahakama na hii yote ilitokana na *recommendation* ya *delay of disposal of civil suit* ya mwaka 1986.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna ripoti ya Tume imetolewa hapa kuhusu watoto na sheria ya watoto tayari tumetunga ripoti ya Tume ilitolewa hapa kuhusu *e-commerce* na *cyber, Crime in Tanzania* mwisho imepelekea marekebisho katika sheria ya ushahidi. Ni kweli kwamba labda Waheshimiwa hawa walikuwa wanataka ile ripoti yote mapendekezo yake yote yatolewe na yatangazwe kwamba tunatunga sheria ya watoto kutokana na *recommendation* ya Tume, lakini Tume ya idara ya Serikali na Tume kazi yake ni kuishauri Serikali, sasa Tume inatoa ushauri Serikali inatekeleza hakuna haja ya kutangaza kwamba hii tumefanya kwa sababu Tume imesema, hii tumefanya kwa sababu Tume ili *recommend*, Tume ina *recommend* tena wakiona kama ni jambo analeta kwenye *miscellaneous* anaweza akatoa *government notice* na tunaweza tukatunga sheria ama kubadilisha sheria ambazo zipo. (*Makofi*)

Pia iliulizwa kwa nini mradi wa maboresho ya mfumo wa madai yaani *civil justice* chini ya *BEST* unachelwa. Mradi huu mchakato wake unacheleweshwa na taratibu tu za upatikanaji wa mshauri mwelekezi ambazo zimebekwa na Benki ya Dunia wote mnafahamu matatizo tunayoyapata katika kutekeleza miradi yetu hasa ile ambayo inafadhiliwa na Benki ya Dunia. Utaratibu wao ni mrefu sana mara nyingi unachelewa, sasa kwa hili limechelewa lakini tumeshampata na taarifa yake ya awali itawasilishwa tarehe 12 Julai, 2010. Kwa hiyo, tunategemea baada ya hapo tutaendelea vizuri na mradi huu.

Mheshimiwa Devota Likokola, naona wataalam wangu waliandika Deodata sasa na mimi likawa linanichanganya kwa sababu nakufahamu wewe ni Devota, sasa nikawa nasema huyu Mbunge simjui. Mheshimiwa Devota Likokola Mbunge wa Viti Maalum ye ye ali sema Serikali kutoa tafsiri na mafunzo ya sheria mbalimbali hasa zile zinazowahusu sana wanawake na makundi maalum. Wanawake wengi wanahitaji kujua sheria za mirathi na sheria za ndoa na sheria za kuzuia ukatili wa binadamu na sheria hususan ukatili kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, nafikiri ni jambo nzuri na Serikali kupitia kwanza Tume ya Kurekebisha Sheria tumefanya tafsiri ya sheria mbalimbali kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu na kuhusu mafunzo ya sheria, tume hiyo inatoa pia elimu ya sheria kwa umma kupitia vyombo vya habari, nafikiri ni kila Jumanne, kipindi chao kiko asubuhi kwa muda wa saa karibu saa tatu ili kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria mbalimbali na mambo mbalimbali ambayo wananchi wanakuwa wanauliza na pale kunakuwa na *interaction* kati yao pamoja na watoa mada. Kubwa lilizungumzwa na wachangiaji wengine wengi akiwemo Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, ni kuhusu mahakama ya kazi hili nimelisemea asubuhi, nimesema wazi wazi kwamba Serikali haina kipingamizi, haikatazi, haizui uanzishwaji wa Mahakama ya Kadhi, lakini mahakama ni suala la imani, dini haiwezi kuanzishwa na mtu ambaye sio Muislamu, ni vigumu kuanzishwa na Serikali ambayo haina dini, itakuwa si Mahakama ya Kadhi tutakuwa tunafanya utani, Mahakama ya Kadhi itaanzishwa na waislamu wenywewe na hivi sasa kama nilivyo sema wako kwenye mchakato wa kufanya hivyo na mimi nasubiri

watakapoleta na mimi jukumu langu ni kuhakikisha tu kwamba zile sheria ambazo zitatumika katika mahakama hizo si zile ambazo zitakwenda kinyume na haki za binadamu si zile ambazo zitakwenda kinyume na kadhalika. Lakini vinginevyo ruksa na Mahakama ya Kadhi wenyewe wanaendelea na mchakato huo hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Fatma Maghimbi, alizungumzia tena maslahi ya Wanasheria wa Tume ya Kurekebisha Sheria, hili nilijaribu kulieleza hata kwenye Kamati kwamba kwa kweli hawa hawatambuliki kama *State Attorneys* na sisi baada ya kukubali ukweli huo tumeamua basi kuangalia jambo hili kutoka *angle* nyingine kwamba tuwaweke sawa na wale ma-*State Attorneys* lakini si lazima tuwaite ma-*State Attorneys* kama suala ni maslahi. Basi watayapata maslahi hayo pale pale walipo bila kuitwa ma-*State Attorneys* kwa sababu kuitwa ma-*State Attorneys* kunatawaliwa na sheria tofauti na sheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaajiri, Mwanasheria Mkuu anasimamia maadili ya ma-*State Attorneys* wake, hawa wanaajiriwa na chombo kingine kiko chini ya sekta ya sheria lakini si chombo ambacho kiko chini ya *Attorney General*. Kwa hiyo, kama ni suala la maslahi hilo tumeshaanza kulifanya kazi na *Chief Secretary*, tuko katika mchakato wa kuhakikisha kwamba wanafikishwa pale lakini wakibakia kama wanasheria katika Tume ya Kurekebisha Sheria. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wale wanasheria wa *RITA* ambao wansemekana wapo waliobakia chini ya *Administrator General* wanaitwa *State Attorneys* na wako ambao sasa wako wameajiriwa na *RITA* wao hawaitwi *State Attorneys* tunasema ni suala tu la *RITA*, waandike barua kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakiomba wale Wanasheria wanaowajiri wao lakini wanafanya kazi za Ma-*State Attorney* wafikiriwe kama Ma-*State Attorneys*.

Mheshimiwa Spika, naomba kama nilivyosema muda wangu ni mdogo na mambo ya kuzungumza ni mengi tutayaandika haya yote na tutawagawia Waheshimiwa Wabunge na nafikiri nimalizie tu kwa kusema kuwa nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao yote ambayo ni mizuri, imeboresha na inaendelea kuimarisha sekta hii ya sheria, nimeshukuru sana wameona mapungufu tuliyokuwa nayo na wametuambia, mtu anayekuambia upungufu wako ni mtu mzuri sana kuliko yule ambaye hakuambii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kukushukuru sana wewe mwenyewe kwa kazi nzuri ambayo umeifanya katika kipindi cha miaka yote mitano na mimi nimejifunza mengi sana kutoka kwako na kuombea heri, uende kule Urambo na wananchi wa Urambo watumie busara ambayo kama sisi tunayo wakurudishe tena katika Bunge hili na uendelee kuwa Spika kwa kipindi kingine ili tuendelee kwa kasi na viwango ambavyo tayari umeshakwishavionyesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kuwashukuru wananchi wa Nachingwea kwa ushirikiano mkubwa sana ambao wamenipa na aliyojasema Mheshimiwa Shibuda nina hakika wameyasikia, usiache mbachao kwa msala upitao, tunarudi tena Nachingwea

nategemea watatuonyesha tena imani ile ile ambayo walituonyesha mwaka 2005 kwa sababu tumewatumikia vyema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno yote hayo naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

KUHUSU UTARATIBU

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, naomba kutumia Kanuni ya 77(2).

SPIKA: Endelea.

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 77(2) ninasimama kukupa taarifa kwamba ninawasiwasi kwamba *quorum* yetu hapa ndani haitoshi, kama inavyotakiwa na Kifungu cha 77(1) na nitasoma pia Kifungu cha 100(1).

Kifungu cha 77(1) kinasema; “Akidi kwa kila kikao cha Bunge wakati wa kufanya maamuzi itakuwa ni nusu ya Wabunge wote, kama ilivyofafanuliwa katika Ibara ya 94 ya Katiba isipokuwa kwamba idadi hiyo haitahusu hoja kuhusu uamuzi wa kubadilisha masharti yoyote ya Katiba kwa mujibu wa Ibara ya 98 ya Katiba.”

Mheshimiwa Spika, hatua tunayoingia sasa inaelezwa na Kifungu cha 101(1) ambacho kinasema; “Katika Kamati ya Matumizi, Mwenyekiti atawahoji wajumbe kuhusu kifungu kimoja kimoja cha Makadirio ya Matumizi ya Mwaka na kila kifungu kitaafikiwa peke yake.”

Sasa kwa kutazama tu hapa ndani inaelekea kwamba idadi yetu haizidi 60 na Wabunge 60 sio nusu ya Wabunge wote, tunaomba kama Kanuni zinavyoendelea mbele iwapo Spika ataangalia basi naomba Spika aangalie nini kinatakiwa kifanyike ili tufanye maamuzi kwa mujibu wa Katiba yetu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana kwa hoja, ni bahati mbaya sana yote uliyosema ni sahihi tu, ila tu kuhusu idadi ya Wabunge hesabu yako wewe nadhani ni tofauti kidogo, Wabunge walioko ni kama nusu hivi ninavyowaona. (*Makofi*)

Usitazame kwa haraka haraka hovyo hovyo, na inasikitisha kwamba Wabunge wa Upinzani ni watano tu, kwa hiyo, kama ninyi mmeamua kugoma ili muweze kuharibu hii hoja basi Spika hawezи kuwasaidia ili uovu mnaotaka kuufanya ufanikiwe. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, kwa maelezo hayo namshukuru sana Mheshimiwa Waziri na ahsante kwa kunitakia mema. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa hivi ni kwamba hoja ilishatolewa na iliungwa mkono lakini kwa mujibu wa Kanuni ya 100, 101, 102, 103 na 104 inabidi tupitie katika utaratibu unaofuata ili tuweze kufika mwisho, kwa hiyo, namuita sasa Katibu ili atuweke katika utaratibu unaohusika.

SPIKA: Na bahati nzuri wameendelea kuongezeka kwa hiyo mambo yanazidi kuwa mazuri. Katibu Kutupitisha kwenye vifungu sasa. (*Kicheko*)

KAMATI YA MATUMIZI

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama

| | |
|---|----------------|
| Kifungu 1001 - <i>Administration and General...</i> | Sh.489,389,200 |
| Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts...</i> | Sh. 86,425,000 |
| Kifungu 1003 - <i>Procurement Management Unit</i> | Sh.18,509,440 |
| Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> | Sh.12,376,000 |
| Kifungu 1005 - <i>Recruitment, Appointment and Confirmation</i> | Sh.183,496,360 |
| Kifungu 1006 - <i>Ethics and Discipline Section</i> | Sh.186,905,000 |

(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

| | |
|--|------------------|
| Kifungu 1001 - <i>Administration and Human Resource Management</i> | Sh. 2,162,805,00 |
| Kifungu 1002 - <i>Finance and Account Unit</i> | Sh. 529,184,000 |
| Kifungu 1003 - <i>Planning Division</i> | Sh. 656,608,000 |
| Kifungu 1004 - <i>Internal Audit Unit</i> | Sh. 447,873,000 |
| Kifungu 1005 - <i>Information, Education and Communication</i> | Sh.336,219,000 |
| Kifungu 1006 - <i>Legal Registry Unit</i> | Sh.340,902,000 |
| Kifungu 1007 - <i>Procurement Management Unit</i> | Sh.343,576,000 |
| Kifungu 1008 - <i>Research and Library Service Unit</i> | Sh.375,202,000 |
| Kifungu 1009 - <i>Management Information System Unit</i> | Sh.445,128,000 |
| Kifungu 2002 - <i>Public Prosecution</i> | 0 |
| Kifungu 2003 - <i>Legislative Drafting</i> | Sh.1,199,401,000 |
| Kifungu 2004 - <i>Zonal Office Arusha</i> | 0 |
| Kifungu 2005 - <i>Zonal Office - Dodoma</i> | 0 |
| Kifungu 2006 - <i>Zonal Office - Dar es Salaam</i> | 0 |
| Kifungu 2007 - <i>Zonal Office - Iringa</i> | 0 |
| Kifungu 2008 - <i>Zonal Office - Moshi</i> | 0 |

| | |
|---|---|
| Kifungu 2009 - <i>Zonal Office</i> - Kagera.... | 0 |
| Kifungu2010 - <i>Zonal Office</i> - Mbeya.... | 0 |
| Kifungu 2011 - <i>Zonal Office</i> - Mtwara.... | 0 |
| Kifungu 2012 - <i>Zonal Office</i> - Mwanza.... | 0 |
| Kifungu 2013 - <i>Zonal Office</i> - Ruvuma.... | 0 |
| Kifungu 2014 - <i>Zonal Office</i> - Sumbawanga.... | 0 |
| Kifungu 2015 - <i>Zonal Office</i> - Tabora.... | 0 |
| Kifungu 2016 - <i>Zonal Office</i> - Tanga.... | 0 |

Kifungu 3001 - *Civil and International Law*

Division.....Sh.1,688,489,000

Kifungu 4001 - *Constitutional Affairs and Human*

Rights.....Sh.953,455,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko
yoyote*)

Fungu 18 – Mahakama Kuu

| | |
|--|-------------------|
| Kifungu 1001 <i>Administration and General (RHC)</i> | Sh.3,813,878,000 |
| Kifungu 1002 <i>Arusha Zone</i> | Sh. 477,260,000 |
| Kifungu 1003 <i>Dar es Salaam Zone</i> | Sh. 2,524,725,000 |
| Kifungu 1004 <i>Dodoma Zone</i> | Sh. 387,968,000 |
| Kifungu 1005 <i>Mbeya Zone</i> | Sh. 462,887,000 |
| Kifungu 1006 <i>Iringa Zone</i> | Sh. 330,185,000 |
| Kifungu 1007 <i>Mtwara Zone</i> | Sh. 392,116,000 |
| Kifungu 1008 <i>Mwanza Zone</i> | Sh. 580,651,000 |
| Kifungu 1009 <i>Songea Zone</i> | Sh. 344,553,000 |
| Kifungu 1010 <i>Tabora Zone</i> | Sh. 548,654,000 |
| Kifungu 1011 <i>Sumbawanga Zone</i> | Sh. 368,008,00 |
| Kifungu 1012 <i>Bukoba Zone</i> | Sh. 370,530,000 |
| Kifungu 1013 <i>Tanga Zone</i> | Sh. 332,185,000 |
| Kifungu 1014 <i>Moshi Zone</i> | Sh. 378,516,000 |
| Kifungu 1016 <i>Resident Magistrate Courts</i> | Sh. 5,932,208,000 |

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko
yoyote*)

Fungu 19 – Mahakama za Wilaya

| | |
|--|--------------------|
| Kifungu 1001 <i>Administration and General</i> | Sh. 1,762,977,516 |
| Kifungu 1002 <i>District Courts</i> | Sh. 4,288,570,550 |
| Kifungu 1003 <i>Primary Court</i> | Sh. 12,268,636,934 |

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko
yoyote*)

Fungu 35 – Divisheni ya Mashtaka

| | |
|--|-------------------|
| Kifungu 2002 <i>Public Prosecutions Division</i> | Sh. 1,519,739,000 |
| Kifungu 2004 <i>Zonal Office Arusha</i> | Sh. 443,351,000 |
| Kifungu 2005 <i>Zonal Office Dodoma</i> | Sh. 400,044,000 |
| Kifungu 2006 <i>Zonal Office Dar es Salaam</i> | Sh. 763,737,000 |
| Kifungu 2007 <i>Zonal Office Iringa</i> | Sh. 171,688,000 |
| Kifungu 2008 <i>Zonal Office Moshi</i> | Sh. 362,012,000 |
| Kifungu 2009 <i>Zonal Office Kagera</i> | Sh. 274,629,000 |
| Kifungu 2010 <i>Zonal Office Mbeya</i> | Sh. 389,701,000 |
| Kifungu 2011 <i>Zonal Office Mtwara</i> | Sh. 258,734,000 |
| Kifungu 2012 <i>Zonal Office Mwanza</i> | Sh. 644,357,000 |
| Kifungu 2013 <i>Zonal Office Ruvuma</i> | Sh. 216,858,000 |
| Kifungu 2014 <i>Zonal Office Sumbawanga</i> | Sh. 173,286,000 |
| Kifungu 2015 <i>Zonal Office Tabora</i> | Sh. 421,267,000 |
| Kifungu 2016 <i>Zonal Office Tanga</i> | Sh. 392,986,000 |
| Kifungu 2017 <i>Zonal Office Shinyanga</i> | Sh. 229,569,000 |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko
yoyote)*

Fungu 40 - Mahakama

| | |
|---|-------------------|
| Kifungu 1001 <i>Administration and General</i> | Sh. 6,925,449,000 |
| Kifungu 1002 <i>Finance and Accounts Unit</i> | Sh. 400,250,000 |
| Kifungu 1003 <i>Internal Audit Unit</i> | Sh. 332,834,000 |
| Kifungu 2001 <i>High Court</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2002 <i>Court of Appeal Dar es Salaam</i> | Sh. 2,279,046,000 |
| Kifungu 2003 <i>Arusha Zone</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2004 <i>Dar es Salaam Zone</i> | Sh.0 |
| Kifungu 2005 <i>Dodoma Zone</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2006 <i>Mbeya Zone</i> | Sh.0 |
| Kifungu 2007 <i>Mtwara Zone</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2008 <i>Mwanza Zone</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2009 <i>Tabora Zone</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2010 <i>Tanga Zone</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2011 <i>Primary Court</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2012 <i>District</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2013 <i>Kagera Zone</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2014 <i>Ruvuma Zone</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2015 <i>Moshi Zone</i> | Sh. 0 |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko
yoyote)*

Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

Kifungu 1001 *Administration and General*Sh. 3,397,095,000

MWENYEKITI: Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Martha M. Mlata, Mheshimiwa *Engineer* Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Diala M. Chilolo, Mheshimiwa Dr. Willibrod P. Slaa, Mheshimiwa Benson M. Mpesa na Mheshimiwa John Paul Lwanji.

Tutaanza na Mbunge wa Kigoma Mjini Mheshimiwa Peter Serukamba.

MHE. PETER J. SERUKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, niliandika kwenye maelezo yangu, nataka kujua Wizara hii ina mpango gani wa kujenga Mahakama za Rufaa kwenye Mikoa ya Tanzania *particularly* Kigoma ukizingatia watu wanapata shida sana wanapotafuta haki zao kwenda Tabora ukizingatia usafiri sasa hivi siyo mzuri sana wanatumia pesa nyingi sana.

Kwa hiyo, watu wenyewe kipato cha chini ni kazi sana kupata haki yake ya rufaa. Nataka kujua tu kwa Mheshimiwa Waziri wana mpango gani ili tuweze kuwasaidia wananchi hawa hasa wanaotoka maeneo ya Kigoma?

MWENYEKITI: Una maana Mahakama Kuu? Ni kweli inafanya shughuli za rufaa lakini ukitamka rufaa moja kwa moja inaleta sura ile nyingine.

Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Peter Serukamba, na kufafanua kwamba kwa sasa tuna mpango wa kujenga Mahakama Kuu katika kila Mkoa na kama nilivyo sema tumeanzia kwa mwaka ujao wa fedha Singida, Mara na Mtwara tutakwenda kidogo kidogo kwa kadri fedha zinavyopatikana na *eventually* tutafika Kigoma.

Sasa Mahakama ya Rufaa kwa kawaida inazunguka tu ina *sit* moja iko Dar es Salaam kwa hiyo hatuwezi kujenga Mahakama ya Rufaa pale, tunachowezza kujenga ni Mahakama Kuu ambayo nayo tutaijenga kwa utaratibu huu wa kwenda kidogo kidogo *unless* kama ninavyo amini mwaka ujao labda Serikali itabidilisha mfumo wake wa Bajeti na tukapata pesa za kutosha basi tutaweza kujenga Mahakama Kuu Kigoma haraka iwezekanavyo.

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Martha Mlata!

MHE. MARTHA M. MLATA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi pia nikoo kwenye *sub vote* hiyo ya 1001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia nilikuwa nimezungumza kwamba pamoja na kwamba Serikali inaandaa Sheria mpya ya Ndoa pamoja na Mirathi kuja hapa Bungeni lakini nikasema mpaka sasa hivi kuna mamia ya wanawake wengi ambao wameondokewa na wenza wao na hawa wengine ambao wametalikiana na wenza wao

kesi zao ziko Mahakamani lakini bado wamekuwa hawatendewi haki kwa sababu hawana hata uwezo wa kuweka wanasheria.

Lakini Mheshimiwa Waziri wakati anajibu sijaona hata azungumze kidogo walau kuwapoza wanawake hawa kwa kuwafariji kwa maneno ya kuwatia moyo. Sasa ninaomba Waziri aweze kutamka neno lolote. Ahstante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, neno la faraja kwa wajane!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, neno la faraja kwa wajane ambao kesi zao ziko Mahakamani ni kwamba tutaongea na Jaji Mkuu ahakikishe kwamba kesi hizo zinafanyika haraka iwezekanavyo. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer Stella M. Manyanya*.

MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ametoa faraja sasa kuhusiana na kesi nyingi zinazowakabili wanawake ni kwamba kuna shughuli ambazo zinaendelea kwa vikundi vya akina mama au watu wengine kujitolea katika kuwasaidia wanawake hao katika kufuatilia kesi zao yaani wanakuwa kama Mawakili na kwa jina maarufu nasikia wanaitwa *Para Legal*.

Naomba nifahamu je, hao wanaofanya shughuli katika misingi hiyo wanafanya kwa sheria maalum au wanafanya tu kwa sababu ya kuweza kusaidia? Na kama hakuna sheria maalum je, Waziri ni lini utafikiria kuweka sheria ambayo itasaidia kuwalinda hao watu kwa kuwa wanasaidia sana hasa vijijini?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la hao wanaotoa huduma za sheria tuseme wako wa aina mbili, kuna wale ambao wanakwenda kwa kivuli cha *Legal Aid* ambao kuna *NGOs* mbalimbali na hata wakati mwingine *Tanganyika Law Society* huwa wanafanya hivyo yaani wanatoa msaada wa sheria kwa watu ambao hawawezi kuajiri mawakili.

Lakini kuna wengine hawa ambao wanaitwa *Para Legals*, hawa tuliwatambua na sisi wapo sehemu nyingi hawaruhusiwi kuingia Mahakamani lakini mara nyingi huwa wanakaa *around* nje ya Mahakama pale na ukitoka tu basi anakuambia wewe ukienda kaseme hivi na hivi. Sasa tunatambua mchango wao na ndiyo maana Tume ya Kurekebisha Sheria ilifanya utafiti mkubwa wa kuhusu uanzishwaji wa Sekta hii ya *Para Legal* na ilitoa mapendekezo na hivi sasa ninavyozungumza na ndiyo maana iliingia kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa hivi ipo katika ngazi ya *Cabinet* kutolewa uamuzi ili sheria itungwe kwanza ya kuwatambua na pia kuweka viwango na watafanya kazi wapi na kama *wata-charge* basi *wa-charge* kiasi kidogo isiwe sawasawa na *Advocate*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, imo katika mchakato.

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa ufanuzi Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Diana Chilolo.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nachangia mchango wangu asubuhi nilikuwa nimezungumzia suala la Mahakama ya Mwanzo ya Utetemi kwamba hiyo Mahakama imeshakamilika, ni nzuri sana lakini ni mwaka mzima haijafunguliwa tatizo ni samani tu. Sijui Mheshimiwa Waziri anasema nini kuhusu Mahakama hii na itaendelea kukaa hivyo mpaka lini?

Lakini hata hivyo, namshukuru sana kwa kutenga fedha kwa ajili ya kuanza kujenga Mahakama Kuu, naamini kuititia hotuba yake atakuwa amekonga nyoyo za Wanasingida. Namshukuru sana na ninaomba majibu. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Mahakama ya Utetemi ambayo imekamilika lakini milango imefungwa.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mahakama ya Utetemi ni sawasawa na suala la Mahakama iliyopo kwa Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa pale ambazo zimekamilika na ni Mahakama kubwa na nzuri lakini bado hazijaanza kutumika. Mimi mwenyewe bahati nzuri nimewahi kuziona hizi Mahakama nikavutiwa sana na niliporudi tu nikazungumza na Jaji Mkuu nikasema basi pindi mtakapopata fedha mfanye vitu viwili vifuatavyo; moja, Mahakama ya ile ya Karatu kwa Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa itumike kama *District Court* kwa sababu ni kubwa sana pale hata vikao vya *High Court* vinaweza kukaa na zipelekwe hizo samani na apelekwe Hakimu haraka.

Hili sasa wenzangu wanalfanyia kazi lakini bado hawajapeleka na niliagiza hivyo hivyo kwa Mahakama ya Utetemi kwamba zipelekwe samani pale na Mahakama ile iweze kufanya kazi. Ninachoweza kusema ni kwamba kwa Bajeti hii tunayopata leo kama mtaipitisha basi kazi hii itafanyika haraka iwezekanavyo ili Mahakama hizo kwa kweli ziweze kufanya kazi na kutoa huduma kwa wananchi.

MWENYEKITI: Ahsante sana, Mheshimiwa Mpesa!

MHE. BENSON M. MPESYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi *programme* hiyo hiyo 10, *sub vote 1001*, kifungu kidogo 210100 Mshahara wa Waziri. Sina shida kabisa na mshahara wa Waziri isipokuwa tu nataka azingatie kile ambacho nitamueleza.

Katika mchango wangu wa maandishi nimeeleza juu ya adha kubwa wanayoipata wazee wa Mabaraza hasa Mahakama ya Mwanzo ya Mbeya Mjini na Mwanjelwa. Wazee hawa wakati ule kesi ilikuwa ni shilingi 1,500, wazee hawa wamekuwa na malimbikizo wanayoidai Serikali takribani miaka miwili hawalipwi na nashukuru kwa nia nzuri ya Serikali ambapo imepandisha sasa kuifanya kesi iwe shilingi 5,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kudaiwa na Wazee wa Baraza ambao tunategemea watoe haki shilingi 1,500 inatia simanzi kidogo. Namuomba Waziri atueleze kwa kupandisha kiwango hiki anakuja na mfumo gani ambao utahakikisha kwamba Mzee wa Baraza anapomaliza kesi zake analipwa bila kukopwa na wengi hawa umri wao umekwenda kuwakopa ni aibu. Ahsante.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli si vizuri kuwakopa wazee hawa, hali zao hawastahili kukopwa hasa kiasi hiki kidogo cha pesa. Kinachotokea ni kwamba pesa hizi zinatoka Hazina zinakuja kama *OC* na zinapelekwa kila mwezi kwenye *Zone* kwa *Judge Incharge* halafu na yeze anazipeleka kule kwenye Mahakama inayohusika. Sasa zoezi hili linaweza kuwa linachukua muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini inawezekana pia vilevile pesa hizi zikatumika kwa shughuli nyingine kinyume na kuwalipa wale wanaostahili, sasa nataka na mimi nisema hapa kwamba kwanza pesa hizi zipelekwe haraka iwezekanavyo, lakini pili zisitumike kwa kazi nyingine yoyote isipokuwa kuwalipa wazee, iwe *first charge* pesa zikifika kwa Hakimu *incharge* kitu cha kwanza ahakikishe wazee hawa wanalipwa shilingi 5,000 yao halafu ndiyo wajinunulie mafuta na karatasi na vitu vingine vya kuendeshea Mahakama. (*Makofi*)

MWENYEKIDI: Ahsante sana na nadhani watusika wamesikia. Mheshimiwa John Lwanji.

MHE. JOHN P. LWANJI: Mheshimiwa mwenyekiti, ahsante. Nami katika mchango wangu nilitaka kujua kuhusu ukarabati wa Mahakama ya Ukimbu, mwaka wa fedha 2009/2010.....

MWENYEKIDI: Mahakama ya wapi?

MHE. JOHN P. LWANJI: Mahakama ya Ukimbu Mgandu. Mwaka wa fedha 2009/2010 zilitengwa shilingi milioni 70 na watusika kama Hakimu wa Wilaya tuliwaarifu, sasa napenda kujua kwa nini Mahakama hiyo haijakarabatiwa? Sikupata jibu.

MWENYEKIDI: Mahakama ya Ukimbu!!

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, kama unavyoona ni vigumu kulitamka labda na mimi kumbukumbu zangu siyo sahihi lakini kulikuwa na maelekezo kwamba Mahakama hii pamoja na nyingine ambayo iko kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mgana Msindai, zikarabatiwe katika mwaka huu wa fedha tunaoumaliza sasa. Sasa kama haijakarabatiwa kama unavyosema Mheshimiwa basi naomba unipe muda nilifuatilie hilo litakuwa la kwangu kusimamia na kuhakikisha kwamba ahadi hii tulioiweka ya kukarabati Mahakama hiyo ya Ukimbu tunaitekeleza.

MWENYEKIDI: Ahsante sana. Mheshimiwa Dr. Willibrod Slaa.

MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, na mimi niko programu hiyo hiyo ya 10, *sub vote 1001* na *sub vote* ndogo zaidi ya 2010100 mshahara wa Waziri sina tatizo na mshahara wa Waziri lakini napenda nitumie kifungu hiki kwanza kumshukuru kwa Mahakama ya Karatu ambayo ilikuwa Mahakama ya Mwanzo na imegeuzwa sasa kuwa Mahakama ya Wilaya. Namshukuru kwa hilo. (*Makofi*)

Napenda kupata ufanuzi mwaka 2006 wakati wa Bajeti hivi hivi nilikuwa nimemuuliza Waziri aliyemtangulia uwezekano wa kubadilisha utaratibu wetu wa uchaguzi kutoka siku ya Jumapili kuwa siku ya katikati ya wiki. Wizara wakati ule ikajibu kwamba watafanya utaratibu na utafiti lakini hatukupata majibu na sasa Tume imetangaza tarehe 31 Oktoba, 2010. Nataka ufanuzi je, tatizo ni Sheria, Katiba au ni kitu gani kwa sababu kuna wenzetu katika nchi nyine wanaotumia siku ya katikati ya wiki ambayo haigusi imani ya dini yoyote au ya dhehebu lolote na vilevile kitu hiki kinakuja mara moja tu katika miaka mitano.

Tatizo ni nini kufanya siku moja tu katika miaka mitano ili wananchi waweze kupiga kura kwa uhuru bila kuzuia haki yao ya kwenda kwenye sehemu zao za ibada na lakini wapate pia muda wa kutosha kuondoa msongamano amba kwa kawaida huwa unatokea watu wakitoka kwenye madhehebu ya dini huwa wanasongamana na hii inafanya utaratibu wa kupiga kura usogee mpaka jioni zaidi, baadaye wanabanana kwenye mstari na uchaguzi unaendelea mpaka kwenye giza suala ambalo linafanya hata hesabu kuchelewa. Tatizo ni nini hasa linalotufanya tushindwe kupanga siku ya katikati ya wiki iwe siku ya kupiga kura? (*Makofi*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Lakini sijui kama hili ni tatizo kwa sasa kwa sababu nadhani muda unaopatikana kwenda kupiga kura unatosha siku ya Jumapili. Lakini kama anavyosema yeye hii ni siku moja tu katika miaka mitano na ni siku moja tu katika miaka mitano ambayo muumini pia anaweza kukosa kwenda kusali ili akatimize wajibu wake wa kupiga kura.

MWENYEKITI: Na ndivyo imekuwa tangu Uhuru kwa hiyo sioni kama ni jambo jipya kabisa limepandishwa moto na baadhi ya jamaa, maana yake ungejaribu ijumaa matatizo, ukijaribu Jumamosi nayo ni Sabato sasa sijui mwisho utafika wapi. Mimi nadhani, ahsante Mheshimiwa Waziri.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

| | |
|---|------------------|
| Kifungu 1002 <i>Finance and General</i> | Sh. 301,830,000 |
| Kifungu 1003 <i>Policy and Information Service</i> | Sh. 478,254,000 |
| Kifungu 1004 <i>Internal Audit Unit</i> | Sh. 102,419,000 |
| Kifungu 1005 <i>Information Education and Communication</i> | Sh. 150, 914,000 |
| Kifungu 1006 <i>Procurement Management Unit</i> | Sh. 162,686,000 |
| Kifungu 1007 <i>Management Information System Unit</i> .. | Sh. 259,725,000 |

Kifungu 2004 *Public Legal Services Unit*..... Sh. 304,959,000
Kifungu 2005 *Legal Reform Unit*..... Sh. 274,176,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu

Kifungu 1001 *Administration and General*Sh. 1,669,556,600
Kifungu 1002 *Finance and Accounts*.....Sh. 140,537,000
Kifungu 1003 *Internal Audit Unit*.....Sh. 55,371,000
Kifungu 1004 *Legal Service*Sh. 167,529,800
Kifungu 1005 *Procurement Unit*.....Sh. 97,214,000
Kifungu 1006 *Management Information Unit*.....Sh.136,943,000
Kifungu 2001 *Administrative Justice*.....Sh.559,608,000
Kifungu 2002 *Human Rights*.....Sh.318, 847,000
Kifungu 2003 *Research and Documentation*.....Sh. 149,188,500
Kifungu 2004 *Public Education and Training*.....Sh. 155,539,100
Kifungu 3001 *Zanzibar Office*Sh. 210,118,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Kifungu 1001 *Administration and General*Sh. 1,335,218,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 60 – Mahakama ya Kazi

Kifungu 1001 *Administration and General*.....Sh. 1,221,957,680
Kifungu 2001 *Arusha Zone*.....Sh. 7,445,320
Kifungu 2002 *Dar es Salaam Zone*.....Sh. 48,180,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 64 – Mahakama ya Biashara

Kifungu 1001 *Administration and General*.....Sh. 1,117,468,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 90 – Mahakama ya Ardhi

Kifungu 1001 *Administration and General*Sh. 1,083,485,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MATUMIZI YA MAENDELEO

Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama

Kifungu 1001 *Administration and General*Sh. 0

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

| | |
|---|-----------------|
| Kifungu 1001 <i>Administration and General</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 1002 <i>Finance and Accounts Unit</i> | Sh.0 |
| Kifungu 1003 <i>Planning Division</i> | Sh.0 |
| Kifungu 1004 <i>Internal Audit Unit</i> | Sh.0 |
| Kifungu 1005 <i>Information, Education and Communication</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2002 <i>Public Prosecution</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2003 <i>Legislative Drafting</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 3001 <i>Civil and International Law Division</i> | Sh. 420,000,000 |
| Kifungu 4001 <i>Constitutional Affairs and Human Rights</i> | Sh. 0 |

(*Vifungu viliwyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, mkisikia kifungu hakikutengewa fedha kwenye vitabu hivi mara kwa mara ni mabadiliko ya uwasilishaji wa takwimu za malipo au vifungu. Kwa mfano, tulipopitia Kitabu cha Pili baadhi ya vifungu vidogo vilivyo husu Mahakama katika Mikoa vilikuwa vimejulimshwa tayari katika Fungu Kuu la Mahakama Kuu, kwa hiyo, havikuonekana utadhani havikutengewa fedha lakini fedha ipo.

Basi ni hivyo hivyo kwa haya tunayoyaona. Endelea Katibu.

Fungu 18 – Mahakama Kuu

Kifungu 1001 *Administration and General*.....Sh. 0
Kifungu 1016 *Resident Magistrative Courts*.....Sh.0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 35 – Divisheni ya Mashtaka

Kifungu 2002 *Public Prosecutions Division*.....Sh. 1,500,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

MWENYEKITI: Maelezo yangu yalikuwa yanahusu Makadirio ya Matumizi ya Kawaida, kwenye haya ya Maendeleo inawezekana kabisa hakuna mradi au mradi ulikwisha kwa hiyo, hakuna tena fedha za Maendeleo kwa mwaka husika. Tunaendelea!

Fungu 40 - Mahakama

Kifungu 1001 *Administration and General*.....Sh. 28,175,554,000

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *Sub vote 1001* kwenye namba 6312 inayohusiana na *Construction and Rehabilitation of Primary Court Buildings.*

Sasa nataka Mheshimiwa Waziri anisaidie kwa sababu kwenye mchango wangu wa maandishi nilizungumzia juu ya ukarabati wa Mahakama ya Mwanzo ya Kawe ambayo kwa kweli inatia aibu sana ukizingatia vigogo wote wanakaa kule mpaka ikaonyeshwa na *Ze Comedy*. Sasa nataka kujua katika hili fungu ile Mahakama yenu ya Mwanzo ya Kawe kule ipo ama haipo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir unafanya nini hapo? Mheshimiwa Waziri Mahakama ya Kawe! (*Kicheko*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Waziri simuoni Mbunge wa Kawe lakini nataka kusema kwamba Mahakama ya Kawe tutaikarabati kwa pesa hizi. (*Makofi*)

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Kifungu 2001 *High Court*.....Sh. 0

Kifungu 2002 *Court of Appeal Dar es Salaam*.....Sh. 0

Kifungu 2011 *Primary Courts*Sh. 0

Kifungu 2012 *District Courts*.....Sh.0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria

| | |
|---|-------------------|
| Kifungu 1001 <i>Administration and General</i> | Sh. 1,200,000,000 |
| Kifungu 1002 <i>Finance and Accounts</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 1003 <i>Policy and Information Services</i> | Sh. 293,578,000 |
| Kifungu 1004 <i>Internal Audit Unit</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 1005 <i>Information, Education and Communication</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 1006 <i>Procurement Management Unit</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 1007 <i>Management Information System</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2004 <i>Public Legal Services Unit</i> | Sh. 0 |
| Kifungu 2005 <i>Legal Reform Unit</i> | Sh. 3,502,857,000 |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko
yoyote)*

Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu

| | |
|--|-----------------|
| Kifungu 1001 <i>Administration and General</i> | Sh. 381,230,000 |
| Kifungu 1004 <i>Legal Services</i> | Sh. 0 |

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko
yoyote)*

| | |
|--|-----------------|
| Kifungu 2002 <i>Human Rights</i> | Sh. 269,969,000 |
|--|-----------------|

MHE. WILSON M. MASILINGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, nilikuwa nasubiri kwa nguvu zote kutaka kujua ufanuzi hapa.

Suala linalohusu haki za binadamu na binadamu wanaoishi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania nimevumilia kwingine kukuta hakuna hela lakini wafadhili wanatusaidia. Naomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria ya nchi hii, hata hapa tumekosa shilingi moja ya kuweka mpaka zitoke nje? Tatizo ni nini kwenye haki za binadamu? Naomba ufanuzi.

MWENYEKITI: Hizi kwenye maendeleo naona tunasaidiwa na *UNDP* lakini Mheshimiwa anauliza kwa nini hakuna fedha zetu wenyewe?

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri za kwetu wenyewe ziko kwenye Kitabu cha Pili kwa maana ya *OC*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri anasema mchango wa Serikali yetu ni katika Matumizi ya Kawaida na masharti mengi yako hivyo kwamba mtachangia mishahara labda ya wataalamu lakini mbia katika maendeleo atajenga kitu, ndiyo ubia wenyewe huo. (*Makofii*)

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko
yoyote)*

Kifungu 2003 Research and Documentation.....Sh. 182,356,000
Kifungu 2004 Public Education and Training.....Sh. 292,660,000

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Kifungu 1001 Administration and GeneralSh. 877,500,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 60 – Mahakama ya Kazi

Kifungu 100 Administration and General.....Sh. 1,824,356,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 64 – Mahakama ya Biashara

Kifungu 1001 Adimistration and General.....Sh. 562,459,000

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Fungu 90 – Mahakama ya Ardhi

Kifungu 1001 Administration and General.....Sh. 535,216,000

MHE. JOHN M. CHEYO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nataka kuuliza juu ya Mahakama hii na zaidi kuhusu majengo ya Mahakama na nilikuwa nategemea angalau mwaka huu baada ya Mheshimiwa Msajili kuja mbele ya Kamati ya PAC na akatoa malalamiko yake kwamba hakuna hata kiwanja cha kujenga Mahakama na ye ye ndiye anayeshughulikia mambo ya ardhi.

Sasa nilikuwa nategemea angalau mwaka huu baada ya sisi kutoa ushauri kwamba angalau kiwanja kikipatikana kungeonyeshwa na fedha hata kidogo hapa juu ya kujenga hii Mahakama angalau ijengwe Dar es Salaam kwa ajili ya kufanya shughuli zake ambazo ni muhimu sana ukizingatia malalamiko mbalimbali na umeonyeshwa hata takwimu ni nusu tu ya malalamiko ndiyo ambayo yanashughulikiwa kwa hivi sasa. Napenda kupata maelezo. (*Makofit*)

MWENYEKITI: Ushauri wa bure tu kwa Serikali mbona viwanja vingi Dodoma? Mnang'ang'ania kujenga Dar es Salaam tu yaani kitu kinachelewa kwa sababu unang'ang'ania kutafuta kiwanja Dar es Salaam, kwa nini? Kwa maoni yangu mimi mfumo mzima wa Mahakama ungeweza kuwa Makao Makuu ambayo ni Dodoma tu kama Bunge liliyvo. (*Makofi*)

Lakini hiyo ni Spika tu anayatoa mawazo yake mara moja moja, lakini Waziri mjibu Mheshimiwa John Cheyo. (*Kicheko*)

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa MwenyeKITI, nilitegemea Mheshimiwa John Cheyo angeniuiliza hili kwenye mshahara wa Waziri maana hapa ni mradi tu wa *BEST* na jinsi ya kuboresha Mahakama hii. Lakini suala hilo basi tumelizingatia na hili la kwako Mheshimiwa Spika mimi mwenyewe ndiye nilikuwa nalitetea hili pamoja ujenzi wa Mahakama ya Rufaa nilikuwa nafikiria ni vitu ambavyo vingeweza kufanyika Dodoma. Kwa hiyo, tutalizingatia na tutaangalia kama iwe Dodoma au Mahakama ya Ardhi ibaki Dar es Salaam tupate kiwanja pale tutajitahidi tufanye hivyo katika mwaka ujao wa fedha. (*Makofi*)

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

(*Bunge lilirudia*)

SPIKA: Katika hatua hii sasa namuita mtoa hoja Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ili atoe taarifa kuhusu kazi iliyofanyika kwenye Kamati ya Matumizi.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2010/2011 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba Makadirio haya sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa MwenyeKITI, naafiki! (*Makofi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2010/2011 yalipitishwa na Bunge*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, Waheshimiwa Wabunge hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ni ya kuliomba Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2010/2011. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nafurahi kutangaza kwamba Bunge la Jamhuri ya Muungano sasa limepitisha Makadirio ya Matumizi kwa Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2010/2011. Nawashukuru wote kwa kazi hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, nikumbushe tu kwamba kesho saa saba Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi yaani Wenyeviti wote 17 wa Kamati tukutane pale katika Ukumbi wa Spika kwa ajili ya kuzingatia kupanga shughuli zilizosalia za Bunge hili. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na kwa kuwa shughuli tulizopanga kwa leo zimefikia hatma yake naliahirisha sasa Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

(Saa 12.42 jioni Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumamosi, Tarehe 26 Juni, 2010 saa tatu asubuhi)